

Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tano - Tarehe 17 Juni, 2003

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 40

Sera ya Uandishi wa Habari

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Kwa kuwa inaonekana kwamba sasa hivi Chuo cha Uandishi wa Habari cha Serikali kilichopo hakiwezi kukidhi mahitaji ya wanafunzi walio wengi yaani nafasi kwenye chuo hicho ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi, hali iliyosababisha watu binafsi kwenye mitaa tofauti kuanzisha vyuo binafsi nya Uandishi wa Habari hivyo kuwa na Waandishi wengi wa Habari wa kujitegemea na baadhi yao hawafuati Maadili ya Uandishi ipasavyo kutokana na kupata mafunzo ya muda mfupi yanayoonyesha kwamba Waandishi hao wamepitia mafunzo tu ya Uandishi wa Habari badala ya kupatiwa mafunzo ya kina na ya muda mrefu kuhusu taaluma hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Sera ya Uandishi wa Habari takayotumiwa na Waandishi wote sambamba na kazi zao?

(b) Je, ni Waandishi wa Habari wangapi (wa kike/kiume) waliofaulu Diploma ya Habari kuitia chuo hicho tangu kianzishwe hadi sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Jimbo la Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo Sera ya Habari na Utangazaji ambayo hutumiwa na Waandishi wa Habari na Watangazaji katika kazi zao za kila siku tokea mwaka 1993. Sera hiyo hata hivyo ilikuwa na mapungufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuhuisha sera hiyo ya mwaka 1993 ili ilingane na wakati uliopo na hivyo kukidhi haja ya mabadiliko makubwa yaliyotokea duniani yakiwemo ya

utandawazi, sera za soko huria na ujenzi wa demokrasia, ambayo ni muhimu kuyaangalia na kuyazingatia hapa nchini.

Sera inayohuishwa ikikamilika na kupitishwa na Serikali, itaweka mazingira yatakayofanya vyombo vya habari vishamiri na kuviezeshesha kufanya kazi zao katika mazingira ya uhuru unaojali na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania.

Pia vitahimizwa kufuata kikamilifu miiko na maadili ya taaluma ya uandishi na utangazaji wa habari nchini, kwa mujibu wa sheria zilizowekwa, ili viimarike na viweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

(b) Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari waliofuzu na kupata Diploma ya Habari katika Chuo cha Uandishi wa Habari cha Serikali, yaani *TSJ*, tangu kianzishwe mwaka 1977 hadi 2002 ni Wanawake 188 na wanaume 392 jumla yao 580.

Mchangano ni kama ifuatavyo:-

| Mwaka | Jina la Kozi | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|------------------|--------------------|------------|------------|------------|
| 1977-1999 | Diploma ya Kawaida | 164 | 363 | 527 |
| 1998 - 2001 | Diploma ya Uzamili | 13 | 14 | 27 |
| 1999 - 2002 | Diploma ya Juu | 11 | 15 | 26 |
| JUMLA KUU | | 188 | 392 | 580 |

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba Sera ya habari ina mapungufu. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Vyuo vya Uandishi wa Habari vya Mitaani ambavyo hutoa mafunzo ya miezi mitatu mitatu ambayo hayatoshi kwa taaluma hiyo na yanachangia kudidimiza fani hii?

Pili, ni vigezo gani vinatumika katika kutoa vibali kwa vyuo kama hivyo? Ahsante sana.
(*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, kwanza nafikiri kwamba, kuwa na vyuo ambavyo vinatoa kozi fupi si makosa hata kidogo, bali vinasaidia kuimarisha taaluma ya habari. Kwa hiyo, mwenye kutaka taaluma anachagua aende kozi fupi za miezi mitatu, miezi sita, ya mwaka mmoja au Diploma. Ningependa niseme kwamba, si makosa kwa wenye vyuo kuwa na kozi fupi fupi za miezi mitatu, muhimu ni kuimarisha taaluma ile ili waandishi watoke pale na ujuzi wa kutosha.

Pili, vigezo inategemea kila chuo kuna vigezo maalum ambavyo vimewekwa na Serikali. Lakini cha msingi ni kwamba, lazima vyuo hivyo viwe na taaluma ambayo kwanza iangaliwe na Serikali na kudhibitishwa lakini la msingi ni kwamba, la zima Waandishi wa Habari wawe na taaluma ya uadilifu na ujuzi ili kukidhi haja hii ya Sera ya Uandishi wa Habari.

Kwa hiyo, la msingi ni kwamba kila chuo kinaangalia *syllabus* yake na kwa hiyo wahusika wanahakikisha kwamba, sera hii inafaa kwa ajili ya vyuo hivyo.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, labda nikumbushe tu

kwamba, kwa sababu sera inasisitiza angalau kila Wilaya iwe na Waandishi wa Habari, lakini kuna Wilaya nyingine hazina Waandishi wa Habari ikiwemo Kondo. Je, Waziri ana mipango gani ya kuziwezesha Wilaya nyingine zote zilizobaki ziwe na Waandishi wa Habari? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, katika sera yetu ambayo tumeiruhusu sasa hivi inasisitiza kwamba, lazima kila mwananchi apate haki ya kupata habari na kutoa habari na hii ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sera yetu hii itahimiza hivyo na Serikali inajitahidi kwa uwezo wake ikiwezekana kuanza katika Mikoa na baadaye kila Wilaya, kwa kutegemea hali ya uwezo wa Serikali katika kufanikisha jambo hili. Lakini nia yetu ni kuwezesha kila Wilaya inakuwa na Mwandishi wa Habari.

Na. 41

Viongozi Waliotembelea Mkoo wa Rukwa

MHE. PONSIANO D. NYAMI aliuliza:-

Kwa kuwa suala la Viongozi kutembelea wananchi ni muhimu kwa vile hupata fursa ya kujifunza mengi na hata kutoa hamasa kwa wananchi wenyewe:-

- (a) Je, ni Mawaziri wa Wizara zipi ambao wamekwishatemebelea Mkoo wa Rukwa tangu awamu ya tatu ianze uongozi wake mwaka 1995 hadi sasa?
- (b) Je, ni Mawaziri wa Wizara zipi ambao hawajatembelea Mkoo huo na kwa nini hasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mawaziri na Manaibu Waziri wa Wizara 12 walishafanya ziara 26 katika Mkoo wa Rukwa tangu awamu ya tatu ianze uongozi wake mwaka 1995 hadi sasa. Wizara hizo ni Ofisi ya Waziri Mkoo, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ujenzi.

(b) Waheshimiwa Mawaziri wengine hawajatembelea Mkoo wa Rukwa, kwa sababu walilazimika kutembelea Mikoa mingine, pia sambamba na kutekeleza majukumu mengine ya Kitaifa.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1995 mpaka mwaka 2003 tulipo leo ni muda mrefu. Je, kitendo cha Mawaziri wa Wizara nyingine kutotembelea Rukwa ni hali ile ile ya kutojali Mikoo huo kwa vile uko pembezoni na hauna maendeleo na pengine wanaona kwamba watapoteza muda wakienda katika Mikoo huo, hasa ukitalia maanani kwamba katika Mikoo mingine wanarudi mara mbili mbili au mara tatu tatu? (*Makofi*)

La pili, je, wanaona usumbufu kwenda katika Mkoo wa Rukwa kwa vile hakuna barabara kwa mfano barabara za lami na nyinyi zimechimbika sana, kwa hiyo wanaona kwenda huko itakuwa pengine ni kupata usumbufu bila sababu. Naomba wanieleze ni lini wanategemea sasa kuja kwa kusukumwa na Wizara yako? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) : Mheshimiwa Spika, nafahamu Mheshimiwa Nyami, anafahamu kwamba nchi hii ni kubwa, lakini anajua majukumu ya kila Wizara na sera zake na anajua ratiba za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM inavyohitaji Serikali kufanya kazi zake. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia tena Mheshimiwa Nyami

kwamba, pengine kama ningeleta orodha ya ziara hizo katika Mikoa yote, ungeweza ukaona wazi kwamba Mkoa wa Rukwa umepitiwa zaidi kuliko Mikoa mingine. (*Makofii*)

Suala la kutojali halipo, kutokopendelea halipo. Nchi ni moja na Serikali ni moja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi hakuna mtu ambaye atautenga Mkao wa Rukwa. Suala la usumbufu kwa sababu ya barabara mbaya halipo kwa sababu ziko barabara mbaya zaidi kuliko hiyo ya Rukwa na unajua jitihada za Serikali zinazofanywa hivi sasa katika kurekebisha barabara hiyo. Kwa hiyo, nataka uamini Mheshimiwa Nyami kwamba, Serikali inajitahidi, viongozi hawa wanajitahidi kufanya kazi yao kwa mujibu wa majukumu yao na utaratibu uliowekwa. (*Makofii*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa ziara zote mbili ambazo amezifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkoani Mbeya amepitia Mbeya Mjini akienda Mbozi na Rungwe; na kwa kuwa wananchi wa Mbeya Mjini na Wilaya nyingine zilizosalia wangetamani sana kumwona Rais anatembelea rasmi Wilaya hizo; je, Waziri yupo tayari kutubebea ombi hili alipeleke kwa Rais ili azitembelee Wilaya ambazo hazijatembelewa? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba, Rais ni Kiongozi wa Taifa na anao utaratibu wa kufanya ziara katika kutembelea Mkoa sambamba na kufanya kazi nyingine za ndani na nje. Wakati utakapofika kwa mujibu wa ratiba yake, naamini atatembelea katika Wilaya hizo za Mkoa wa Mbeya. (*Makofii*)

Na. 42

Baraza la Taifa la Vijana

MHE. ASHA A. NGEDE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo mwaka 1997 ilibuni na kuanza kuratibu mpango wa uanzishwaji wa chombo cha kuwaunganisha vijana wote Tanzania bila kujali itikadi zao za kisiasa ambapo mpango huo ulianzia *VETA Dar es Salaam*; na kwa kuwa chombo hicho mwaka 1998 huko Iringa kilifika hatua ya kupitisha rasimu ya Katiba yake na jina rasmi kwa kuitwa Baraza la Taifa la Vijana kama zilivyo nchi mbalimbali duniani:-

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza mpango huo umefikia wapi?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa, kucheleweshwa kwa mpango huo wa kuwapa chombo hicho kunawafanya vijana hao kutumiwa vibaya na baadhi ya wanasiasa hususan katika vipindi vyta Kampeni za Chaguzi mbalimbali hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ngede, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Serikali kupitia Wizara yangu ilibuni na kuanza kuratibu mpango wa kuanzishwa kwa chombo kinachounganisha vijana wote Tanzania bila kujali itikadi zao za kisiasa kuanzia Novemba, 1998. Mwezi Juni, 1999 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Kamati ya Kitaifa ya Uundwaji wa Baraza la Vijana Tanzania, kwa msaada wa Shirika la *Friedrich Ebert Stifting (FES)*, iliandaa kongamano la Kitaifa mjini Iringa, ambalo lilishirikisha Mikoa yote, jinsia zote na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na zile za dini, elimu, siasa na Serikali kwa ujumla. Kongamano hili liliwezesha kupata rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la kuandaa chombo hiki ni muhimu na nyeti, Kamati ya Kuratibu Uundwaji wa Baraza hili imekuwa ikiendelea na mchakato wake kwa makini, ikizingatia hadidu

za rejea zilizotolewa katika kongamano. Kazi kubwa iliyoagizwa ilikuwa kuendelea kukusanya maoni zaidi ya vijana waliopo mashulenii, vyuoni, mijini na vijijini ili kuboresha rasimu ya Katiba.

Hivi sasa, Kamati hiyo imekwishawasilisha Serikalini rasimu ya Katiba iliyozingatia maoni yaliyokwishakusanya ili ipitishwe katika ngazi mbalimbali kabla ya kuandaa Muswada wa Sheria ya kuhalalisha uundaji wa chombo hicho. Hata hivyo, Kamati bado inaendelea kupokea maoni ambayo yatasaidia kuboresha rasimu iliyopo hivi sasa. Katika kongamano lililofanyika tarehe 5 - 9 Mei, 2002 lililoandalila na *UNICEF*, suala la BAVITA lilijadiliwa kwa upana zaidi na hivyo mchango zaidi wa chombo hiki ulipatikana na ambaao utawasilishwa katika hatua zinazoendelea hivi sasa.

(b) Kwa kuwa lengo ni kuwa na chombo kilichoandalila na kushirikisha vijana wote nchini, utaratibu unaofuatwa hivi sasa haukusudii kuchelewesha kuundwa kwa Baraza. Utaratibu unaofuatwa unalenga kupata chombo muafaka. Kwa hatua iliyofikia, tunatarajia kuwa tutafanikiwa, baadaye kuandaa Muswada wa Sheria na kuleta hapa Bungeni, kuunda chombo hiki.

MHE. ASHA A. NGEDE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, je, Wizara hutumia utaratibu gani katika uteuzi wa vijana endapo inatokea mialiko mbalimbali duniani ili kupata uwakilishi wa vijana hao? (*Makofi*)

Pili, je, kwa kukosekana chombo hicho Wizara haioni utaratibu wa uteuzi huo wa uwakilishi unaleta hisia za ubaguzi na upendeleo hasa kwa vijana waliokuwa katika Vyama vya Upinzani? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika kuteua vijana inapotokea shughuli yoyote ya nje unategemea sana shughuli yenye iliyopo huko nje. Kama vijana wanategemea kwenda huko wanakwenda kwa maana ya michezo, itachukua vijana wa michezo. Ikiwa vijana wanaokwenda huko wanahitaji labda shughuli inayohusiana na masuala ya kupambana na maambukizo ya UKIMWI, tutatumia wadau wanaoshughulikia masuala ya UKIMWI ili kuwapata vijana wanaostahili kufanya hivyo.

Kwa mtindo huo basi si kweli kwamba uteuzi huo unaleta hisia za upendeleo au wa kisiasa au kijinsia. Ningependa niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba, uteuzi huu unapofanywa unakuwa ni wa wazi kabisa na ndiyo maana hata hivi juzi tulikuwa na vijana wawili kule Botswana katika Mkutano wa Vijana wa *Commonwealth* na walioshinda wala sio kundi la vijana wa CCM lakini ni kikundi cha Uzalishaji Mali cha Nguvu Kazi kutoka Wilaya ya Sengerema na Jimbo la Sengerema, ambaao ndio washindi wa Jumuiya ya Madola katika uzalishaji mali. (*Makofi*)

Na. 43

Haki za Msingi kwa Watoto Yatima

MHE. BAHATI ALI ABEID aliuliza:-

Kwa kuwa Ugonjwa wa UKIMWI unazidi kuleta athari kubwa kwa jamii; na kwa kuwa ugonjwa huo mpaka sasa haujapata matibabu wala kinga na wazazi wengi wanaofariki huacha watoto wengi yatima ambaao hukosa malezi na matunzo bora na matokeo yake wanakuwa wakizurura mitaani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia huduma muhimu za kijamii kama haki za msingi za Kibinadamu watoto yatima ambaao wazazi wao wamefariki kutokana na UKIMWI?

(b) Hadi swali hili linapo jibowi; je, ni watoto wangapi wa aina hiyo waliopo kwa kila Mkoa na kila Wilaya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Malezi ya Watoto Yatima ndani ya Jamii (*Community Based Care and Support for Orphans and other Vulnerable Children*). Mkakati huu unawawezesha watoto yatima kupata huduma za msingi ndani ya jamii, kuzingatia haki za watoto kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Kiafrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto. Huduma hizo ni pamoja na elimu, afya, maji safi na salama na kuwashakikishia kupata chakula na lishe.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*) na *Axios Foundation Tanzania*, huendesha mpango wa majaribio wa kuwashadumia watoto yatima na walio katika mazingira magumu katika Wilaya za Bagamoyo, Karagwe, Kisarawe, Magu, Makete, Musoma Vijijini, Rungwe, Manispaa ya Mbeya na Muheza. Katika kipindi cha mwaka 2003/04 Wizara ina mpango wa kupanua huduma hii katika Wilaya za Temeke, Masasi, Manispaa ya Mwanza, Bunda, Singida Mjini, Singida Vijijini, Iringa Mjini na Kilosa.

Sera ya nchi kuhusiana na malezi na matunzo kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu inasisitiza umuhimu wa kuwajumuisha pamoja na watoto wengine (*integration*) ili kuondoa unyanyapaa (*stigmatisation*).

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kuwa hatuna takwimu sahihi kuhusu watoto hao kwa kila Mkoa na Wilaya Tanzania Bara na Visiwani. Aidha, Ofisi yangu inawasiliana na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa ili kupata fedha za kufanya utafiti na kupata idadi kamili kuhusu watoto hao.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nilikuwa na swali dogo tu. Je, Serikali ina mpango wa kuandaa utaratibu wa kuweza kuwasajili hawa watoto yatima ili tuwe na takwimu sahihi hapo baadaye?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi nilisema hivi sasa tunashirikiana na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa ili kupata fedha za kuendesha utafiti anaozungumzia Mheshimiwa Kidawa.

Hata hivyo, tungependa kuwakumbusha Watanzania wenzetu kuitia Bunge lako Tukufu kwamba, nia ya Serikali kwa kweli sio tu kusaidia hawa watoto yatima lakini ni kuzuia watoto yatima kutengwa na kukua katika makuzi ambayo yanawafanya wajisikie hawana wazazi, hawana ndugu. Huo ndio msisitizo mkubwa ambao Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tuusisitize katika Majimbo yetu kwamba watoto yatima hata kama wamefiwa na wazazi wao wote wawili, basi penye baba mdogo, mjomba, shangazi, waendelee kuwalea watoto hawa ili wasijione tofauti na Watanzania wenzao pale wanapokuwa wamepata umri.

Na. 44

Dhana ya HESAWA

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR aliuliza:-

Kwa kuwa katika mipango ya kuinua uwezo wa nguvu za wanajamii Serikali kuitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ina lengo la kusambaza uzoefu uliopatikana chini ya Mradi wa HESAWA kwa Mikoa mitatu itakayochaguliwa:-

- Je, dhana hiyo ilitumika vizuri hapo nyuma kwa Mikoa iliyopita?
- Je, ni Mikoa ipi sasa itapewa kipaumbele hicho?
- Je, msaada wa shilingi 1.4 bilioni wa *SIDA* ulisaidia Wilaya ngapi na ultumika vizuri kwa kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, dhana ya *HESAWA* imetumika vizuri katika Mikoa mitatu ya Kagera, Mara na Mwanza. Wananchi wa Mikoa hiyo wameshiriki kikamilifu katika kuandaa na kutekeleza mpango wa afya kupitia maji safi na usafi wa mazingira. Aidha, wananchi walikuwa wakichangia gharama za utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa wananchi vijijini, pamoja na watendaji katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya, ili kuimarisha ushiriki wao katika kuilewa na kuitekeleza dhana hii. Mafanikio ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa mpango huu yanadhihirisha wazi kuwa dhana ya *HESAWA* imetumika vizuri katika Mikoa hiyo mitatu. Baadhi ya mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa mpango huu ni kama ifuatavyo:-

- Visima 3,800 vimejengwa;
- Miradi 915 ya bomba na gati za kuchota maji zimejengwa;
- Vyanzo vya asili vya maji 1,200 vimeboreshwa;
- Vyoo vya taasisi 950 vimejengwa;
- Vyoo 37,000 vya kaya vimejengwa;
- Matanki 400 ya kukinga maji ya mvua ya kaya yamejengwa;
- Matanki 270 ya kuvunia maji ya mvua ya taasisi yamejengwa; na
- Wahudumu wa afya 2000 wamepatiwa mafunzo.

(b) Mheshimiwa Spika, dhana ya *HESAWA* sasa imezingatiwa katika Sera ya Taifa ya Maji iliyozinduliwa mwezi machi mwaka huu wa 2003 na Sera ya Maendeleo ya Jamii. Kwa sababu hiyo ni dhahiri kuwa dhana hiyo inatekelezwa katika Mikoa yote kama sehemu ya utekelezaji wa Sera hizo. Katika kipindi cha mwaka 2000/2001, Wizara ilipanga kueneza dhana ya *HESAWA* katika Mikoa ya Singida, Tabora na Shinyanga kwa kuanzia. Kutokana na ufinyu wa Bajeti hatukuweza kufanya hivyo.

Hata hivyo, katika Mkutano Mkuu wa Wizara, uliofanyika mwezi Oktoba mwaka 2002, uzoefu wa utekelezaji wa dhana hii katika Mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara, ulijadiliwa kwa kirefu na washiriki ambaa walitoka katika Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara. Katika mkutano huo washiriki walikubaliana kuwa dhana hiyo ni nzuri na waliazimia kueneza katika Wilaya zao.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2000/2001, msaada wa kiasi cha shilingi bilioni 1.4 ulitolewa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA*. Fedha hizo ziliikuwa kwa ajili ya Wilaya 16 ambazo ni Sengerema, Ukerewe, Magu, Geita, Missungwi, Klimba, Jiji la Mwanza, Karagwe, Bukoba Vijijini, Muleba, Biharamulo, Ngara, Bunda, Tarime, Musoma Vijijini na Serengeti. Msaada huo uliotolewa umetumika katika kukarabati miradi mbalimbali ya maji, vyoo vya taasisi na mafunzo kwa wanavikundi.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali lifuatato. Je, kuna vigezo gani viliviyotumika katika kuchagua Wilaya au Mikoa ambayo imeanzia katika mradi huo?

Je, ufinyu wa Bajeti aliousema Mheshimiwa Naibu Waziri katika Bajeti hii ufinyu huu utaondoka?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, tulianza na Mikoa hiyo mitatu kwa sababu Mikoa hiyo ndiyo ilipendekezwa na hao wahisani wakubwa walikuwa ni *SIDA*.

Pili, kwa upande wa ufinyu wa Bajeti naona katika jibu langu nimesema kwamba, sasa mradi huu umemalizika mnamo tarehe 30 Juni, 2002 na imependekezwa kwamba sasa dhana hii ya *HESAWA* ichukuliwe katika Bajeti ya Halmashauri zinazohusika. Kwa hiyo, kama Bajeti ikeruhusu masuala haya yataendelea kwa nguvu zote.

MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba, Mikoa hii iliyochaguliwa ilipendekezwa na hao wahisani au wafadhili kwa kuanzia. Je, Wizara haioni kwamba inaweza kuwashawishi wafadhili hawa wakiona kama Mikoa mingine ndiyo inahitaji zaidi miradi hii iwepo kuliko hiyo iliyo tajwa. Je, Wizara haiwezi kushawishi wafadhili wakageuza ili kwenda kwenye Mikoa ambayo inahitaji zaidi mradi huu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingi huwa inaanzishwa nchini. Huu sio mradi wa kwanza na utakuta kwamba miradi inapoanzishwa inakwenda katika sehemu tu ya nchi au baadhi tu ya Mikoa. Sasa mradi huu ulipendekezwa kwamba uanzishwe katika sehemu ya Mkoa au sehemu ya Ziwa.

Mikoa hii mitatu ni sehemu ya Ziwa Victoria na kwa sababu sasa mradi huu tayari umesitishwa, ukiniambia kwamba niende tena pale kwa wale wahisani tunaweza tukaenda tukazungumza nao labda kwa awamu inayofuata. Lakini kwa awamu hii mradi huu umesitishwa. Lakini dhana inaendelea pale pale. (*Makofii*)

Na. 45

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera kinatoa mchango mkubwa katika harakati za kupambana na umaskini; na kwa kuwa chuo hicho hakina umeme wa uhakika na mfumo wake wa maji umechakaa; je, Serikali hadi sasa imechukua hatua zipi kusaidia Chuo hicho kupunguza kero zinazokikabilii?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo: -

Chuo cha Gera kama vivilvyo vyuo vingi nchini kina kero mbalimbali zinazozua ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Kero ambazo Wizara yangu inazifahamu katika chuo hiki ni uchakavu wa majengo/miundombinu mingine, ukosefu wa umeme, ukosefu wa fedha za uendeshaji na upungufu wa wakufunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango mkubwa unaotolewa na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera katika harakati za kupambana na umaskini, Serikali imechukua hatua zifuatazo katika kukipunguzia Chuo hiki kero hizo zinazokikabilii: Katika mwaka wa fedha 2001/2002, Chuo kilipatiwa jumla ya Sh. 2,000,000/= na vile vile, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo kilipatiwa Sh. 2,140,000/= kwa ajili ya uendeshaji, Chuo kimepatiwa jenereta ndogo ya umeme na pia Chuo kimepatiwa Sh. 4,000,000/= mwaka 2002/2003 kwa ajili ya ukarabati wa majengo.

Aidha, Chuo kimepatiwa mkufunzi mpya wa somo la uelewa (*General Subject*) mwezi Aprili, 2002 ili kupunguza kero ya upungufu wa watumishi uliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Kamala yenye Kumb. Na. NKG.MB.Vol.59/506 ya tarehe 19 Agosti, 2002 iliyobainisha mahitaji ya ukarabati wa mfumo wa maji ya Sh. 4,000,000/=. Baada ya kupokea barua hiyo, Wizara yangu ilimwagiza Mkuu wa Chuo cha Gera kutuma makisio ya ukarabati wa mfumo wa maji kwa mchanganuo wake halisi. Makisio hayo pamoja na ya vyuo vingine yamezingatiwa katika bajeti ya Wizara ya mwaka 2003/2004.

Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa tutaendelea kutatua kero hizi zinazovikabili vyuo vyetu, kikiwemo Chuo cha Gera, hatua kwa hatua kwa jinsi uchumi wa nchi unavyoendelea kuimarika na hali ya kifedha kuruhusu. (*Makofi*)

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada ambazo Wizara imekuwa ikizichukua, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alipotembelea chuo hicho alijionea tatizo mojawapo la umeme; na kwa kuwa aliungana na chuo hicho kuiandikia barua Wizara ya Nishati na Madini ili iweze kukipatia chuo hicho umeme; je, barua aliyoiandikia Wizara ya Nishati na Madini ilikwishajibwa au hajajibwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri ungemwachia mwenye Wizara yake, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba, taarifa hizi kwa kweli ndiyo nazisikia sasa hivi na nitakuwa tayari kwenda kuzifutilia baada ya kikao hiki cha Bunge ili kuhakikisha kwamba, Mheshimiwa Mbunge anajibiwa ipasavyo.

Pili, napenda kusema kwamba, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alivyojibu vizuri sana hapa Bungeni, ni kweli kwamba chuo hiki kimepatiwa umeme wa jenereta. Umeme wa aina hii ni moja ya njia za umeme ambazo tunazalisha pia katika maeneo mengi hapa nchini. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba umeme huu wa jenereta hautoshelezi, basi sisi katika Wizara tutakuwa tayari kuititia taratibu zilizopo kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wizara husika na kuhakikisha kwamba wanapata umeme wa njia nyingine (*Grid*). (*Makofi*)

MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Vyuo hivi tulipovianzisha Tanzania matumaini yetu yalikuwa ni kupanua uwezo wa kiufundi katika sehemu mbalimbali za nchi na kwa kuwa sasa hivi inaonekana kama uendeshaji wake unahitaji kuweka mfumo mwingine ili kuweza kuviimarisha vyuo hivi, pale Sengerema tuna vyuo viwili pamoja na kile cha Karumo. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliani nami kwamba sasa ni muda muafaka kushirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu katika kuviwekeea vyuo hivi mfumo mpya ili kuweza kuviimarisha dhana ya ufundi katika Sayansi na Teknolojia kuititia vyuo hivi? (*Makofi*)

SPIKA: Naona kama ni swali jipya, sijui kama Naibu Waziri anaweza kujibu. Anahitaji notisi ili aweze kulijibu vizuri.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa vyuo hivi ni muhimu sana katika maendeleo yetu na kwa kuwa kuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo baadhi yake vina majengo makubwa sana lakini wanachukua wanafunzi 10, 15 hadi 20 tu:-

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba ili kuvitumia vizuri vyuo hivi kuna haja ya kuchukua wanafunzi wa kutosha ili tuweze kukidhi haja ya kutoa mafunzo ya ufundi yanayotakiwa?

(b) Kwa kuwa Serikali iliahidi kuviiamarisha vyuo hivyo kwa kuvipatia vitendea kazi nya kutosha, je, ni lini Vyuo nya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Kisalu - Mpwapwa vitapatiwa vifaa nya kutosha ili viweze kutoa elimu ya ufundi inayotakiwa? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, nchi hii ina Vyuo nya Maendeleo ya Wananchi 58 na vyuo hivyo vyote vinahudumiwa tu. Nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba, tuna matatizo, lakini pamoja na matatizo hayo tunajaribu kuvisaidia vyuo hivi kila mwaka. Kwa mfano, mwaka 2002 tulikarabati vyuo vипатавyo 15.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivyo vina bodi zake na Mwenyekiti wa Bodi ni Mkurugenzi wa Halmashauri husika, sisi Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo, pamoja na Wabunge wa Viti Maalum, ni Wajumbe katika Bodi hizo. Ninashauri kwamba bodi hizo zikae ili tuweze kujadili kwa pamoja matatizo ya vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa vyuo ambavyo viko karibu sana na Halmashauri ni Chuo cha Ifakara, Chuo cha Kasulu, Chuo cha Kibondo, Chuo cha Kilosa, Chuo cha Mbanga, Chuo cha Msingi, Chuo cha Newala, Chuo cha Rubondo na kadhalika. Napenda kutoa wito kwamba, vyuo vilivyobakia navyo viwe karibu sana na Halmashauri ili tuweze kuleta maendeleo kwa pamoja. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Na. 46

Barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay*

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA aliuliza: -

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 barabara ya Mtwara - Masasi - Tunduru - Namtumbo - Songea - Mbanga hadi *Mbamba Bay* ni mionganoni mwa barabara zilizopangwa kutengeneza kwa kiwango cha lami katika kipindi cha 2001 - 2005. Je, matengenezo ya barabara hiyo yataanza lini?

WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbanga Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu swali namba 118 la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge kuwa, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya kazi za upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*), kwa barabara ya Mtwara - Masasi - Tunduru - Songea - *Mbamba Bay* zimekamilika na tayari Mhandisi huyo amekwishaanza kufanya kazi hiyo. Kazi hiyo ya upembuzi yakinifu sasa imeanza na inaendelea kufanyika na inatarajiwaa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba 2003. Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, ndipo tutakapojuu gharama za ujenzi wa barabara hiyo. Hivi sasa Wizara yangu inasubiri kukamilika kwa kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na baada ya hapo tutaanza kutafuta fedha za kugharamia usanifu na ujenzi wa barabara husika. (*Makofii*)

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ni kichocheo muhimu sana cha maendeleo katika Mikoa hiyo ya Mtwara na Ruvuma; na kwa kuwa kutokana na kuwa na barabara mbaya sekta mbalimbali haziendelei kama utalii, biashara na maendeleo ya sekta nyingine; je, Serikali itakuwa tayari kuwathibitishia wananchi wa mikoa hiyo kama *survey* ikikamilika fedha zitapatikana haraka ili barabara hiyo itengenezwe kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa barabara ya Mtwara - Masasi - Mbamba Bay ni kichocheo kikubwa katika maendeleo ya Mikoa ya Mtwara pamoja na Ruvuma. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zilizopatikana ambazo ni karibu shilingi bilioni moja zinazotumika sasa hivi kwa ajili ya kufanya *feasibility study*, zinadhihirisha kwamba, ni nia ya Serikali katika kuhakikisha kwamba barabara hiyo yenze jumla ya kilometra zaidi ya 650 inajengwa kwa kiwango cha lami. Upatikanaji wa fedha utategemea kumalizika kwa *feasibility study* ambayo inafanyika sasa hivi. Lakini pia kwa taarifa tu ya Mheshimiwa Mbunge, napenda kumjulisha kwamba katika kuhakikisha kuwa barabara hii inajengwa katika kiwango cha lami imewekwa pia katika mpango (*Priority No.1*), kwenye barabara za *East African Community* zitakazoshughulikiwa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu baada ya *feasibility study* fedha zitapatikana kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. (*Makofifi*)

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Baada ya majibu mazuri aliyayatoa Mheshimiwa Waziri, kwa vile safari ya kwenda Mbamba Bay unaweza ukapita barabara ya Mtwara - Mnazi Mmoja - Masasi au barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia kwamba mpango uliopo na huo alioutaja sasa hivi kuhusiana na ujenzi wa barabara hii unahusisha barabara hii inayotoka Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*) unapofanyika kwa kawaida huwa unaangalia barabara ambayo ni fupi zaidi na ambayo haipunguzia gharama Serikali katika matengenezo yake. Kwa hiyo, kwa kuzingatia hili, barabara ambayo inafanyiwa *feasibility study* ni ile ya kutoka kwenye Bandari ya Mtwara - Mnazi Mmoja - Masasi - Mbamba Bay. Barabara ya Tandahimba - Newala - Masasi ni barabara ya Mkao na itaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za *Road Fund* na itaendelea kutengenezwa katika kiwango cha changarawe. (*Makofifi*)

Na. 47

Survey na kuweka lami Barabara ya Uchumi ya Soni - Dindira

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swalı langu la nyongeza kuhusu barabara za chai za *East Usambara* (Amani) kwamba zihusishwe pia zile za *West Usambara* ilinielekeza nipeleke maelezo kwa Meneja wa Mkao wa *TANROADS* - Tanga; na kwa kuwa nimeshapeleka maelezo hayo hapo tarehe 20 Aprili, 2001 kwa kuzingatia vigezo viliviyowekwa kitaalam: -

- (a) Je, ni lini barabara hiyo itafanyiwa *survey* ili gharama yake iweze kujulikana?
- (b) Je, isingekuwa vyema barabara hiyo ikafanyiwa *survey* kutokana na umuhimu wake katika kusafirisha chai kwenda kwenye masoko ya nje ikahusishwa pia na misaada inayotolewa kwa ajili ya kuendeleza zao la chai?
- (c) Kwa kuwa sasa ni mwaka wa tatu tangu niandike barua yangu bila kupewa maelekezo yoyote toka kwa wahusika; je, mimi kama Mbunge nichukue hatua gani?

WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

Barabara ya Soni - Bumbuli hadi Dindira ina urefu wa kilomita 45.1 ikiwa ni ya tabaka la changarawe kati ya Soni hadi Bumbuli (kilomita 21) na kutoka Bumbuli hadi Dindira (kilomita 24.1) ni ya tabaka la udongo.

Barabara hii ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), Mkoa wa Tanga. Napenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, inaelewa vizuri umuhimu wa barabara hii, ambayo hutumika kwa kusafirishia zao la chai kutoka kwenye mashamba makubwa ya Mponde na Dindira na pia mashamba mengine yanayomilikiwa na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutambua umuhimu huo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara katika mwaka wa fedha 2001/2002, ilitumia jumla ya shilingi milioni 17.5 kufanya matengenezo ya kawaida, umbali wa kilomita 38 katika barabara hii na kwa mwaka wa fedha 2002/2003 kiasi cha shilingi milioni 88 kimetumika kugharamia ukarabati wa kilomita 6.5 na matengenezo ya kawaida katika kilomita 39 za barabara hii.

Barabara ya Soni - Dindira itafanyiwa *survey* kutegemeana na uwezo wa Serikali kifedha ili gharama za kuijenga kwa kiwango cha lami ziweze kujulikana na hii ni kwa sababu pia kuwa barabara hii inahusisha kuendeleza zao la chai.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizopo zinaonesha kwamba, ombi la Mheshimiwa Mbunge la kutaka barabara hii ifanyiwe *survey* liliwasilishwa kwa Meneja wa Mkoa *TANROADS* Tanga, kwa barua yenye Kumb. Na. MB/RRB/13/8 ya tarehe 20 Aprili, 2001 na kupokelewa tarehe 6 Juni, 2001.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imetenga shilingi milioni 30 katika bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004 ili zitumike kufanya upembusi yakinifu kwa barabara ya Soni hadi Dindira. Aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) itaendelea kuifanya matengenezo barabara hii ili iweze kupitika wakati wote kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. (*Makofi*)

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge hili kwa dhati kabisa nini kiungo kati ya Wakala wa Barabara na Uongozi wa Wilaya au Mkoa hasa kwa vile kikao cha *Regional Road Board* kinaitishwa kwa ridhaa ya Wakala wenye na wakati mwingine hakiitishwi, mfano ni kwa Mikoa ya Arusha na Manyara mwaka huu na hatujui hata kilichopendekezwa katika bajeti hii kwa Mikoa hiyo kuhusu utengenezaji wa barabara?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 1998, ambayo ilianzisha Mfuko wa Barabara. Katika Mfuko wa Barabara ndipo kuna fedha ambazo huwa zinatolewa kwa ajili ya *TANROADS*, kuna fedha ambazo zinatolewa chini ya TAMISEMI na kuna fedha ambazo zinatolewa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mahusiano yaliyopo katika vyombo hivi ni kuwa kwanza, *TANROADS* katika kufanya kazi yoyote huwa ni lazima ipeleke *performance agreement* kwenye Mfuko wa Barabara ambao una Wajumbe wanane, wanne kutoka Serikalini na wanne kutoka kwa watumaji wa barabara. *Performance agreement* ile ikishakubalika ndipo *TANROADS* wanakwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kuhusisha uhusiano mzuri kati ya Wizara, *TANROADS*, pamoja na Uongozi wa Mikoa na Wilaya, huwa kuna vikao vya *Road Board* na katika vikao hivi Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Mkoa na vikao hivi huitishwa na yeye. Kwa hiyo, ninategemea Mkuu wa Mkoa wa Manyara, ataweza kuitisha vikao ili Waheshimiwa Wabunge waweze kushiriki katika kujadili mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, vikao vya *Road Board* huwa viko chini ya Mwenyekiti, ambaye ni Mkuu wa Mkoa na Makamu Mwenyekiti huwa ni Mbunge mmojawapo anayeteuliwa kutoka kwenye Mkoa unaohusika. (*Makofi*)

Vivutio vya Watalii Lindi na Mtwara

MHE. MARTHA M. WEJJA (k.n.y. MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME) aliuliza: -

Kwa kuwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara zipo raslimali ambazo zinaweza kuvutia watalii kama vile majengo ya kale yaliyopo Kilwa na Mikindani, ufukwe wa bahari mzuri na wa kustaajabisha uliopo Msambati Mtwara vijijini: Je, ni lini Serikali itaanzisha Sekta ya Kitalii katika Mikoa hiyo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na taarifa ya wataalam wa utalii walitembelea Mkao wa Lindi na kutoptaka na taarifa za kitaalam kutoka Mtwara, Mikoa hiyo imebainishwa kuwa na raslimali za kuweza kuvutia watalii. Vivutio hivyo ni pamoja na wanyamapori, fukwe nzuri za kuvutia, mapango na magofu yenye historia ya Kilwa na utajiri mkubwa wa mila na desturi za wananchi waishio katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tayari Wizara yangu inajishughulisha na uendelezaji wa utalii katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*), Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Serikali za Japan na Ufaransa, tunaendesha Mradi wa Uhifadhi na Uendelezaji Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma hii, baadhi ya kazi zilizoainishwa katika malengo ya mradi zimekwishaanza na nyingine bado kwa kuzingatia muda wake wa kuanza. Kazi ambazo tayari zimeanza na zinaendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa gati eneo la Kilwa Kisiwani, ukarabati wa Msikiti Mkuu, ukarabati wa nyumba ya kupumzikia wageni na usafi wa maeneo ndani na nje ya magofu. Kazi nyingine ni kuweka mtambo wa umeme unaotumia mionzi ya jua ili kuhudumia nyumba ya wageni, zahanati na gereza la kale eneo la Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu kupitia Hifadhi ya Bahari na maeneo Tengefu (*Marine Parks*) na kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo (*UNDP*) na Benki ya Dunia, tunaendeleza Hifadhi ya Bahari ya *Mnazi Bay* katika nyanja za utalii na hifadhi. Hifadhi hii ni maarufu kwa matumbawe, nyangumi, pomboo (*dolphins*), ndege na misitu ya mikoko. Uendelezaji utalii katika hifadhi hii utaongeza pato la hifadhi na kuchangia maendeleo ya wananchi waishio katika eneo hilo na Mikoa ya Kusini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) na wadau wengine wanaendeleza miradi ya maendeleo yenye lengo la kuboresha mifumo ya usafiri kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ujulikanao kama *Mtwara Development Corridor*. Chini ya Mpango huu, upanuzi wa Bandari ya Mtwara na uendelezaji wa miundombinu utachangia kupanuka kwa Sekta ya Utalii katika eneo la Mikoa ya Kusini. Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuvutia uwekezaji katika maeneo ya Lindi na Mtwara ambayo yamo katika Ukanda wa Kusini wa Utalii kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuweka taarifa katika tovuti ya Wizara inayolenga wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba, zipo juhudii za dhati kabisa kwa upande wa Serikali katika kuendeleza utalii katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na Ukanda wa Kusini kama ilivyoainishwa kwenye Mpango Kamambe wa Utalii (*Tourism Master Plan*).

MHE. MARTHA M. WEJJA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza tu mpangilio uliopo kwenye makaratsasi, je, ni lini utekelezaji huo utaanza ili tujue alichosema kama kinawezekana?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Wejja, atembelee eneo hili la Kusini tunalolitaja. Kwa kweli atakubaliana nami kwamba, kuna mabadiliko makubwa sana. Nimezungumzia *Tourism Master Plan*, lakini hata ukifika hivi sasa utakuta kuna mabadiliko makubwa yamefanyika kule Kilwa Kisiwani.

Waheshimiwa Wabunge, labda ningewaeleza tu kwamba, hivi sasa hata wale watalii ambao wanataka kutembelea sehemu za Kilwa inabidi wafanye *booking* kabla hawaajaenda huko. Kwa hiyo, mabadiliko yameshaanza na yanaendelea. (*Makofi*)

MHE. LEDIANA M. NG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa maeneo ya utalii aliyoyataja Mheshimiwa Waziri yapo maeneo ya Mtwara na Lindi, pia Mkoa wa Iringa una maeneo ya utalii na ya vivutio kama Kalenga, Lugalo, Isimila, Tosamaganga na Idodi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaahidi nini wananchi wa Mkoa wa Iringa ili na wao kupata vivutio yya utalii kama hivyo vinavyofanywa Mtwara na Lindi? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nilishawahi kujibu swali hapa Bungeni kwamba, kwa upande wa Iringa tayari wataalam wameshafika na tayari mambo yanafanyika. Kwa mfano, eneo lile la Chifu Mkwawa sehemu za Kalenga, kuna mabadiliko makubwa ambayo yanafanyika. Pia, kuna matengenezo ya *museum* pale sehemu ambapo Chifu Mkwawa alikuwepo. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, kwa upande wa Iringa kuna mambo makubwa ambayo yameshafanyika na ninawombwa Mheshimiwa Mng'ong'o akipata nafasi atembelee maeneo hayo. (*Makofi*)

Na. 49

Watanzania Kutembelea Mbuga za Wanyama

MHE. RUTH B. MSAFIRI aliuliza: -

Kwa kuwa tunazo mbuga za wanyama Tanzania ambazo ni kivutio kikubwa cha watalii; na kwa kuwa Watanzania hasa watokao nje ya maeneo ya mbuga za wanyama wangependa kutembelea mbuga hizo; je, Serikali ina utaratibu gani nafuu kwa Mtanzania kutembelea mbuga hizo na kupata huduma ile ile kwa gharama nafuu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanzisha utaratibu wa kuwawezesha Wananchi kutembelea hifadhi kwa gharama nafuu kabisa. Tozo za kuingia hifadhini ni kama ifuatavyo: -

(a) Tozo ya kuingia Hifadhi za Taifa, Arusha, Kilimanjaro, Tarangire, Manyara na Serengeti ni Sh. 1,500/= kwa watu wazima wanaozidi miaka 16. Watoto kati ya miaka 5 - 16 hulipa tozo ya Sh.500/= tu;

(b) Hifadhi za Katavi, Mikumi, Ruaha, Rubondo na Udzungwa hutoza Sh. 1,000/= kwa mtu mzima na Sh. 500/= kwa watoto kati ya umri wa miaka 5 -16;

(c) Gharama au tozo la kuingia katika Hifadhi za Gombe na Mahale ni Sh. 1,500/= kwa mtu mzima na Sh. 500/= kwa watoto kati ya miaka 5 - 16; na

(d) Watoto chini ya miaka 5 hawatozwi ada ya kiingilio.

Hali kadhalika, hakuna tozo la ada ya kiingilio kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, gharama au tozo kwa magari ya Watanzania ni kama ifuatavyo: -

- (a) Tani moja hadi tani mbili ni Sh.2,000/=;
- (b) Tani mbili hadi saba ni Sh.10,000/=; na
- (c) Zaidi ya tani saba ni Sh.15,000/=.

Gharama hizi ni ndogo sana ikilinganishwa na gharama wanazotozwa wageni kutoka nje ya nchi. Vile vile, hifadhi za Taifa zimeanzisha mpango wa malazi nafuu kwa Wananchi.

- (i) Hifadhi za Rubondo, Manyara, Mikumi, Kilimanjaro na Gombe zina *hostels* ambazo hutoza Sh. 500/= kwa kulala mtu mmoja kwa siku moja;
- (ii) Hifadhi ya Serengeti ina *hostel* ya kisasa ambayo hutoza Sh.3,000/= kwa mtu mmoja kwa siku. Hifadhi za Manyara, Ruaha na Mikumi zina mabanda ambayo hutoza Sh.3,000/= kwa siku kwa mtu mmoja;
- (iii) Hifadhi za Serengeti, Ruaha, Mikumi, Arusha na Katavi zina nyumba ya kupumzikia wageni (*Rest Houses*), ambazo hutoza Sh.5,000/= kwa usiku mmoja kwa mtu mmoja; na
- (iv) Hifadhi za Gombe na Mahale zina nyumba za kupumzikia wageni ambazo hutoza shilingi 2,000/= kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Hifadhi za Taifa zina mkakati wa kuanzisha hosteli na huduma nyingine za malazi kwa kila hifadhi ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanaweza kupata huduma hizo kwa gharama nafuu.

MHE. LUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, ambayo hasa ndiyo lilikuwa kusudio la swalilangu kutaka kujuu ni mkakati gani unaowahamasisha Watanzania kutaka kwenda kuona mbuga zao za Wanyama.

Sasa swalilangu kutaka kujuu ni mkakati gani unaowahamasisha Watanzania, ambao wanatoka nje ya hifadhi ili waweze kwenda kuziona hizo mbuga ili kuondoa ile dhana ya kusema kwamba hizo mbuga ni kwa ajili tu ya wageni wa kutoka nje? (*Makofifi*)

Pili, iko mbuga moja katika Hifadhi ya Biharamulo. Je, kuna utaratibu gani kuhusu hifadhi hiyo na yenye kuiweka katika taratibu za mbuga kama zingine? (*Makofifi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba katika sehemu hii ndipo ambapo hivi sasa tunatilia mkazo. Ni sehemu ambayo miaka ya nyuma tulikuwa hatutilia mkazo sana. Mkazo mkubwa ulikuwa kwa watalii ambao wanatoka nje. Lakini hivi sasa mkazo mkubwa nao pia unatiliwa kwa watalii wa kutoka ndani ya nchi na ndiyo jibu ambalo nilolitoa. Sasa kuhusu kutangaza mbuga hizo, tumeanza kutangaza kwa wananchi ili waweze kuyatembelea maeneo mbalimbali. Mara nyingi sana tumefanya uhamasishaji kwa mfano kwa wananchi wa maeneo ya Mwanza, Mara, tumekuwa na matangazo na uhamasishaji pale Mwanza ili wananchi waweze kutembelea Mbuga ya Serengeti. Lakini pia mtakumbuka kwa Waheshimiwa Wabunge, ambao wanatembelea katika maonyesho ya Kitaifa kila mwaka, tuna mpango wa kuwapeleka wananchi Mikumi. Kwa hiyo, kuna utaratibu maalum wa kukodisha gari ambapo wananchi wanalipa shilingi 10,000/= kwa siku wanapelekwa Mikumi na kurudi na jambo hili kwa kweli limesaidia sana kutangaza nchi yetu.

Kwa hiyo, Wizara kwa ujumla itazidi kusisitiza kutangaza vivutio vyetu hivi ili wananchi yenye waweze kuvitembelea.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali uliowekwa na kanuni umekwisha. Sasa tunaendelea na mambo mengine. Kabla ya kuendelea kuna taarifa zifuatazo:-

Taarifa ya kwanza, Waheshimiwa Wabunge, niliwhi kumtambulisha Balozi wa Japan, aliyejkuwa amemaliza muda wake kwamba aliomba aje kuwaaga Wabunge kwa kukaa kwenye *gallery* na mimi kumtambulisha kwamba yupo kwa nia ya kuagana na Wabunge. Sasa leo nataka kumtambulisha Mheshimiwa Balozi wa Sweden, Sten Raylander, ambaye naye amekuja kwa madhumuni hayo hayo ya kuwaaga Wabunge, atasimama ili muweze kumwona. (*Makofi*)

Balozi Raylander, amefuatana na mkewe kama mlivyoona na Maafisa wawili wa Ubalizi. Baadaye kidogo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ingawa hoja yake iko Bungeni, hatakuwepo hapa kwa sababu pamoja na kuaga Bunge, Mheshimiwa Balozi Raylander amekuja kusaini Mkataba na Serikali ya Tanzania wa kutoa msaada wa shilingi bilioni 42. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ana idhini ya kutokuwa Bungeni kwa kipindi kama cha nusu saa hivi. Kwa hiyo, Manaibu wake wa Wizara ya Fedha wataendelea kupokea michango ya Wabunge. (*Makofi*)

Taarifa ya pili ni vikao vya leo. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa tano asubuhi hii, kwenye vyumba vya Kamati chumba namba 56.

Kikao cha pili kimeitishwa na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Joel Bendera, anaomba Wajumbe wote wa Umoja wa Wabunge Wana michezo wakutane leo saa saba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, kikao cha asubuhi, kwa mazungumzo ambayo atayaongoza mwenyewe. Mwisho wa matangazo ya vikao.

Taarifa nyininge moja niseme kwamba, ingawa tuliweka kwenye mbao za matangazo orodha ya waliomba kuchangia, naomba kufafanua kwamba, ile imepangwa kwa kadri tulivyopokea maombi tu si kwamba watachangia kwa utaratibu huo. Kwa sababu tunapanga orodha kwa vigezo fulani fulani, lazima kuweka uwiano mzuri baina ya Wabunge Wanawake, Wanaume, Wabunge wa Upinzani. Kwa hiyo, ilikuwa ni kuonyesha tu nani yuko kwenye orodha ya kuchangia, lakinii hawataitwa kwa mtiririko huo. (*Makofi*)

Taarifa nyininge ni kwamba, sasa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu, wamepewa ofisi katika Jengo la Utawala. Kwa hiyo, Wajumbe wao wanaweza kuonana na Wenyeviti katika ofisi zao za kudumu katika ghorofa ya tatu ya Jengo la Utawala. Sasa kama niliyotangaza jana kwamba, nitakuwa nawapangia zamu wale wanaonisaidia kuongoza Bunge, leo itakuwa ni zamu ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kuongoza Bunge ili naye ajenge uzoefu kama alivyofanya mwenzake jana. Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/2004 na Makadirio
ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004**

(*Majadiliano yanaendelea*)

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza asubuhi hii.

Lakini la pili, naomba nichukue nafasi hii niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo uliopita. Naomba tufanye kazi kwa pamoja ya kujenga nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, ambao ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa dira ya hali halisi ya maendeleo ya nchi yetu katika kipindi cha mwaka huu tunaoanza Julai, Mosi mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kusema kwamba, hotuba za Mawaziri wote wawili kwa kweli zimekuwa hotuba za mapinduzi kabisa. Waswahili wanasema aliye na macho haambiwi tazama, kwa sababu inaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka miwili, mitatu, iliyopita niliwahi kuongea katika Bunge hili kwamba, Serikali imefanya vizuri katika eneo la kuendesha *macro-economy* kama uchumi ule wa *balance sheet*, mambo ya *finance*, walianza vizuri sana toka awamu ya pili na kuendelea. Lakini kwa sababu moja au nyingine, hali ya uchumi ilikuwa imeelezwa wakati wote kwamba nchi yetu uchumi wake unakua. Lakini ulikuwa unakua kwa maana hiyo kwamba, umeweza ku-*balance* vitabu vyetu kulingana na hali halisi ya dunia, lakini ilikuwa bado kabisa kuwfikia wananchi. Sasa naona Serikali baada ya kufanya hatua ya kuweza kurekebisha uchumi kwa ngazi hii ya juu sana, sasa imeanza kurekebisha uchumi kwa ngazi ya wananchi. (*Makofi*)

Sasa hayo ndiyo mapinduzi yanapoanza na ndiyo sifa kubwa pekee ya hotuba hii kulinganisha na hotuba nyingine za miaka iliyopita, maana ilikuwa ni kitu ambacho hakifikiriki. Wananchi wote nchi nzima wanaelezwa kwamba uchumi umekua, wanasema ndiyo tunasikia lakini mtu akijiangalia mwenyewe anajiuliza huu ukuaji wa uchumi unahusika nini na maisha yangu maana shida zinaongezeka. Uzuri ni kwamba Waziri wa Fedha katika *paragraph* ya 30 ameelezea kabisa kwamba, maendeleo ya huduma za jamii, sasa yanakwenda kwa wananchi. Ameelezea kwamba umaskini wa kipato umeongezeka kwa hiyo hawajakataa kwamba hayo hayapo, maana naona kuna watu wanaeleza kwamba nchi hii ni maskini. Waziri wa Fedha anakiri kwamba huo umaskini umeongezeka na kwa kweli hilo ndilo eneo ambalo ningependa kuwekea mkazo kwamba, ikiwa mwananchi mmoja mmoja umaskini wake umeongezeka mafanikio yanayopatikana kwa maeneo mengine kama huduma za jamii yatapungua baada ya muda mfupi.

Kwa mfano, mpango wa Serikali wa Elimu ya Msingi unakwenda vizuri. Mpango wa Serikali kwenye eneo la huduma za afya ingawa bado haujaonekana vizuri lakini mimi najua unakuja vizuri. Kwenye eneo la maji hatujakamilisha vizuri, lakini hatua zinaonekana zipo. Kwenye maendeleo ya barabara na vitu vingine hatujakamilisha vizuri lakini maendeleo yapo. (*Makofi*)

Sasa iwapo eneo la umaskini wa kipato cha Mtanzania halitataliwa mkazo wa nguvu, mafanikio yote haya hayawezi kuwa stahimilivu kwa sababu itafika mahali hatutaendelea milele kwamba watoto wataendelea kusoma bila ada, haiwezekani kwa sababu sasa hivi tumeweza haya kwa sababu tuna mpango huu wa *HIPC* wa kusamehewa madeni, mpango wa *World Bank* kutusaidia na hivyo ndiyo Bajeti yetu imekuwa tegemezi kwa asilimia 45, maana ni kwamba sasa ni wakati wa kukazana kabisa katika eneo la kuondoa umaskini wa kipato kwa mtu mmoja mmoja, Kijiji, Kata, Wilaya na mwisho Taifa zima, hili ni muhimu. (*Makofi*)

Matokeo ya kuwa na hali ngumu ya uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na familia zao yanaonekana ni vijana kujaa kwa wingi mijini, wanatoka vijijini wakiamini kwamba mjini watapata kazi, wakifika mjini hakuna kazi. Wako watu wajanja wanawatumia vijana wasiokuwa na kazi kwa malengo yao binafsi, yawe ya kisiasa, yawe ya aina nyingine yoyote hata madawa ya kulevy, kuna watu wanataka kujitajirisha kwa sababu vijana hawa hawana kazi wanaanza kuwaingiza katika mambo ambayo ni ya ovyo. Vile vile haya masuala ya ubakaji nayo pia ni sababu mojawapo yanachangiwa na hilo kwa sababu mtu hana kazi, ameingizwa kwenye mambo ya madawa ya kulevy na vitendo vingine vya ubakaji na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, najaribu kueleza jinsi athari za kutokuwa na kipato kwa mtu mmoja zinavyoweza kuwa kubwa katika jamii yetu. Hivi sasa tunalalamika ujambazi umekithiri katika nchi yetu ni mkubwa sana. Sijui kama wanaoshikwa wale kwa sababu hutakuta mtu mzima wa umri zaidi ya miaka 70 kwenye ujambazi, kama yupo basi yuko nyuma ya hawa, lakini wanaotenda vitendo hivi ni vijana. Yote haya yanatokana na kwamba hawana shughuli ya kufanya, hawana kipato cha kuwapatia riziki yao bali

kilichobaki ni kufanya vitu ambavyo jamii kwa kweli haifurahishwi na inakosesha amani. Mheshimiwa Waziri, amesema uchumi wetu umekua tulivu, ni kweli lakini tunakokwenda inaonekana utulivu huu utakuwa hauna maana kwa sababu haisaidii mtu kujisaidia mwenyewe kuongeza uchumi wake, halafu kesho wanakuja watu wengine wanavamia nyumba yake na kumnyang'anya mali hata pengine kuondoa maisha yake. Kwa hiyo, hii hali inatokea kwa sababu ya umaskini wa kipato cha wananchi wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, elimu ni njia mojawapo muhimu sana ya kupambana na umaskini. Lakini sasa nini kinachoanza, ni elimu au kipato? Sasa mimi nasema yote yanatakiwa kuanza pamoja na ni mara chache sana watu wengine elimu wanashindwa kufikiri nini cha kufanya. Kwa hiyo, mimi naomba sana familia zetu ziwezeshe kupata kipato, waone umuhimu wa kupeleka watoto wao shule na wasome vizuri kusudi wawe raia wema na watu ambao wanawenza kufikiri namna ya kuendesha maisha yao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru Serikali kwa kuliona hilo. Serikali imeliona hilo imejaribu katika Bajeti hii kutafuta mbinu mbalimbali za kuweza kusaidia watu kuondokana na matatizo ya kipato chao. Moja kubwa ambalo limefanywa katika eneo linalonihusu mimi ni ile ruzuku ya mbolea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, watu wa mikoa hiyo ya kusini iliyoitwa *big four*, kipindi fulani sidhani kama ilikuwa ni *big four* kwa sababu ya mbolea ni kwa sababu uzalishaji wao wa mazao ya mahindi ulikuwa mkubwa. Kweli ulishuka sana kwa sababu ya gharama za mbolea ambazo zilikuwa kwa kweli hazitabiriki. Kukosa mbolea sehemu ile ni afadhali uache kabisa kulima na ukiacha kulima ni kwamba kutakuwa na njaa na kukiwa na njaa wewe utakuwa umepoteza utu wako kabisa. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kutuwekea ruzuku katika suala la mbolea. Hiyo ni hatua moja kama walivyoeleza wenzangu bado tunajiuliza ni namna gani ruzuku hii itaweza kudhibitiwa na ikawaendea walengwa kweli kweli na wajanja wachache watakaochukua mbolea hiyo rahisi na kupeleka kwenye maeneo ambayo mbolea ni ya ghali. Hilo bado nadhani ni suala ambalo tunawenza kulifanyia kazi ama Wizara yenye au pamoja na sisi. (*Makofî*)

Lakini pia natoa wito kwa wananchi kwamba wakati Serikali imechukua hatua hii, basi na wao pia wajipange wawe na malengo siyo mtu anachukua tu kwa kubabaisha, anafanya mambo yake yasiyoeleweka. Ila tatizo ambalo litatokea tena ni lile alilosema Mheshimiwa mmoja hapa kwamba, hivi soko la haya mahindi yatakayolimwa itakuwaje? Kwa sababu tuna ushahidi kwamba katika mikoa hii gunia zima la mahindi lenye madebe saba limewahi kuuzwa kwa Sh. 3,000/= . Sasa hata kama ruzuku itatolewa bei ya mahindi kama ni Sh. 3,000/= kwa kweli nayo itakuwa ni kichekesho. Sasa sijui soko la mahindi la eneo hili yatakuwa yanauzwa wapi?

Kama tutaachiwa huru basi waruhusiwe pia kuuza katika nchi za jirani kwa Mikoa ya Ruvuma, wanawenza kuuza mpaka Malawi ingawa nako kuna taarifa kwamba safari hii wana mahindi. Eneo la Mikoa ya Iringa wanawenza kuuza pia Malawi na Zambia, Mbeya wanawenza kuuza Zambia na Rukwa wanawenza kuuza Zambia, kama hivyo ndivyo, basi kwa kweli tutakuwa tumefaidi kwa maana hiyo. (*Makofî*)

Lakini pia kuna suala la Serikali kukubali kuunga mkono ulimaji wa mazao fulani fulani. Sasa hayo nayo tulifikiri yafikiriwe kwa sababu kuna Wilaya nyingine kubwa kama Wilaya ya Njombe ni Wilaya yenye Majimbo matatu na kwa kweli ina hali ya hewa inayotofautiana sana katika maeneo hayo. Huwezi kusema chai ilimwe kila mahali Njombe, haiwezekani. Chai inaweza kulimwa Jimboni kwangu tu Njombe Kusini na pengine kidogo Njombe Kaskazini. Lakini Njombe Magharibi kama siyo alizeti mazao mengine yote hayastawi. Sasa nilifikiri hili suala la kwamba kila Wilaya iwe na zao moja pengine hatukuwa tumezingatia hilo, ni muhimu kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kusema kwamba, huu mpango na mkakati mzuri wa Serikali wa kuondoa umaskini, katika Kamati ya Mazingira, tumeangalia Serikali imeziwekeea utaratibu wa kutathmini utekelezaji wake mpaka ngazi fulani. Lakini tuliona kabisa tathmini ile inakosa uhusiano. Waheshimiwa wawakilishi wa wananchi kuanzia Wabunge na Madiwani, hawakushiriki katika kutathmini ute utaratibu. (*Makofî*)

Sisi tunashauri kabisa tutafute vigezo vya kutathmini, mipango hii itaendeleaje, kama fedha zinazopelekwa zinawafikia wananchi, je, fedha zinazopelekwa zinafanya kazi zilizokusudiwa na

Waheshimiwa Wabunge waone upungufu wa utekelezaji wa mpango huo na ikibidi wawasaidie wananchi kuongeza mapato kwa sababu Serikali imetoa *input* sasa sisi tuongeze mapato kusudi tuweze kuona kwamba mpango huu si wa Serikali bali ni mpango wa wananchi. Kwa hiyo, wawakilishi wa wananchi watengenezewa vigezo vya namna ya kufanya tathmini katika maeneo wanayofanya kazi. Je, fedha zilizopelekwa zimefanya kazi na ni kazi gani, je, wananchi na Mheshimiwa Mbunge, wafanye nini ili kuuboresha ule mpango, kama ni kuongeza mapato mambo gani yafanywe? Kwa hiyo, tathmini hiyo ingekuwa ya maana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Canada kupitia *Canadian Parliamentary Centre*, wameanzisha *network* ya kuondoa umaskini, pia wameanzisha *network* ya Maendeleo ya Wanawake na *network* ya *Anti-Corruption*. Sasa tulifiki wale wanajaribu kujifunza namna Wabunge, wanavyoshiriki katika kutathmini maendeleo ya wananchi hasa katika ngazi ya kuondoa umaskini. Mimi nadhani tukifanya hivyo, uwajibikaji hauwi wa Serikali pekee, bali unakuwa pamoja na sisi wawakilishi wa wananchi na wananchi wenyewe.

Kwa hiyo, wito wangu ni kwamba, Serikali ikubali tutengeneze *network* ya kutathmini mpaka vijijini kama hela zinazokwenda zinafanya kazi na wajibu wa eneo lile ni husika. Kwa hiyo na Madiwani pia wahusike. Kwa hiyo, tutakuwa hatumwachii mtu mmoja na tutakuwa tunatumia raslimali yetu ndogo kwa kikamilifu kuleta mabadiliko katika jamii tunayoishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naendelea kulifuatilia hili katika Kamati ambayo mimi naisimamia na kwa kweli ni nia yetu kwamba ikifanikiwa kufanya hivyo, Wabunge wote wajifunze kwa kupewa semina ya namna ya kufanya usimamizi wa kuondoa umaskini katika ngazi ya wananchi. Kwa hiyo, tutakuwa tunashirikiana Serikali na sisi wenyewe. Hela yetu ndogo hii izae matunda, iweze kuonyesha mabadiliko halisi ya wananchi. Wananchi wajisikie kubadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuwapa malipo Watendaji wa Vijiji. Kwa sababu sasa Watendaji wa Vijiji watakuwa na kazi ya kusimamia maendeleo, siyo kudai kodi na kufukuzana milimani na wananchi. Kwa hiyo, watasimamia maendeleo. Kwa hiyo, tathmini hii ikifanyika sisi tutajua Mtendaji gani, anafanya kazi gani na wenyewe wanaweza kuwajibika kwa kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mikataba ambayo inapaswa isainiwe na Watendaji wa Vijiji ni ile ya utendaji ya kusimamia mpango wa kuondoa umaskini kwa ngazi ya wananchi. Tukifanya hivyo haitachukua hata miaka mitatu, wananchi wetu wataanza kufanya kazi kwa bidii, wananchi wetu wataanza kupata matokeo ya jasho lao na Serikali itaanza kupata mafanikio ya mipango yake ambayo tunafikiri itakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja na naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri na wewe mwenyewe nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aje akalie kiti.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na nadhani nitajitahidi kuwa mwadilifu, usije ukaniadhibu hapa kama Mwenyekiti. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati mwenzio lakini basi nitajitahidi kusema kwa adabu kabisa leo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitumie nafasi hii kwa kweli kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha, pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafshajji, kwa hotuba nzuri kabisa ambazo kwa kweli zimetoa mwelekeo Taifa hili tunakwenda wapi katika kipindi hiki kilichobaki cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kwa kifupi sana kwa sababu mengi kwa kweli yamekwishaongelewa kwenye Bajeti hii na nataka nianze kwanza kabisa, kwa kuipongeza Serikali kwa kuona kero zinazowakabili wananchi kwa muda mrefu sasa kwa kweli zimepata majibu. (*Makofi*)

Kero mojawapo kubwa ni suala la kuondoa kodi ya maendeleo ambayo kwa kweli wote tunakubaliana kwamba, ilikuwa na usumbufu na adha kubwa sana kutoka kwa wakusanyaji wenyewe na viwango vilikuwa vikubwa. Viwango vilikuwa vinatofautiana Wilaya hadi Wilaya kwa hiyo vile vile ilikuwa inaleta tofauti ya maendeleo kati ya Wilaya na Wilaya. Lakini vile vile Serikali imeona kwamba, fedha zilizokuwa zinakusanywa siyo zote zilikuwa zinafika kwenye Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, utaratibu uliokuwepo ulikuwa unatoa kwa kweli mwanya kwa ajili ya matumizi mabaya ya fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile suala la kuona kwamba takwimu zilizokuwa zinatumika wakati wa ukusanyaji wa kodi ya maendeleo hazikuwa sahihi hata kidogo. Takwimu zilikuwa chini na hazikuwa sahihi kabisa. Unaweza kukuta Wilaya ina watu kama laki tatu, lakini unakuta wanaolipa ile kodi wanakuwa kwenye labda elfu ishirini na tano, elfu thelethini. Kwa hiyo, unakuta watu wachache wanabeba mzigo wa maendeleo kwa kweli kwa ajili ya watu wengi sana.

Vile vile usimamizi nao ulikuwa mbovu kabisa. Usimamizi mbovu ulikuwa unatokana na watendaji ambao kwa kweli walikuwa na matatizo. Matatizo ya Watendaji mojawapo ilikuwa Watendaji waliokuwepo kwa kweli walikuwa hawana sifa za kielimu ambazo kwa kweli zilikuwa zinawasaidia katika kusimamia maendeleo. Vile vile walikuwa hawana taaluma katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya wananchi. Lakini vile vile ajira zao zilikuwa haziaminiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa naomba niishauri Serikali isirudie makosa haya kwamba takwimu za kodi au za walipa kodi siyo sahihi. Kwa hiyo, nataka niishauri Serikali kwamba wakati itakapokuwa inatoa ruzuku kwa Halmashauri za Wilaya, ipeleke ruzuku kwa kuangalia takwimu sahihi na kwa sababu sensa imekwishafanyika, hakuna sababu tena ya kuangalia miaka ya nyuma jinsi makusanyo yalivyokuwa yanafanyika kwenye Halmashauri za Wilaya kwa sababu takwimu zao hazikuwa sahihi. Naomba Serikali isirudi tena katika kuona kosa hili. Takwimu za walipa kodi kwa kila Wilaya ziainishwe na zifulikane kabisa ni ngapi na Serikali itoe ruzuku kulingana na hizo takwimu na si ambazo walizokuwa nazo kwenye Halmashauri za Wilaya kwa sababu hazikuwa sahihi. (*Makofi*)

La pili, naomba kuishauri Serikali inapoajiri Watendaji kwanza, nakubali kwamb a ni vizuri waajiri Watendaji wa muda kwa kazi ya mkataba. Lakini ajira izingatie taaluma pamoja na elimu. Hili ni jambo muhimu sana, tusirudi katika ule utaratibu kwamba basi Mtendaji kule kijijini anateuliwa kadri viongozi wa vijiji wanavyoona. Tunaomba vifuatwe vigezo vya kitaaluma ili hawa Watendaji sasa kwa kweli wasimamie maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo la kwanza, naomba sasa niende kwenye jambo la pili ambalo kwa kweli ni la huduma za kiuchumi. Katika upande huu nitazungumzia suala la kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka iliyopita kwa kweli tulikuwa na mwelekeo mzuri. Kasi ya kupeleka umeme vijijini ilikuwa kubwa. Lakini baada ya kufanya marekebisho kwenye Shirika la *TANESCO*, sasa shughuli nydingi za kupeleka umeme vijijini zimesimama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi ambayo imeweza kuendelea bila kuwekeza kwenye nishati kwenye vijiji vyake. Umeme kwa *Net Group Solution* ya sasa nakubali kwamba inaweza kuwa ni suala la biashara. Lakini umeme kwa Serikali tunaomba liwe jambo la uwekezaji kwenye vijiji ili maendeleo yapatikane kutoka kule kwenye vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo kwenye vijiji vya Jimbo langu. Kuna vijiji viwili ambavyo vilikuwa havina umeme, Kijiji cha Magugu na Kijiji cha Galapo vilipata umeme kiasi cha miaka kama mitatu na nusu iliyopita na baada ya kupata umeme, vijiji hivyo vimebadilika sana. Kwa mfano, mashine za kusaga zilikuwa tatu zimeongezeka mpaka 20 na sasa hivi *TANESCO* kwa mfano, pale Magugu wanapata karibu shilingi milioni 66 kwa mwaka. Fedha hizi zilikuwa hazipo na wananchi wanapata zaidi ya shilingi milioni 150. Sasa ukweli ni kwamba, katika vijiji hivi umaskini kwa vyovoyote vile utaanza kupungua kwa sababu tayari wanayo silaha ya maendeleo. (*Makofi*)

Kijiji cha Galapo ambacho kilikuwa hakina umeme, sasa baada ya kupata umeme wanatumia zaidi ya *unit* 26,000 ambapo karibu shilingi milioni 33 zinakusanya kwa mwaka na TANESCO na wananchi wenyewe wanaotumia umeme kwa ajili ya mashine na kadhalika wanapata zaidi ya shilingi karibu milioni 75 kwa mwaka. Sasa kasi imeachwa kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali irudi na kuona namna gani sasa umeme utapelekwa vijijini kwa sababu tusipofanya hivi tukadhani umeme ni suala tu la biashara, hatuwezi kuendeleza nchi yetu. Mimi naomba vijiji vyote ambavyo viko kwenye *line* kwa mfano ya umeme na mradi wowote ambao unapita, ni muhimu kabisa Serikali ihakikishe kwamba, vijiji vinavyopitiwa na *line* vinapatiwa umeme. Hilo ni jambo la muhimu sana, tusipowekeza waache wenzetu wa TANESCO amba ni *Net Group Solution*, wafanye biashara, lakini Serikali itafute hata mfuko basi wa kuhakikisha kwamba umeme unapelekwa vijijini. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo nilitaka kugusia ni suala la huduma za afya. Wote tunafahamu kwamba, jukumu moja la Wizara ya Afya ni kudhibiti magonjwa na vile vile kupunguza idadi ya vifo hasa kwa watoto wachanga na watoto walio na umri chini ya miaka mitano na hasa ambao wanashambuliwa sana na ugonjwa wa malaria. Lakini kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha, tunaona kwamba, bajeti badala ya kuisaidia Wizara ya Afya, sasa inaongeza ugumu wa mapambano ya kuzuia malaria. (*Makofi*)

Hili limezungumzwa na mimi nataka nisisitize tu kwamba, ni vizuri tuendelee kuangalia kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Sasa Serikali inatoza kodi kwenye dawa ya ngao, kwenye malighafi ya vyandarua, kwenye dawa na vifaa, kwenye misaada na dawa kutoka kwa wahisani. Sasa utozaji wa kodi wa aina hii kwa vyovoyote vile utapunguza uwezo wa Serikali kununua dawa na hivyo kupunguza uwezo wa mapambano hayo ya kuzuia malaria na magonjwa mengine. Tunaomba kwa dhati kabisa, Serikali iondoe kodi ambayo Waziri wa Fedha ameionyesha kwenye maeneo ambayo nimeyataja na hasa kwenye dawa ya ngao, malighafi ya vyandarua, dawa na vifaa vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, jambo hili tunaona ni zito na tunaomba kabisa Serikali kwa namna yoyote ile, ione jambo hili kwamba ni zito, iondoe kodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni suala la maji. Wote tunakubaliana kwamba maji ni uhai. Vile vile, maji yanayofaa kwa ajili ya matumizi ya binadamu ni ghali kabisa kupatikana kwake kwa sababu yanapatikana aidha kwenye vilele vya milima na ardhini. Hayo ndio maji yanayoweza kufaa kwa binadamu. Sasa ipo miradi mingi ambayo ilikuwa imeachwa kwa muda mrefu sana au imechakaa au imetelekezwa kwa miaka mingi na ahadi moja ya Serikali ni kufufua miradi hii. Sasa tunaomba kabisa Serikali ijielekeze huko kufufua miradi ya maji ambayo ilikuwa imetelekezwa kwa muda mrefu katika Wilaya mbalimbali na Wilaya yangu ikiwa mojawapo. Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu, nilimwandikia barua kwamba ingekuwa vigumu sana mimi kuunga mkono hoja yake kama asingeangalia suala hilo. Lakini nashukuru nimeiona kwenye vitabu vya Bajeti ya Wizara ya Maji. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, miradi hii muhimu ambayo imetelekezwa kwa muda mrefu sasa itafufuliwa katika kila Wilaya. Hii ni ahadi moja kubwa ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nilitaka niseme juu ya barabara na bahati nzuri Mheshimiwa Marmo, Mbunge wa Mbulu, ameliulizia kwenye swalii la nyongeza asubuhi hii ya leo kwamba, Mkoa wa Manyara ni Mkoa mpya, ni Mkoa amba hauna hata kipande chochote cha lami na zipo barabara zilikuwa za Mkoa tulipokuwa kwenye Mkoa wa Arusha. Lakini Mkoa wa Manyara kwa kuwa ni Mkoa mpya unahitaji barabara zake ziangaliwe kwa namna ya kipekee.

Sasa kama alivyosema Mheshimiwa Marmo kwenye swalii lake, sikuweza kupata nafasi ya kuka kwenye *Road Board* ya Mkao wa Manyara, lakini naomba basi jambo hilo sasa lichukuliwe na Wizara ya Ujenzi kuona kwamba, kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba Mkao wa Manyara, *network* ya barabara zake zinarekebishwa. Wote kama tunavyofahamu, mtoto mchanga anahitaji mambo mengi zaidi kuliko mtu mzima. Sasa Mkao wa Manyara ni Mkao mchanga, hivyo unahitaji kuangaliwa kwa namna ya pekee kabisa katika miundombinu, huduma za kiuchumi na huduma za kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitumie nafasi hii kuwapongeza tena Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri na nitamke kwamba, naiunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. SULEIMAN AHMED SADIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wapya wote, kwa kuchaguliwa na kuingia katika Bunge hili, nawatachia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mramba, pamoja na Mheshimiwa Kigoda, kwa hotuba zao nzuri, kwa kazi kubwa waliyofanya hatimaye leo Bunge zima linaunga mkono hotuba zao. Nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutumia nafasi hii nimpongeze Ndugu Harry Kitilya, kwa kuchaguliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Kodi ya Mapato, pamoja na Ndugu Luoga kuwa Msaidizi wake. Mheshimiwa Rais, amefanya mabadiliko katika eneo hili la mapato, amewachagua hawa baada ya kuona utendaji wao wa kazi na kwa kweli na mimi naungana naye na ninawatachia kila la kheri. Lakini niwape mtihani mmoja, Bwana Kitilya na Bwana Luoga mna kazi kubwa, mmechaguliwa katika kipindi muafaka na leo mtaona kazi kubwa iliyoko mbele yenu itaanzia katika Bunge hili. Nawatachia kila la kheri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hotuba zote mbili mia kwa mia na pia kuna maeneo mawili, matatu, naomba kutumia nafasi hii kuishauri Serikali. Jukumu la Serikali ni kusimamia mapato yake katika maeneo yote, lakini katika hili Serikali bado haijatueleza lolote kuhusu eneo la mafuta. Lawama ni nyingi sana katika kodi, mianya ni mingi lakini tunapokwenda ndani katika eneo la ma futa bado Serikali haijasema kitu. Nashauri *TRA* ndio wawe wasimamizi wakubwa wa kukusanya mapato yote katika eneo la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali itueleze ni chombo kipi kinawajibika kusimamia suala la mafuta hapa nchini? Nchi zote duniani eneo hili la mafuta linakuwa ni eneo nyeti, ni eneo ambalo ndio kioo cha mapato ya Serikali. Leo katika Taifa hili tumezungumzia sana mianya, tunabadilisha mikakati kila mwaka, Waziri anakuja na hili, kesho anakuja na hili, keshokutwa anakuja na hili. Waziri atueleze hivi ni chombo gani kinawajibika kusimamia mafuta Tanzania? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemba Waziri atueleze nini hatma ya *TIPER* katika Taifa letu. Leo tulikuwa tuna *TIPER* lakini *TIPER* ile ilikuwa na mambo mengi, ilikuwa na mkakati mkubwa sana na kulikuwa na mambo mazuri sana yalikuwa yameahidiwa na Mawaziri mbalimbali. Mheshimiwa Kigoda kwa wakati wake, Mheshimiwa Shija, Mheshimiwa Yona na wengine. Kila Waziri alikuwa anazungumzia mkakati wa eneo la mafuta, lakini leo mikakati yote ile tumeisahau, badala yake kila mwaka Waziri anakuja na jipya. Tukiyumba leo katika eneo la mafuta tutaipeleka nchi yetu pabaya.

Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 70 amezungumzia mkakati katika eneo la mafuta na suala la *flow meter*. Mimi naungana na utaratibu wa kuweka *flow meter*, lakini siungi mkono jinsi *flow meter* ile itakavyowekwa. *Flow meter* ile inawekwa pale meli zinapoegeshwa, ni utaratibu ambaou utakuja kutusumbua. *Distance* ni kubwa sana kuanzia meli inapoegeshwa mpaka inapokwenda kwenye *Depot*. Leo taarifa tulizonazo ni kwamba, pale Bandarini tunaweza tukaweka *flow meter* katika maeneo ambayo wataalam walikwishapendekeza. Kuna *Main ford*. Ipo *Main ford* ya *TIPER* na ya *THA*. Lakini, hivi Waziri kwa kushirikiana na wataalam wake, amewe ka utaratibu gani wa kuangalia nchi kama *UK* au *Sweden*? Wale wenzetu hawatumii utaratibu wa *dipstick*. Wana mambo haya ambayo tunakwenda nayo sisi leo. Lakini sisi badala ya kufuata utaratibu ambaou wenzetu wanafanya, wataalam wanatushauri, tunakwenda na utaratibu ambaou sisi wenye tunajiweke. Hili ni tatizo kubwa. Bwana Kitilya una mtihani mkubwa sana katika eneo la mafuta na katika eneo la forodha. Kwa kweli naomba macho yenu mtupie pale, uchumi wa nchi upo pale. Leo ndani ya Bunge kila Mbunge anayeinuka anasema kodi ya maendeleo imefutwa, tunashereheke. Lakini imetokana na nini? Imetokana na kukua kwa uchumi, imetokana na kazi nzuri ya kukusanya mapato katika Taifa letu. Tusipokuwa makini katika eneo la mafuta, tutakuja kupata mattatizo huko tunakokwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na utaratibu mzuri wa *transit* ambao umependekezwa na Waziri wa Fedha, sina matatizo, tuone utaratibu huo utasaidiaje. Lakini utaratibu ambao labda Waziri autupie macho ni lile suala la siku 15 kuhusu mafuta yatakayoingia na kulipiwa ushuru. Hapa tunachofanya ni kudhibiti, lakini katika udhibiti wetu tunaweza tukaharibu. Siku 15, je, yule anayeleta mafuta alete mafuta ya siku 15 tu? Baada ya siku 15, mafuta yatakapoisha tutafanya nini? Kwa nini tusjiwekee utaratibu angalau tuenze na siku 30? Wenzetu wadau wamependekeza katika *paper* yao siku 60. Mimi naishauri Serikali ianze na siku 30 angalau eneo hili nyeti tuenze kukabiliana nalo. Kuna matatizo mengi hapa, lakini suala la *flow meter* nalo tuwe makini. Ziko *flow meter* za kila aina, tusije tukapata wadanganyifu wachache wakafaidika hapa. Iwe ni *open tender, specification* za Kimataifa zinajulikana, zitangazwe tupate *flow meter* ambayo haitaleta bughudha. Kesho tukipata mgomo hapa nchi itapata tatizo kubwa katika eneo la mafuta. Naishauri Serikali iwe makini kweli katika eneo hili nyeti. Mawazo ya Waziri wa Fedha ni mazuri, nayaunga mkono, naomba ayaboreshe hatua kwa hatua.

Eneo lingine ambalo ningeomba Waziri alitazame katika uchumi wa Taifa hili, tuangalie hawa wafanyabiashara wadogo wadogo. Tunapozungumzia wafanyabiashara wadogo ni hawa ambao wameanzisha uchumi wa kujitegemea. Leo wengi wanamiliki *taxi*, wanamiliki daladala, wanamiliki mafuso, lakini matairi ambayo wanayatumia yanatozwa ushuru wa asilimia 85, *nylon tyres*. *40 percent suspended duty, 25 percent import duty, 20 percent VAT*. Huyu mtu mdogo hatukumtazama badala yake tunakwenda kupunguza ushuru wa tairi za *Radial Tyres* wanayotumia wakubwa kama vile *Scandnavia, Saddiq Line* na wengine wote. Huyu Mfanyabiashara mdogo hatukumuangalia. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, wameleta vilio na wengine wanasesma ninyi wakubwa mmejipendelea, mmepunguza ushuru kwa matairi makubwa ya magari ya wakubwa, sisi wenye *taxi* ambao tunatumia matairi ya China, ushuru ni asilimia 85, Wabunge tupunguzieni ushuru wa muda, kazi yetu ni kushauri, tunaomba Serikali isikie kilio hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, angalau kwa hatua za awali kwamba, *suspended duty* angeipunguza kutoka asilimia 40 angalau mpaka kumi au kwa kuanzia twende na ishirini. Kodi nyingine zingebaki, *25 percent import duty, 20 percent VAT*. Twende hapo kwa kuondoa tu *suspended duty* aidha yote, robo au nusu. Wabunge wote wana magari humu ndani, lakini suala hili hakuna hata mmoja ambaye ameliona. Naomba sana Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Shamba la Dakawa. *Dakawa Rice Farm* ni shamba kubwa lipo pale Dakawa katika Wilaya mpya ya Mvomero. Ni muda mrefu tumelizungumzia Shamba la Dakawa, mpaka leo Serikali haijatoa tamko lolote. Mheshimiwa Waziri siku za nyuma alitoa tamko kwamba, lile shamba analigawa nusu kwa wakulima wadogo na nusu wanapewa Kiwanda cha Mtibwa walime zao la miwa. Mtibwa wamepewa *Dakawa Ranch*. Lile eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya Mtibwa, nashauri wapewe wakulima wadogo walime miwa kama Wizara ilivyopendekeza kwa ajili ya Kiwanda cha Sukari. Lakini kuna mgogoro pale, kuna tatizo kubwa la umwagiliaji. Lile shamba kuna watu wachache sasa hivi wanatumia Polisi, wanatumia mabavu, wanamwagia katika maeneo yao. Serikali tumezungumza mwaka 2001 Waziri Keenja nilikwenda naye pale katika shamba lile akatoa tamko lakini utekelezaji mpaka leo haupo. Ningeshauri Serikali katika Shamba la Dakawa sasa ikae iona ni jinsi gani Serikali itatoa lile shamba kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunazungumzia elimu. Lakini kwa upande wa elimu, Serikali tunaipongeza, imejitahidi sana, lakini Vyuo vyetu Vikuu vina matatizo. Chuo Kikuu cha Mzumbe ni Chuo Kikuu kipyaa. Kina matatizo ya *computer*, kuna matatizo ya vitendea kazi. Mzumbe leo hata majengo yaliyopo ni yale yale ya zamani. Kama tumeamua kusema elimu, basi iwe elimu ya juu, iwe elimu ya msingi, tuwasaidie. Ningeomba kilio cha Mzumbe kisikilizwe kwa mapana na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ada za Chuo Kikuu cha Mzumbe bado ni kilio cha muda mrefu. Wanafunzi wa Mzumbe wako katika hali ngumu. Leo Chuo Kikuu cha Mzumbe ni kipyaa, kichanga na kwa hiyo kinahitaji malezi. Nafikiri wakati umefika sasa tuhakikishe kwamba, Chuo kile tunakitupia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametangaza Wilaya mpya, mojawapo ikiwa ni Wilaya ya Mvomero. Leo kwenye Bajeti tunaona zimetengwa shilingi milioni mia kwa ajili ya ujenzi wa

Boma kila Wilaya. Tunasema uchumi umekua, tunatenga milioni mia za ujenzi wa Boma, hivi mnategemea tuanze na yale yale matofali ya kuchoma? Hizi ni Wilaya mpya zilizotangazwa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Hebu twende na wakati, uchumi unakua, tuongeze nguvu kidogo, tuongeze bajeti ili hizi Wilaya mpya ziwe Wilaya za mfano huko mbele tunakokwenda. Akija Rais mwingine akigawa Wilaya, Wabunge wakasema tunataka zifanane na zile Wilaya za Mkapa. Ningombwa Serikali ishauri hilo katika Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie suala la umeme. Katika Jimbo la Morogoro Kaskazini, Tarafa ya Mgeta, haina umeme. Mradi umeanza, sasa hivi umesimama. Ningombwa tupate baraka za Wizara ili mradi uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie umeme Sumve. Serikali kupitia *TANESCO* iliahidi kupeleka umeme Sumve katika Kijiji cha Malya na bajeti ilikubaliwa ianze Januari mwaka huu wa 2003. Mpaka leo Malya, hakuna nguzo, hakuna nyaya, ahadi ya Serikali kupitia *TANESCO* ipo hewani. Namwomba Waziri ahakikishe umeme unapatikana Sumve. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kupeleka shilingi milioni 30 kwa ajili ya Mradi wa Maji Sumve na Malya. Leo Sumve na Malya shilingi milioni 30 zimetengwa, pampu ya maji imepelekwa, sasa naomba Wizara ihakikishe kwamba, maji na umeme Sumve vinapewa kipaumbele katika Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimalizie kwa kuzungumzia *PSRC*. *PSRC* wametimiza miaka kumi. Huu ni mwaka 2003 tangu 1993. Katika kipindi cha miaka kumi, ningombwa Serikali ifanye tathmini ya kazi iliyofanywa na *PSRC* lakini na sisi kama Wabunge, ningelishauri Bunge hili lifanye tathmini kupitia Kamati zetu za Bunge, tuone *PSRC* katika kipindi cha miaka kumi wamefanya mini, mapungufu yao ni nini na sisi kama Wabunge, tuweze kuishauri Serikali katika eneo hili. Ningeshauri Kamati hizi za kufutilia tathmini za *PSRC*, ikiwezekana zipate baraka mapema zaidi kupitia Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie na kilimo. Katika eneo la kilimo tuna mkakati mzuri, lakini mkakati wetu huu hebu tungeiga mfano wa *agents* ambazo zipo na zinafanya kazi nzuri. Leo tuna *TANROADS* wanasmamia barabara, wanafanya vizuri, kila Mbunge anapata majibu ya kuridhisha. Leo tuna *TRA* wanasmamia mapato, wanakusanya, wanasmamia wanaleta. Kwa hiyo, majibu yanapatikana. Kwenye kilimo tunashindwa nini kuanzisha *agent* ambayo itasimamia kilimo na kufutilia ahadi za Serikali? Upande wa kilimo tunayumba tu, kila mwaka mkakati huu, kwa nini tusiwe na chombo imara cha kusimamia kilimo kama vile *TANROADS* au *TRA*? Tutafika mahali tutakuwa na majibu mazuri na ya uhakika na tathmini itafanyika. Leo kilimo hakina mwenyewe. Utaratibu ni mzuri, mwaka huu kila Wilaya itataka iweke zao moja au itoe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa kutenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa kisasa. Wanamichezo wamelipokea hili kwa furaha kubwa na wana furaha kubwa na Serikali ya Rais Benjamin William Mkapa na mimi kwa mtazamo wangu, hii ni hatua ya awali. Nina hakika kadri miaka inavyokwenda, bajeti itakuwa inaongezeka siku hadi siku. Hapa tunalipongeza sana hilo.

Mwisho tena nipongeze suala la kuondolewa kwa kodi ya maendeleo. Kodi ya maendeleo ilikuwa ni tatizo Vijiji. Wananchi walikuwa wanasmabuliwa, wengine wanakamatwa na balskeli zao wanapelekwa Vituo vya Polisi, wakati mwingine kulikuwa na risiti za ajabu ajabu, utaratibu mzima wa kodi ya maendeleo ulikuwa sio mzuri. Lakini tatizo hasa lilikuwa kwamba, hata Halmashauri zetu zilikuwa hazina utaratibu mzuri wa kukusanya kodi ya maendeleo. Naipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo na pia wananchi waelewe kwamba kilichofutwa ni kodi ya maendeleo na sio michango ya maendeleo. Michango ya maendeleo tunaomba wananchi wetu waendelee kuchangia kwa ajili ya maendeleo ya Vijiji vyao. Isije ikatokea dhana kwamba Serikali imefuta kodi zote. Serikali imepunguza kero za kodi Vijiji na Mijini. Naomba kwa kutumia Bunge hili, wananchi wajue bado tunataka michango yao kwa ajili ya maendeleo yao na ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda bado unaniruhusu. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofit*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Ahsante sana Mheshimiwa Sadiq na hasa kwa suala la Sumve. Tunaendelea na Mheshimiwa Margareth Bwana, atafuatiwa na Mheshimiwa Isaac Cheyo.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusiana na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri wote wawili. Ninatumia nafasi hii kutamka rasmi kwamba, naziungwa mkono hoja hizo mia kwa mia. (*Makofit*)

Pia, natumia nafasi hii kumpungeza sana Ndugu Kitilya, pamoja na Ndugu Luoga, kwa uteuzi wao uliofanywa na Mheshimiwa Rais. Ni wazi kwamba, Mheshimiwa Rais ameridhika na utendaji wao wa kazi na ninaamini kabisa kwamba, atashirikiana vyema na wananchi katika kuhakikisha kwamba, wanatiniza vyema majukumu yao. Natumia nafasi hii pia kumpungeza Ndugu Lauo na wote anaoshirikiana nao katika suala zima la ukusanyaji wa mapato *TRA* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato wanayoifanya hapa nchini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza kwa dhati Ndugu Sumri Abdallah Salum Mohamed, Mbunge wa Mpanda Magharibi, kwa kuchaguliwa kwake, Ndugu Nazir Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Ndugu Edward Ndeka, Mbunge wa Kasulu Kusini na Ndugu Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, kwa ushindi wao wa kishindo walioupata. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza na Wabunge wengine wote ambaa wamechaguliwa katika kipindi hiki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na Bajeti kama ilivyowasilishwa na Mawaziri wetu wawili. Nimefurahishwa mno na yale yaliyozungumzwa ndani ya Bajeti hiyo, kwa kweli sehemu kubwa ya Bajeti hiyo imewagusa wananchi moja kwa moja. Nitapenda tu nitaje baadhi ya maeneo ambayo mimi binasifi yamenigusa mia kwa mia. La kwanza ni ile ada iliyokuwa ikitolewa au ikilipwa wakati wa kuomba kibali cha kuzika katika maeneo ya Mjini, kwamba hii imefutwa. Kwa kweli hii ilikuwa ni kero. Mtu amefiwa lakini anatakiwa kulipa kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya kupata kibali cha kuzika. Hii nayo kwa kweli wa meipokea kwa mikono miwili na wamefurahishwa sana na uamuji huu wa Serikali. (*Makofit*)

Lakini la pili, limeshazungumzwa na wenzangu kuhusu suala la uwanja wa kisasa wa michezo. Mheshimiwa Rais wetu amezungumza kwamba, atahakikisha kwamba uwanja huu unakamilika kujengwa kabla hajamaliza kipindi chake cha uongozi na sasa tumeanza kujionea sisi wenyewe, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imetenga bajeti ya shilingi bilioni tano ya awali kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kimefurahisha kupita mengine pia ni suala la kodi ya maendeleo kufutwa. Wote tunajua kwamba, tumekuwa tukipata matatizo makubwa sana na wananchi wetu mpaka ikafikia mahali wengine wakawa wanakimbia majumba yao, wanalala nje kwa ajili ya kukimbia msako huu wa kodi. Kwa hiyo, kwa kweli hoja hii wananchi wameipokea kwa mikono miwili na wamefurahishwa sana.

Lakini lingine ni kutengwa kwa Sh. 70,786,000/= kwa ajili ya Polisi kwa lengo la kusaidia kukabiliana na uhalifu nchini. Kwa kweli hii pia tumeipokea na tumefurahishwa sana na ninaamini kwamba itakuwa imesaidia kwa kiasi kikubwa kutafuta vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuliimarisha hili Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nirudi kwenye hoja ambayo nina mambo matano ningependa niyazungumzie. La kwanza ni kuhusiana na pendekezo la Serikali kutoza asilimia 15 ya ushuru wa bidhaa ya mifuko ya plastiki inayoagizwa kutoka nje na ile inayozalishwa hapa hapa nchini. Naupongeza sana uamuji huu wa Serikali na wote tunakubaliana kwamba, kwa kweli mifuko hii ya plastiki inachangia na inaendelea kuchangia katika suala zima la uchafuzi wa mazingira. Ukiangalia katika fukwe za bahari, maziwa na mito yote imejaa mifuko ya plastiki. Sasa katika hii pamoja na kwamba Serikali imeweka kodi ya asilimia 15, mimi nilikuwa napenda nitoe pendekezo na niungane na Kamati ya Maliasili

na Mazingira, ambayo mwaka 2002 walifanya ziara ya kutembelea Jiji la Dar es Salaam na katika maeneo mbalimbali wakajionea namna mifuko hii ya plastiki inavyochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira. Sasa katika hili nilikuwa napenda kuishauri Serikali ichukue hatua zaidi ya kufuta matumizi ya mifuko hii mapema iwezekanavyo kwa sababu kwa kweli haisaidii isipokuwa inaendelea tu kuchangia uchafuzi wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hili ni suala la wastaifu. Ninaipongeza sana Serikali yetu kwa kuangalia wastaifu hawa na hatimaye kuweza kutoa kauli ambayo imeingizwa ndani ya bajeti kwamba kuanzia sasa Wastaifu wote watalipwa pensheni kuanzia Sh. 20,000/= kwa mwezi. Katika hili nilikuwa napenda nifahamu kwamba, kuna wale wastaifu ambao walishachukua pesa zao kwa mkupuo wa miaka 15 na kuchukuliwa kwa fedha ile kulisababishwa na kiasi kidogo cha fedha ambacho walikuwa wanapata. Unakuta mtu pensheni yake aliyokuwa amepangiwa ni Sh. 150/= kwa mwezi. Baada ya kustaifu maana yake inabidi arudi Kijiji kule alikotoka. Sasa kufunga safari kuja kuifuata ile Sh.150/= kwa kweli unakuta gharama anayoipata ni kubwa sana ukilinganisha na kile kiasi cha fedha anachokwenda kukichukua. Sasa katika hii walilazimika kuchukua pensheni yao ya miaka 15. Mungu bariki hawa watu mpaka sasa wapo hai, pamoja na kwamba walifanya kazi yao vizuri mpaka kufikia hatua ya kustaifu, lakini bado wangali hai mpaka wakati huu. (*Makofi*)

Nilikuwa naomba nifahamu Serikali inasema nini kuhusiana na wale wastaifu waliozwishachukua pensheni zao kwa mkupuo wa miaka mitano? Wastaifu hawa watashirikishwa vipi katika huu utaratibu wa sasa? Nilikuwa ninadhani kwamba kuna haja ya Serikali kuliangalia hili, kwa sababu kwanza kitendo cha kukaa miaka 15 baada ya kustaifu wanastahili ponezi kubwa sana, kwa sababu wengi wao baada ya mtu kustaifu unakuta haizidi miaka mitano sita wanakufa. Lakini watu hawa mpaka sasa bado wapo na wanashiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali iliangularie na ione inatamka nini kwa hawa wastaifu ambao bado wapo kwamba na wenyele watashirikishwa katika huu utaratibu wa sasa au utaratibu utakuwaje? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa upande wa hawa wastaifu, kumekuwepo pia na kero mbalimbali ambazo wastaifu hawa wamekuwa wakizipata wakati walipokuwa wanafuatilia fedha zao huko Wizarani kabla ya huu utaratibu mpya wa kuweka *centers* katika Mikoa yetu. Sasa nilikuwa nataka njue kwamba, je, Serikali imejandaa vipi katika kutatta matatizo mbalimbali ambayo yanawahu hawa wastaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la barabara Vijijini. Ninapenda nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali yetu, kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kufanya sasa hivi ya kuunganisha barabara zinazounganisha Mkoa mmoja na mwingine. Nina furaha kutamka kwamba, kwa upande wa Mkoa wa Rukwa, ile barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, sasa hivi taratibu zinaendelea za kuweka madaraja na ninaamini baada ya utaratibu wa madaraja kukamilika, ambapo kwa taarifa tuliyonayo ni kwamba ujenzi wa madaraja yale unategemea kukamilika Desemba, mwaka huu wa 2003. Kwa hiyo, ni wazi kwamba, mara tu baada ya madaraja yale kukamilika, shughuli za uwekaji wa lami zitaanza kwa awamu kwa kilomita 50 kutoka Tunduma mpaka Ndalambo.

Kwa hiyo, utaratibu huu ni nzuri. Lakini pia nilikuwa ninapenda niiombe Serikali kupitia utaratibu wake wa *TASAF*, *TASAF* ilipoanzishwa ilianza na baadhi ya Wilaya kama majaribio na utaratibu huu unategemewa kumalizika katika kipindi hiki. Nilikuwa ninaomba kwamba, kuanzia awamu inayofuata ya huu mpango wa *TASAF*, nguvu zielekezwe zaidi katika vijiji na Serikali itoe *support* ya kutosha *support* huu mifuko wa *TASAF* ili kuwezesha utengenezaji wa barabara za vijiji uweze kukamilika na kuweza kuwepo na mawasiliano mazuri kati ya kijiji kwa kijiji katika suala zima la mawasiliano. Kwa sababu huko vijijini ndiko waliko waza lishaji wengi wa chakula na mazao mbalimbali ya biashara.

Vijijini sasa hivi hakuna barabara, tunapasua tu mapori, tunapita tu kwenye majani, ni marefu kiasi ambacho kwa kweli huwezi kujua kwamba hapa ni barabara. Sasa nadhani kuna haja ya utaratibu huu wa *TASAF* utakapokuwa umekamilika ambao utaunganisha Wilaya zote katika nchi, basi mifuko huu uweze kutunishwa ili utengenezaji wa barabara katika vijiji uweze kutiliwa maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni suala la mkakati wa kuimarisha viwanda unaoandaliwa hivi sasa hususan katika eneo la nishati. Mheshimiwa Waziri, hili amelizungumza na sisi pia katika Kamati yetu ya uwekezaji na biashara tulifanya ziara ya kutembelea katika viwanda mbalimbali na kupata nafasi ya kuzungumza na *management* ya viwanda hivyo. Lakini kikubwa ambacho tulikuja kukigundua kule kila tulipokuwa tukipita, tulikuwa tukilalamikiwa kuhusu gharama kubwa za umeme. Gharama zile ndiyo zinazochangia kwa kiasi kikubwa upandaji wa gharama za bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda kile. Sasa katika mazingira haya, kuna haja Serikali kulitazama hili. Kwa sababu kitakachokuja kujitokeza ni kwamba tutajikuta katika hili Soko la Afrika Mashariki, bidhaa zetu zitashindwa kupata soko. Kwa sababu ya gharama kubwa ya uzalishaji ya bidhaa ile.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, kuna haja ya kulitazama hili na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu, kuhakikisha kwamba, umeme haukatikikatiki na kuhakikisha kwamba bidhaa zetu zinazozalishwa hapa nchini kunakuwa na unafuu kwa kiasi kikubwa ambao wenye viwanda wamekuwa wakilalamika kwamba gharama ya umeme ni kubwa mno na ndiyo inayochangia kwa kiasi kikubwa upandaji wa bidhaa ile inayozalishwa.

Lingine Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na Watendaji wa Vijiji kulisipwa na Serikali. Kwa kweli hii imeleta nafuu kubwa sana kwa Halmashauri zetu. Halmashauri zetu zilikuwa na kazi kubwa sana katika maeneo ya kuwalipa Watendaji hawa na ilifikia mahali sasa ilibidi Watendaji hao watumie nguvu kuhakikisha kwamba wanapata fedha za kodi ili kuweza kupata pesa ya kwenda kuwakilisha kule hatimaye na wao waweze kupata mishahara. Lakini kwa kufanya hivi, Serikali imeisaidia kupunguza mzigo kwa Halmashauri na pia kuwawezesha Watendaji wale kufanya kazi yao kwa uhakika, wakiwa na matumaini kwamba, wana uhakika wa kupata mishahara yao kwa mwezi.

Kwa hayo, machache Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache juu ya hotuba hizi mbili ambazo ziko mbele yetu. Kwanza kabisa, naungana na wenzangu kuwapongeza Wabunge wote wapya walioingia ndani ya Bunge hili kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika mwezi uliopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabla sijasema yale machache ambayo nataka kuchangia, nilitaka kwanza tukumbushane, mimi nimeingia Bungeni mwaka 1995 na nilipoingia ndani ya Bunge hili, hali ya uchumi wetu ilikuwa mbaya sana. Lakini leo tunazungumzia uchumi ambao unakua kwa asilimia 6.2, mwaka 1995 uchumi ulikuwa unakua kwa asilimia moja na nusu. Leo uchumi wetu unafanya vizuri sana kiasi kwamba mfumuko wa bei umepungua kutoka asilimia 40 mwaka 1995 na leo hii tunazungumzia asilimia 4.2. Mwaka 1995 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa sawa na manunuza ya nje ya mwezi mmoja. Leo tunazungumzia bilioni 1.5 dola za Marekani ambazo ziko sawa na manunuza ya bidhaa na huduma kutoka nje ya miezi nane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama *performance* ya *economy* yetu miaka nane iliyopita ni nzuri sana. Lazima tutoe pongeza kubwa kwa Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa uwezo wake mkubwa wa kujenga utulivu wa uchumi katika nchi yetu (*Micro-economy Stability*). Bila utulivu ndani ya uchumi hatuwezi hata kidogo tukaendelea. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kazi hiyo kubwa. (*Makofii*)

Pili, ningependa nivipongeze vyombovya Serikali. Kwanza ningependa kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri sana ambayo imefanya. *TRA* imeongeza makusanyo ya mapato, kodi kutoka shilingi bilioni 25 miaka minane iliyopita au miaka sita iliyopita hadi kufikia sasa shilingi bilioni 105. *TRA* inastahili pongeza kubwa ingawa makusanyo hayo siyo makubwa, kwa sababu bado kuna mianya mikubwa ya ukwepaji wa kodi na tunaamini kwamba, kutokana na uteuzi mpya uliotolewa jana na Mheshimiwa Rais wetu, vijana hawa ambao wameteuliwa kuongoza *TRA* wataweza kuziba mianya hiyo. (*Makofii*)

Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake mzuri sana uliofanya kutozwa kodi ya VAT katika shughuli zake za biashara. Serikali iliamua vizuri sana kwamba shughuli zake za manunuzi ya bidhaa na huduma zitozwe kodi ya VAT na hiyo imeongeza mapato makubwa kwa upande wa Serikali. Ningependa Serikali ifikirie kwa makini zaidi iamue vile vile shughuli nyingi za biashara ambazo inazifanya zitozwe kodi ili kuiwezesha *TRA* kuongeza mapato yake na kwa kweli ni kuiwezesha Serikali yenewe kwa sababu mapato yanarudishwa Serikalini kufanya kazi za kuendesha Serikali. Nilikuwa nafikiria kwa mfano, Serikali inaamua kwamba mali zake zote zilipiwe Bima, vitu kama magari, nyumba na mali nyingine zilipiwe Bima, Serikali inaweza ikafikiri kwamba ni fedha nyingi sana. Lakini hizo fedha zinakwenda wapi? Hizo fedha zitaingia ndani ya uchumi, zitazunguka ndani ya uchumi na hatimaye zitaingia mikononi mwa *TRA* na kuongeza mapato yake.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba, ukichukua Serikali kama Serikali, *it is a huge business corporation* na inaweza ikaongeza sana mapato kwa Serikali na kwa uchumi wa nchi kama itaamua kutozwa kodi katika shughuli mbalimbali za biashara ambazo inafanya, kama ilivyoamua kutozwa kodi ya VAT katika manunuzi ya bidhaa na huduma za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo kingine ambacho nilitaka nikipongeze ni *Bank of Tanzania (BOT)*. Hiki ni chombo ambacho kinaangalia jinsi uchumi wetu unavyofanya kazi. Ukiipongeza Serikali kwa kujenga utulivu ndani ya uchumi, kwa kweli unaipongeza *BOT*. *BOT* imefanya kazi nzuri hasa kwa kuhakikisha kwamba vigezo vyote hivyo ambavyo tunavizungumzia katika kupima maendeleo ya uchumi, *BOT* kazi yake ni kuhakikisha kwamba, vinakuwa katika uwiano ambao unatakiwa.

Kwa mfano, ujazo wa fedha ndani ya uchumi. Miaka miwili, mitatu, iliyopita nilisimama Bungeni hapa kuzungumzia juu ya mfumko wa bei kwamba wakati ule ilikuwa ni vigumu sana kwangu kuamini kwamba mfumko wa bei ulikuwa unapungua kwa sababu uzalishaji wa mali ndani ya viwanda, uzalishaji wa mazao makuu ya kilimo yote yalikuwa yanapungua. Kwa hiyo, isingekuwa rahisi kwangu wakati ule kukubali kwamba, mfumko wa bei ulikuwa unapungua na nikasema kwamba mfumko wa bei unapungua kwa sababu *BOT* ni makini kupunguza fedha ambazo zilizagaa katika uchumi.

Lakini nikashauri kwamba, mkakati ule unaweza tu ukasaidia Serikali kupunguza mfumko wa bei kwa kipindi kifupi. Baadaye ni lazima mfumko wa bei upunguzwe kutokana na nguvu za soko, *forces of supply and demand*. Leo katika kitabu cha Waziri wa Fedha anatueleza kwamba, mfumko wa bei sasa unapungua kutokana na nguvu ya soko. Hii inaonyesha kwamba uchumi unakua. Kwa hiyo, naipongeza sana *BOT* kazi hiyo. (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la shilingi ya Tanzania kupungua thamani. Hili ni suala zito na tumeambiwa kwamba *BOT* imeachia shilingi icheze kutokana na nguvu ya soko na tunaona thamani ya shilingi inapungua kutoka shilingi 800 kwa dola moja mpaka hivi sasa shilingi 1,000 na kitu.

Mimi nasema kwa uchumi dhaifu kama wa Tanzania, siyo sahihi kuiachia shilingi iwe *regulated* na nguvu za soko. Shilingi tukiiachia ipoteze thamani yake, itakuwa ni matatizo kwa uchumi wa Tanzania. Kwa sababu tungekuwa na uchumi mzito, uchumi mzuri ambao unazalisha bidhaa na huduma kwa wingi, thamani ya shilingi ikipungua maana yake nini? Maana yake mauzo yanaongezeka, tunauza bidhaa nyingi nchi za nje, lakini kwa sababu hatuna cha kuuza, ni lazima tulinde shilingi yetu isipungue sana thamani yake kwa sababu matokeo yake ni kwamba, wananchi wataanza kupata matatizo sana kiuchumi ndani ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* ya pili ambayo nilitaka niizungumzie ni ibara ya 44 hadi 47. Nilikuwa nataka nizungumzie juu ya hizi fedha ambazo tumeweka akiba Benki Kuu ambayo imefikia shilingi bilioni 1.5 *dollars* ambayo ni kama *trillion 1.5*. Hizi ni fedha nyingi sana. Ningemba Waziri wa Fedha, atueleze mchanganuo wa fedha hizo. Ninaanza kuamini kwamba, fedha hizo ni mikopo au misada ambayo ina masharti magumu. Sidhani kama sehemu ya fedha hizo inatokana na nguvu zetu sisi wenewe, kutokana na mauzo ya bidhaa ambazo tunazalisha hapa nchini. (*Makofi*)

Kama sehemu kubwa ya fedha hizo ni kutokana na mauzo ya bidhaa na huduma tunazozalisha hapa nchini, basi ningependekeza kwa Serikali kwamba, sehemu kubwa basi ichukuliwe iwekwe kwenye

ku-support budget yetu. Kwa mwaka huu tumechukua shilingi bilioni 21.36 ambayo tumeipeleka ku-support budget. Lakini kwa bajeti ambayo ni tegemezi kama ya kwetu, kwa nini tusitumie fedha hizi kwa wingi zaidi ili tupunguze bajeti yetu kutegemea misaada kutoka nje. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali itoe mchanganuo huu ili tujuue hiki kiasi cha fedha ya akiba ni fedha za aina gani na masharti yake ya kuzitumia katika uchumi wa nchi yetu ni yepi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa nijielekeze kwenye ibara ya 44. Ibara hii ya 44 inatoa mambo mbalimbali jinsi gani fedha zetu zitagawiwa katika bajeti hii na naipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwamba wameamua kupeleka fedha za kilimo moja kwa moja kwenye Wilaya. Lakini ningombwa sana Serikali iwe macho, ikiamua kupeleka hizi fedha moja kwa moja Wilayani. Kwa sababu kule hatuna *capacity* katika Idara hizi za Kilimo. Hatuna wafanyakazi ambao wana uwezo wa kuzitumia hizi fedha kwa ufanisi mpaka mkulima akaona faida au akaona mafanikio kutoptokana na hizi fedha. Imani yangu ni kwamba, hizi fedha zikifika kule Wilayani zinaweza zikatumiwa vibaya. Kwa hiyo, naomba sana hizi fedha wakizituma kule, Serikali ikahakikishe kwamba, zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Pili, ni hiki kifungu cha sita, kinachohusu kuwawezesha sasa Wakuu wa Wilaya ili wapate fedha moja kwa moja kutoka Wizarani. Mimi hili nimelifurahia sana. Kwa sababu ukitazama huko Wilayani hivi sasa Wakuu wa Wilaya ni tegemezi wakubwa wa Halmashauri na mara kwa mara hata maamuzi yao ya utawala yanapingwa pingwa kutoptokana na ufukara wa Ofisi zao. Hawafanyi mambo kulingana na jinsi ambavyo wangependa wayafanye kwa sababu Ofisi zao hazina kitu. Ili Mkuu wa Wilaya afike Wilayani, ni lazima ambembeleze Mkurugenzi, apate mafuta kwenye gari yake. Sasa katika hali hiyo huwezi ukamtegemea Mkuu wa Wilaya afanye kazi ambayo amejipangia na kwa kweli hicho ni kinyume cha utawala bora ambao Serikali yetu ya Awamu ya Tatu inauzungumzia mara kwa mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bajeti hii nimeipenda sana. Niombe tu Serikali kwamba lengo lake la Bajeti hii ambalo ni kufikia makusanyo ya ndani asilimia 13.2 ya Pato la Taifa, lengo hilo linaweza likafikiwa ikiwa tu Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kuna utulivu ndani ya uchumi wetu, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa na Serikali itahakikisha kwamba, umeme unafikishwa katika vijiji ambavyo bado havijapata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili suala la umeme, ningependa kuchukua nafasi hii niishukuru Serikali kwamba, Wilaya yangu ya Kyela imeweza kufikisha umeme katika Kijiji cha Boda, imeweza kufikisha umeme katika Kijiji cha Busale, imeweza kufikisha umeme katika Kijiji cha Ipinda, hivi sasa naomba ifikishe umeme katika Kijiji cha Matema.

Nakushukuru sana na ninaunga mkono hotuba hii ya bajeti. (*Makofii*)

MHE. PHILIP S. MARMO: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango mdogo katika hotuba mbili hizi, kwanza ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2003/2004 na Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha, kwa mwaka 2003/2004. Kabla sijatoa mchango wangu huo, naomba niwapongeze Wabunge wote wapya walioingia katika Nyumba hii wa vyama vyote. Napenda kusema kwamba Nyumba hii ina kazi kubwa sana kama utapenda kufanya kazi. Pia kama hupendi kufanya kazi unaweza kufanya hivyo, lakini hukumu yake ni baada ya miaka miwili na nusu. Karibuni sana. (*Makofii*)

Nawapongeza sana Mawaziri wote wawili na watumishi wa Wizara zao, kwa kazi ngumu ya kufikisha hotuba hii ya Bajeti mbele yetu leo. Pia naupongeza Uongozi mpya wa TRA, Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga na wenzao wote katika TRA, kwamba mbele yenu kuna kazi kubwa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Tunawatakia fanaka tele na kila la kheri. Lakini kazi hii kubwa tunaomba muwasaidie wananchi wa Tanzania kwa uwezo wenu wote kwa vile katika hotuba yangu hii nitapendekeza angalau muongeze mapato ya ndani kwa mara mbili ilivyo sasa na inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamesema Bajeti hii ni nzuri na mimi pia nasema ni nzuri. Lakini kusema kuwa ni nzuri tu maana yake nini au ni ile ya Kiswahili kusema kwamba uzuri uko katika macho ya anayeona au kwako ni chongo kwangu ni kengeza. Hapana! Bajeti nzuri lazima iwe na sifa

ambazo zinakubalika duniani kote na labda niwakumbushe wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwamba, Bajeti nzuri inatakiwa iangalie hasa maeneo matano muhimu.

Kwanza, inatafuta mapato kwa haki, inatoza kodi kwa bidhaa za kifahari na kutoza kodi kwa watu wenye uwezo, lakini inawapa unafuu wazalishaji, wajenga uchumi, hawa ni wakulima wetu, hawa ni wavuvi, ni wafugaji, wenye viwanda, wenye migodi na kadhalika. Pili, jitihada lazima ilekezwe ili kufanya Bajeti hiyo iwe nzuri, kwa walaji kama nilivyosema, wa bidhaa za kifahari, pombe za kifahari, vinywaji vingine nya kifahari, sigara za kifahari, magari ya kifahari. Tatu, hata siku moja, Bajeti nzuri haiwezi kuwa na lengo la kufurahisha wananchi tu kwamba hatimaye baada ya miezi kumi na miwili pengine tumefikia hali ya kuchapisha noti maana yake kumekuwa na mfumko labda wa bei.

Nne, Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti nzuri, ni Bajeti yenye upeo wa muda mrefu. Kwa sababu sisi leo tuko hapa, lakini baadaye wenzetu watakuja, wasituone kwamba tulikuwa na ufinyu wa kuangalia mbele na kwa misingi hii naweza kusema kwa kiwango kikubwa Bajeti hii ni nzuri. Lakini hapa kwa kila upeo, kila upeo tunapotegemea asilimia 45 toka nje kwa matumizi yetu siyo upeo wa mbali, sio jambo zuri. Lakini hili suala la kwamba fedha zatoka kwa wafadhili mimi hainibughudhi hata wakileta asilimia 75 hii haingetubughudhi. Hii hainiudhi hata kidogo, maadam tu hawaingilii mambo yetu. Maadam tu matakwa ya nchi yetu yanatekelezwa. Lakini itakuwa hivyo?

Haitakuwa hivyo hata siku moja na ndiyo changamoto ambayo tunaipa sasa uongozi mpya wa *TRA*. Wenzetu jirani zetu, tunasoma Bajeti siku moja, Kenya na Uganda. Kenya ilikuwa tegemezi kama sisi katika Bajeti, lakini walinyimwa misaada na hawakutetereka, pamoja na ubadhirifu mdogo mdogo kama uliopo hapa kwetu, lakini makusanyo yao yaliweza kuendesha nchi yao kwa miaka miwili mfululizo. (*Makofii*)

Mimi siamini hata kidogo kwamba uchumi wa Kenya, ni mara nne ya ule uchumi wa Tanzania, kwa sababu makusanyo ya Kenya ni *trillion* nne shilingi za Tanzania, wameendesha nchi yao kwa shilingi *trillion* 4 kwa shilingi za Tanzania. *TRA* wakusanyaji wetu wanakusanya *trillion* 1.2. Akili ya kawaida ya elimu ya chini kabisa, kuangalia uchumi wa Tanzania, uchumi wa Kenya, uchumi wa Uganda, hauwezi kufikisha mahali pa kusema kwamba, uchumi wa Kenya ni mara nne kuliko uchumi wa Tanzania na Serikali mpya ya Kenya inasema, watafikisha makusanyo katika miaka michache ijayo mpaka shilingi *trillion* 6 za Tanzania.

Kwa hiyo, changamoto kwa *TRA* kwamba *trillion* 1.2 ni ndogo sana. Tunahitaji sasa shilingi bilioni 5 za ziada kwa ajili ya Serikali za Mitaa baada ya kodi zenyenye kero kuondolewa. Kwa mujibu wa Katiba sisi kama Serikali za Mitaa, baada ya zile kodi za kero kuondolewa na hizi shilingi bilioni 5 zitapatikana baada ya makusanyo kuongezwa na uchumi wetu unakaribia wa Kenya ambayo inaelekea kukusanya *trillion* 6. Kwa nini Tanzania isielekee kwenye *trillion* 4 kwa mwaka na hatutakuwa na haja kubwa sana ya fedha za wafadhili kwa kiasi hiki. (*Makofii*)

Kwanza, hii ni changamoto ambayo sisi wote tunawapa wenzetu hasa Uongozi mpya wa *TRA*. Sasa tunakuja hili suala la kodi za kero ambazo zimeondolewa na Serikali na kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu ambao ninawawakilisha. Namshukuru sana Waziri wa Fedha na wenzake, ambao walibuni jambo hili. Kwa hakika wanatekeleza masharti ya Katiba. Kwa sababu Katiba yetu inatambua wazi wazi kuwepo kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutekeleza masharti ya Uongozi wa Serikali kutoka juu mpaka chini.

Katiba hata sehemu moja haijaipa Serikali yeoyote ya Mitaa, majukumu ya kukusanya kodi. Ni Sheria tu ambayo tumeitunga baadaye. Katiba yenyeve iko wazi katika ibara ya 146(ii) kwamba bila kuathiri maelezo ya jumla yaliyomo katika ibara ndogo ya (i) ya ibara hii, chombo cha Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sheria iliyokianzisha, kitagusika na shughuli zifuatazo:-

Shughuli hizi ni shughuli pekee za Serikali za Mitaa. Moja, kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake. Pili, kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na ulinzi wa wananchi.

Tatu, kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kutumia demokrasia hiyo ili kuhakikisha maendeleo ya wananchi. Hakuna neno hata moja la kwamba wanawajibika kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba mkusanyaji wa kodi ni Serikali Kuu na baada ya kukusanya inagawanya kwa haki katika maeneo yote kwa kutumia utaratibu na mtiririko wa Serikali za Mitaa. Kwa kuondoa kodi hizo za kero kwa hesabu ndogo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mahesabu ya Serikali za Mitaa, kwa hesabu ndogo tutahitaji kati ya shilingi bilioni nne na shilingi bilioni tano kwa mwaka ili kufidia pengo litakalotokana na kuondolewa kwa kodi hizi. Kwa hiyo, bila shaka Mheshimiwa Waziri hili ataliweka maanani kwa sababu ni jukumu la Katiba na Serikali Kuu na kwa maana hii Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema Bajeti hii ni nzuri lakini kila kizuri pia kina matatizo yake. Mimi na wenzangu wengi tumeona dosari kubwa katika Kitabu cha Nne cha Maendeleo. Mikoa na Wizara kila kasma, kasma kubwa na kasma ndogo wote muangalie kile kitabu, hakuna uwazi, kuna mambo ya kufichwa, pengine inapingana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukurasa wa 28 mpaka ukurasa wa 31. Inapingana kabisa na kasma zilizopo kwa mfano katika Wizara ya Kilimo na Chakula ambayo tumeipa fedha nyingi sana, shilingi bilioni 31 hizi zinatumikaje?

Kwa mfano *Agricultural Program Support, allowances*, hii ni Bajeti ya Maendeleo unasema *allowances three hundred and thirty one million, Agricultural Institutes, allowances two hundred and twenty eight million, fedha za JICA wameleta, Intergrated Programmes First Phase Management, Employment allowances forty three million, Support for Agricultural Extension-Employment allowance two hundred and ten billion, Basic Salaries and Non Pensionable Post, eight nine million, Employment allowances, thirty fifty one million na hii peste control, unakwenda moja kwa moja ni allowances, ni office supplies, ni travel and substances allowances most seventy percent*. Sasa wote tunaweza kutafsiri hii maana yake ni nini, tunamfikishia mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda naomba niende haraka kidogo, kwa Wizara hii ya Fedha naomba nimalizie kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nilitoa mimi siku moja, kwamba nini wajibu wa Benki Kuu katika kusimamia na kudhibiti mienendo ya Benki za Biashara katika nchi hii, tuliwahi kuuliza hapa. Hadi leo Benki kadhaa zimeporomoka na wananchi wameathirika, Gavana wa Benki Kuu amewajibika namna gani?

Inakuwaje Wakurugenzi na wawekezaji wenyewe kampuni zao wanaanzisha chombo cha fedha au Benki halafu sifa zao sisi watu wa Vijijini tunazifahamu ni mbaya kwa nini Gavana wa Benki hajui? Pamoja na lile suala la *Delphis Bank* ambayo pia imeanguka, kwa nini hakufahamu kuwa sifa ya yule mwekezaji ni mbaya? Sheria inasema wazi kwamba kama Mkurugenzi wa Kampuni au Benki ana sifa mbaya tusikubali awekeze hasa kwenye eneo nyeti kama la Benki? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini Mabenki yanaporomo ka, hivi ni hatua gani inachukuliwa na ni nani anawajibika kwa matatizo ambayo wanayapata wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa upande wa kilimo, tunashukuru kila Wilaya itapata fedha kidogo. Lakini mimi bado nina wasiwasimkubwa juu ya sera ya kilimo na uendeshaji wa kilimo katika nchi yetu. Kweli wakulima wetu wengi ni wadogo, hawa wakulima wadogo inaonekana kama mchango wao ni mdogo na watu wanaupuuza. Lakini sehemu kubwa ya dunia inalishwa na wakulima wadogo. Nenda India, China, Philippines, Indonesia na kadhalika robo tatu ya dunia wanalishwa na wakulima wadogo na sisi pia tungeweza kulishwa na wakulima wadogo na pia tuwe na ziada. Hatuwakatai pia wakulima wakubwa, wakulima wakubwa nao wawekewe mpango na utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa ajili ya muda nilitaka kwenda kwa undani kabisa kuhusu Kitabu Na. 4 cha Maendeleo ambacho kwa maoni yangu fedha hizi zinatumia Ofisi za Serikali kama *Cash Office* ama Ofisi za Malipo tu siyo kwa ajili ya miradi.

Kwa hiyo, sura ya kile kitabu mimi ningependa ibadilike badala ya Ofisi za Wizara kuwa Ofisi za Malipo ya kawaida, iwe Ofisi za Malipo za Miradi inayoendelea, Miradi iliyokamilika na Miradi iliyoanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache kwa vile Bajeti yenye ni nzuri hii dosari mimi naamini inaweza ikarekebishwa. Kwa hiyo, naiunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubhi hii ya leo ili na mimi niweze kuchangia machache kwa hoja hizi mbili za Bajeti ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijafanya hivyo, basi niruhusu na mimi niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliopita katika uchaguzi mdogo, wote kwa ushindi wao na kuweza kuingia kwenye Bunge lako Tukufu. Napenda kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nichukue nafasi hii niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba na pia nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, kwa hotuba nzuri ile ya Bajeti na ile ya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa letu. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamechangia na karibu wote wamesifu na kuipongeza Bajeti hii. Mimi sitakuwa tofauti, nami naunga mkono kwamba hii ni Bajeti nzuri na nasema ya kwamba inawezekana ni Bajeti ya kwanza kwa miaka mingi kidogo sasa ambayo tayari inatuweka katika hali ya kusimama kwa miguu miwili ili tuweze kukimbia. Mimi napenda kuipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitachangia machache kama wenzangu walivyofanya. Lakini kwanza nianze kwa kusema kwamba pamoja na mambo mengi yalioelezwa katika Bajeti hizi mbili, Bajeti ya Serikali na Taarifa ya Uchumi, kwa kweli wananchi wa Watanzania na hasa sisi Waheshimiwa Wabunge tumezipokea kwa moyo mkunjufu na kwa kweli kwa kuona kwamba jitihada kubwa imefanyika ili itusaidie kupunguza umaskini wa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bajeti nzuri na hatua nzuri ambazo zimechukuliwa katika Bajeti hiyo na Taarifa ya Mipango, naomba kutoa rai kwamba pengine ni vema tubadili tabia. Ni vema tubadili tabia hasa katika upande ule wa nidhamu. Bajeti hii ni nzuri na tuna matumaini makubwa na matokeo ya Bajeti hii lakini kama hatutaitekeleza Bajeti hii kwa nidhamu ya hali ya juu, inawezekana matumaini ya Watanzania yasifike pale ambapo tunakusudia kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka nidhamu zaidi katika ukusanyaji wa mapato, tunataka nidhamu katika matumizi, tunataka nidhamu ofisini na viwandani, pia tunataka nidhamu mashambani katika mazao yote ya kilimo, chakula na biashara.

Naomba tufike mahala kila mtu awajibike sehemu yake, kama hatufanyi hilo, Bajeti hii nzuri inaweza ikaingia dosari kubwa sana wakati wa utekelezaji wa shughuli zake. Nidhamu ya matumizi na pia nidhamu ya mapato ni kitu muhimu sana katika mpango huo wote wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa kwa hatua zilizochukuliwa za kumsaidia Mtanzania mnyonge kupata nafuu ya maisha, maeneo ya kodi zilizoondolewa, leseni mbalimbali, maeneo ya ruzuku kwa mbolea na pia maeneo ya mifuko ya kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara, wafugaji na pia wavuvi yote ni hatua nzuri sana. Kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba wananchi wameishangilia sana hii Bajeti kwa kuondoa baadhi ya zile kero ambazo wenzangu wamezisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kero hizo imesemwa sana na mimi naomba niiseme, ni ile inayoitwa kodi ya maendeleo. Kule Wilayani kwetu Lushoto miaka michache ya nyuma tuliporuhusiwa kuamua tufanye nini, sisi tuliiionda kodi ya maendeleo kwa akina mama, kwa hiyo tukaendelea kuilipa sisi wanaume hadi juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipotamka kwa mba sasa kodi hiyo inaondolewa kabisa. Tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameshangilia sana kuondoka kwa kodi hii kwa sababu ya kero na matatizo makubwa ambayo walikuwa wanayapata. Mimi tangu nimepata nafasi hii ya kupewa uwakilishi wa Jimbo la Mlalo nimeishi Vijijini, Kijiji cha Lukozi, Kata ya Malindi, Tarafa ya Mlalo na Jimbo la Mlalo. Nimeshuhudia matatizo makubwa sana ya kero hii ya kodi ya maendeleo. Wananchi wameteswa, mahala pengine wamepigwa, wamepata ngeu mpaka damu zinatoka. Wananchi wamefungwa mashati msururu kama wezi, tatizo ni kero ya kodi ya maendeleo. Wananchi wamekimbia majumbani kwao wamekwenda msituni kwa sababu ya kero ya kodi ya maendeleo na pia wananchi wengine hata wamefungwa magerezani kwa sababu ya kero ya kodi ya maendeleo.

Kwa hiyo, kuondolewa kwa kodi hii pamoja na zile adha na bughudha nydinge zote wananchi wameipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwaondolewa adha kubwa hii ambayo miaka yote walikuwa hawana raha katika maisha yao. Tunaishukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu tatizo la chakula. Ni kweli kwamba hali ya chakula nchini siyo nzuri, mwaka huu maeneo mengi hata kule Wilayani kwetu yako maeneo ambayo yana matatizo makubwa ya chakula na kwa kweli hali ya mvua ya mwaka huu, mvua za vuli na pia mvua za masika hazikunyesha kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, lakini tuna maeneo ambayo kusema kweli yasingekuwa yanashubiri mvua.

Mimi naomba kwamba pamoja na Bajeti nzuri hii Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza jitihada zaidi katika upande wa kilimo cha umwagiliaji. Umaskini wa kukosa chakula ni umaskini wa hatari sana duniani na mimi sioni ni kwa namna gani Tanzania itaepuka kupokea amri kutoka Mataifa mengine ikiwa hatuwezi kabis a kujitegemea kwa chakula, hili ni jambo la ajabu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati yako, Kamati ya Kilimo, Ardhi na Maendeleo ya Maji na Mifugo. Tulipata nafasi ya kutembelea Mkoa wa Morogoro, tukatembelea Mashamba ya Miwa na Viwanda vya Sukari Kilombero pamoja na Mtibwa, tulipata bahati ya kujifunza na kuelewa Mkoa wa Morogoro uko namna gani. Jambo moja ambalo kwa kweli ni la kweli lakini pia linashangaza, ni kwamba Mkoa peke yake wa Morogoro unayo mito isiyokauka kwa mwaka mzima, mito 176. Katika hali ya namna hiyo ukiambiwa Tanzania tuna njaa na Morogoro kuna upungufu wa chakula kama ni mgeni wa nchi hii unaweza usiamini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naiomba Serikali pamoja sasa na kujali kuimarisha kilimo, nguvu zaidi zipelekwe upande ule wa umwagiliaji, maji ya bure yanakwenda baharini yanapotea bila kutumiwa, uwezo ambao hata Mkoa mmoja tu ungeweza kulisha Taifa nzima bila kuomba wala kutafuta chakula mahala pengine. Jambo hili tuisipojitahidi kulichangamkia itakuwa ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu. Naomba pia katika maeneo yale ya hatua za kuchangamkia kuimarisha kilimo basi utafiti pia utiliwe mkazo na matokeo ya tafiti mbalimbali za mazao ya kilimo uweze kuwafikia wakulima kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naona nilizungumze ni lile linalohusu nia ya Serikali na mpango wa Serikali wa kuanzisha Benki mpya ya kuwashudumia wakulima na wavuvi. Wazo hili ni nzuri kabisa ingawa mimi sikutazamia kwamba wazo hili lingekuja wakati huu kwa sababu inaelekeea Mabenki yetu yote tumekuwa tukiyauza, sasa nilidhani labda lilikuja kwa bahati mbaya. Lakini kama lilikuja kwa nia njema, mwenzangu mmoja jana aliogopa kusema, mimi nalisema lakini silisemi kwa malumbano nasema kama kawaida ya Waheshimiwa Wabunge katika kuishauri Serikali kwamba ichukue mkondo ambao utaendelea kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini. (*Makofî*)

Sasa kwa sababu nia ya Serikali ni kuanzisha Benki mpya, mimi nadhani kuanzisha Benki mpya kabisa ni gharama kubwa sana kuliko kutumia baadhi ya Benki tulizonazo zikafanya kazi ya kuweza kuhudumia kilimo. Hivi tuna tatizo gani na hii *NMB* ambayo tuna nia ya kuiuza?

Sasa kama wakati umefika tunataka tuanzishe Benki ya kuwashudumia wakulima na wavuvi kwa nini tusiigeuze hii, kwa nini tusiibadili hii, kwanza Benki yenyewe ina mtandao mkubwa nchi nzima halafu Benki yenyewe ina majengo na Maofisi ya kutosha, ina wataalam wengi, imeshaingiza sehemu nydinge teknolojia ya kisasa, hivi kwa nini Benki hii tuisiitumie, kwani tunapata amri kwa nani? Maana kama sisi

ndio tunaamua mimi kwa dhati kabisa naishauri Serikali sasa badala ya kuanzisha Benki mpya, Benki hii tuigeuze iwahudumie wakulima kama Serikali ilivyokusudia.

Lakini kwa sababu mpango huu upo na tunaukubali najua gharama ya kuigeuza Benki iliyopo itakuwa ni rahisi zaidi kuliko gharama ya kuanzisha Benki mpya. Sasa zile fedha zitakazobaki kwenye mpango huo basi tuzitumbukize kwenye kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuharakisha nia yetu ya kujitegemea katika kuondokana na umaskini wa ajabu wa kukosa chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ushauri wangu kwamba tutumbukize huko ili wananchi wawewe kumwagilia na ikiwezekana tuainishe mabonde yote nchini ambayo yanawezekana kumwagilia, kule Lunguza na pia kule Mnazi kwenye Jimbo langu, ni maeneo mazuri sana ambayo yanawezekana kumwagiliwa. Basi fedha hizi zikielekezwa huko tunaweza kabisa tukafuta tabia na hali hii ya umaskini uliokithiri wa kuomba omnia chakula, kwa nini tusidharauliwe kama hali hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba katika Kitabu cha Taarifa ya Hali ya Uchumi, Mheshimiwa Waziri alizungumzia sana kuhusu masuala ya ubinafsishaji pale na akasema kwamba karibu viwanda viliyyobinafsishwa asilimia 60 ni Watanzania, *well!* Sina sababu ya kukataa hilo. Lakini kwa sababu kauli za Serikali wakati mwininge zinagongana pengine ni vizuri sasa tufike wakati Waheshimiwa Wabunge wapewe orodha ya watu hawa walioziwa viwanda, hawa Watanzania ni akina nani? Maana haiwezekani kwa kweli tukaendelea kuwaacha wazalendo wa nchi yetu wakakaa pengine wakawa ni washangiliaji wa uchumi wa nchi yao, haiwezekani na matokeo yake ni kwamba miaka michache ijayo mambo yatakuwa mbaya kweli, wala tusije tukashangaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siamini kusikia baadhi ya kauli za viongozi wetu kwamba Mtanzania anayetaka kununua kiwanda au shamba ashindane na wale wengine wanaotaka ili akishinda apewe. Mimi nina wasiwasi mkubwa kwa sababu jamani ni juzi tu, hivi ni Watanzania wangapi hasa wazalendo wanaoweza kushindana na watu waliozoea shughuli za ubepari miaka chungu nzima, ni akina nani, tumesahau kauli ya Hayati Mwalimu Julius Nyerere ya juzi tu, tumesahau Mwalimu kaondoka juzi, amesema: "Hivi kweli tuna kijana wetu anaitwa Mbwana Matumla, hivi kweli anaweza kuingia ulingo mmoja akapigana ngumi na Michael Tyson, hivi kweli inauezekana"?

Sasa kama hatutakuwa na makusudi ya kuwapendelea Watanzania wazalendo ili waingie kwenye mfumo wa uchumi wa nchi yao, tutakuwa tumeikosea haki sana nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni malalamiko na manung'uniko ambayo nimeyasikia sikia kwenye Miji yetu na hasa Mji wa Dar es Salaam. Inaelekea Miji yetu imevamiwa na vijana wengi wageni, lakini hata kwenye vi-hotel hoteli unakuta watu wanafanya kazi za kawaida kabisa ambazo Watanzania wangeweza kuzifanya, kwenye *ma-garage* na pia kwenye vioski kule, hivi tuna utaratibu gani wa kuweza kuzuia haki ya Mtanzania wa kawaida kufanya kazi zile anazoziveza, hivi wenzetu wanakwenda hivi kweli?

Kwa hiyo, mimi hata ile hali ya kuzuka kwa ujambazi siishangai maana yake inaelekea tumefika mahali tumelala, vijana wamejaa kila mahala, hawa wanatoka nchi za jirani, wengine wanatoka nje na wengine wanatoka Asia, kazi ambazo kila Mtanzania angeweza kuzifanya. Mimi naomba tuwalinde watu wetu ili wawewe kupewa zile kazi ambazo ni za kawaida kabisa na uwezo wa kuzifanya wanao. (*Makofi*)

Nami napenda niungane na wenzangu kwamba pengine Serikali yetu iangalie upya jitihada za kueneza umeme Vijijini. Haipendezi tukizungumzia maendeleo, maendeleo ni pamoja na umeme, simu, barabara na pia maji. Sasa inaonekana tangu wamewapata hawa watawala wapya mambo ni kama yamesimama, Serikali imesema inachukua jukumu la kupeleka umeme Vijijini lakini tunaona kama vile hakuna hatua zinazochukuliwa, hivi tuseme nini? Tunaomba majibu kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme wa Jimbo langu la Mlalo ulikuwa haujakkamilika, kuna Vijiji vinne viliachwa kwenye mradi ule, nimepiga kelele, nimesema lakini majibu ya kutosha sijayapatna, naomba nipate sasa, Kijiji cha Mlesa, Zaizo, Dule, Ngazi na Mhelo vilikuwa kwenye mradi ule toka mwanzo lakini vimeenguliwa, tafadhali naomba majibu. Nashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ya mimi kuweza kuchangia katika hoja mbili zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi, wapiga kura wa Jimbo langu la Babati Magharibi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba nzuri ambayo waliitoa hivi karibuni. Nashukuru kwamba nimepata nafasi hii ya kuchangia na kuleta baadhi ya maombi yao kama mwakilishi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imesifiwa sana, hoja zote mbili na mara tu ilipowasilishwa tulipata simu kutoka kila kona ya nchi yetu na hususan katika Jimbo langu kwamba nifikishe salamu za pongezi kwa Serikali ambayo imejionyesha kweli kwamba ni Serikali sikivu, Serikali ya CCM. Hakika ni Bajeti ambayo imelenga katika kupunguza lakini hatimaye kuondoa kabisa umaskini katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa mafanikio makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu, uchumi kwa ujumla. Tumelezwa kwamba uchumi jumla umekua kwa asilimia 6.2, tena zaidi ya matarajio ambayo yalikuwa yamewekwa ambayo ilikuwa ni asilimia 5.9. Kwa hiyo, ndiyo msingi huu ambao unatuwezesha sasa kuelekea kwenye uchumi, wanasesma katika *Micro-level*; na Serikali yetu imejionyesha kabisa kwamba imejielekeza kule kwa jinsi Bajeti hii ilivyowasilishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza kabisa liliodhihirika kwa wananchi bila kuingilia ndani falsafa ya uchumi, ni suala hili linalowagusa wao kwa karibu zaidi na kwa urahisi, ni suala la mfumo mzima wa kodi. Kwa kuanzia Serikali imefuta kodi ya kichwa, kwa kweli hilo tunaipongeza Serikali kwa nguvu zote na wananchi wamefurahia na kuipokea hatua hii ya Serikali, katika hilo tunaipongeza Serikali. Masuala ya uchumi na falsafa ya uchumi kwa ujumla nitawaachia waliobobeaa katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa niende kwenye maeneo ambayo nilikuwa nimekusudia kutoa mchango wangu katika kuboresha hotuba hii ya Bajeti na Mipango ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha ambao tunauanza mwezi Julai. Kama ilivyokwishatajwa au tuseme Bajeti yenyewe inavyojielekeza, suala zima ni kuondoa umaskini na kuenenda katika dira ya kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025 na maeneo kadhaa yameainishwa na Serikali yetu kwa njia ya Bajeti hiyo ambayo ni miundombinu ya barabara, barabara Vijijini, kilimo, afya, elimu, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kuipongeza Serikali nikianzia na kilimo kwamba imejielekeza katika kuboresha kilimo ambacho kwa miaka mingi iliyopita na itakayokuja ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye aya ya 34 Mheshimiwa mtoa hoja ametuelezea mkakati wa kuinua kilimo kwamba unazingatia mambo kadha wa kadha na yameorodheshwa kadri ya mambo 11, sina haja ya kuyataja moja baada ya lingine.

Lakini napenda niseme kwamba ingekuwa ni vizuri kama kweli tunakusudia kuwa na kilimo ambacho ni endelevu, tuongezee na kipengele cha uchimbaji mpya wa mabwawa, malambo na ukarabati kwa yale ya zamani ambayo yanahitaji kukarabatiwa au kupanuliwa, hivyo tunaweza kuzungumzia habari ya kilimo endelevu na pia kilimo cha umwagiliaji, vinginevyo tumeendelea kurudia suala hili la upatikanaji wa maji katika nchi yetu lakini sijaona kwa kweli suala zima la upatikanaji wa maji kwa njia ya mabwawa au malambo kwamba limetiliwa maanani.

Mimi naamini Serikali ingeweza kutenga hela nyingi zaidi katika eneo hilo ili maji ambayo kwa kweli ni tegemeo kubwa kwa kila kiumbe achilia mbali kilimo, kwa kweli yangepaswa kupewa kipaumbele cha kwanza kabisa kama ambavyo sasa hivi tumeanza kuweka kipaumbele katika barabara. Kwa hiyo, nisisitize kwa Serikali na kuishauri kwamba tuweze kujielekeza hapo kwenye kuchimba mabwawa

makubwa kwenye mabonde na kwenye mito ili kuweza kui-intercept maji ambayo yanatiririka kwenye maziwa na bahari bila matumizi yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusemea kidogo habari ya kilimo na upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo nijielekeze kwenye eneo la barabara. Katika kuzungumzia kuondoa umaskini katika nchi yetu kila mzungumzaji humu ndani amegusia barabara na katika vitabu vyetu mbalimbali vya Bajeti tumezungumzia barabara lakini nimeona barabara zinazozungumzwa zaidi ni hizi barabara kuu, *trunk roads, regional roads* ambazo ziko katika mamlaka ya Wizara ya Ujenzi, lakini vile vile kuna barabara za Wilaya, lakini pia kuna barabara za Vijijini.

Sasa barabara za Vijijini kama tunavyodai kwamba ni eneo la kuondoa umaskini na ndiyo kipaumbele cha kwanza katika maeneo ambayo Serikali imeweka kama kipaumbele, mimi nimeona bado hapo hapajafikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipendekeze tu kwa Serikali kwamba ili kuweza kufikia barabara zile za Vijijini, *access roads* zile na mwananchi akaguswa na jitihada hizo, kufanyike au kuchukuliwe hatua za dharura kabisa za awali ili kumfikia huyo mwananchi au maskini kwa njia ya kuzitengeneza hizo barabara, barabara za udongo maana yake nazo ni barabara, tunaposema barabara siyo lazima ujenge barabara za changarawe ambazo wengine kitaalam wanaita *engineered gravel roads* lakini bado unawenza kuwa na barabara za udongo nzuri tu zinazopitika kwa mwaka mzima ili ukamfikie mwananchi wa Kijijini.

Lakini sasa hivi inavyoonyesha tunapozungumza habari ya kujenga barabara katika nchi hii tunafikiria barabara za lami au changarawe lakini kuna barabara hizo za udongo ambazo sasa hivi zimeachwa na zipo vijijini katika maeneo tunayoishi sisi au wananchi walio wengi. Kwa hiyo, mkakati wa kwanza ambapo wananchi wanaweza kuona *effect* au *impact* yake ni kufanyike kazi ya *grading*; najua wengi hapa hawatakubaliana nami katika suala la *grading* watasema ni kuweka vumbi tu barabarani lakini *uki-grade* barabara ni mojawapo ya *maintenance means* katika barabara hizo ukawa na *shape* ya barabara mpaka vijijini. Mwaka unaofuata ukashughulikia habari ya *drainage* au mifereji, makalvati, madaraja na mwaka unaofuata sasa uendelee na hatua hizo zingine za kuweka changarawe; wakati huo lakini barabara hizo zimeshatumika na zinaendelea kutumika siku hadi siku. *Maintenance* ya barabara ni *on going process* huwezi kusema leo umetengeneza barabara ukasema kazi hiyo imeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine katika Wilaya zetu ni *capacity* ndogo katika ku-maintain barabara hizi. Naomba hapo paangaliwe ili kuwe na *capacity* ya kutosha kwa maana ya *procurement*, kwa maana ya kusimamia utendaji wa kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa upande wa usalama. Niipongeza Serikali kwa kuipa eneo hili fedha nydingi zaidi juu ya fedha ambazo mwaka jana tuliwapa. Hivi sasa imefikia bilioni sabini (70) kutoka bilioni hamsini na tano (55) za mwaka jana. Naomba fedha hizo basi kwa kweli ziweze kuonyesha matokeo yake.

Hivi sasa hali ya nchi yetu kuhusiana na usalama ni mbaya sana raia wengi wafanyabiashara, wafanyakazi wamepoteza maisha yao kutokana na ujambazi. Hivi sasa tumeona Polisi wameanza kuzinduka lakini ni baada ya wenzao kuuawa. Sasa hii inaleta picha ambayo sio nzuri kwamba kumbe kwa wengine waliokuwa wanauawa ilikuwa kama ni kitu cha kawaida. Nafikiri suala hili lisiwe linafanyika kama *operation* kwa sababu ya kupambana na hawa wageni ambao wametuingilia hivi sasa lakini liwe ni suala la kudumu, isiwe tena ile watu wanaita ni nguvu ya soda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa elimu. Naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mfuko wa kuwasaidia wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwasomesha Elimu ya Sekondari. Lakini katika Wilaya zetu mara nydingine jambo hili halijaeleweka bado Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari wanawauudisha watoto nyumbani eti kwa sababu wameshindwa kulipia karo. Nafikiri suala hili lizingatiwe kwa makini katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa pensheni. Kwa kweli eneo hili ni mojawapo ya maeneo ambayo wastaafu wamelipokea kwa shukrani kubwa sana kwamba sasa kiwango cha chini kimepanda hadi Sh.20,000. Lakini kwa wale ambao tumewasiliana wanaomba kipindi hiki cha miezi sita ya kusubiri - hizo Sh. 20,000 itakuwa sasa mara sita; ndio wapokee hizo fedha - angalau basi iwe kila miezi mitatu sasa.

Hivi sasa mstaafu anaweza kufunga safari kufuata Sh.60,000 Wilayani au Benki. Lakini kusubiri kwa miezi sita imeonekana haina tena mantiki kwa sasa sababu mwanzoni pesa ilikuwa ndogo mno, ndio maana ikawa *accumulated* kwa miezi sita *li* iweze kuwa *at least substantial amount* ya kumwezesha yeye kusafiri na kuzifuata Wilayani; sasa hivi hiyo mantiki haipo tena. Kwa hiyo, naomba hiyo irekebishwe iwe miezi mitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie juu ya simu. Kwa kweli simu ni eneo ambalo kiuchumi ni nyeti kabisa lakini kupandisha gharama za simu inafanya *expansion* ya simu hizo kufika vijijini kuwa tatizo kubwa kwa sababu hakuna atakayekuwa ana-*afford* gharama za hiyo simu. Kwa hiyo ile dhana ya Serikali kwamba simu zifike mpaka vijijini inakuwa defeated. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri niwasilishe hayo machache katika nia ya kuboresha hoja hizi mbili zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naipongeza Serikali na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kuitaka Serikali kujizatiti katika nidhamu ya kazi ili bajeti hiyo iwe na maana kabisa ambayo kwayo tuko hapa kuipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii. Kwanza niwapongeze Wabunge wapya walioingia katika Bunge hili na hasa Wabunge wa CCM. Tunawakaribisha tufanye kazi pamoja. Pia nawapongeza Wapinzani ambao wameingia katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inapongezwa na kila aliyechangia na Watanzania wote kwa kweli wamefurahia sana jinsi bajeti hii ilivyowasilishwa kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na wafanyakazi wote katika Wizara hiyo tunawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuandaa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii kimsingi inatekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2000 na jinsi iliviotengenezwa inazingatia kilio cha Watanzania cha muda mrefu kuhusu tatizo la msingi ambalo ni umaskini na kuondokana na kero mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwasibu. Bajeti imewalenga sana hawa maskini na imewaondolea matatizo waliokuwa nayo ili waweze kupata nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya Watanzania wamejikita katika kilimo na kilimo hiki kwa bahati mbaya ni kilimo duni wanatumia zana zisizokuwa bora, mbegu zisizokuwa bora na hivyo mapato yao yamekuwa duni. Lakini bajeti hii sasa inaanza kutoa mwanga ili wakulima wa Tanzania hawa wadogo wadogo waanze kujinunulia zana zilizo bora, mbegu bora halafu watumie mbolea na madawa kwa ajili ya mimea yao na madawa kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa katika bajeti hii ni kuhusu fidia ya bei ya mbolea ambayo imetolewa kwa Mikoa minne Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Sisi Wabunge wa Mikoa hii minne tunatoa ahadi kwa Serikali kwamba tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuzalisha zaidi na wala wananchi wetu hawahitaji kuhimizwa kwa sababu miaka yote ni wakulima wazuri na wamekuwa wakizalisha. Kwa kweli tunapongeza sana juhudhi za Serikali. Lakini isiwe tu ni kwa mwaka huu jambo hili liwe endelevu kwa sababu nchi zilizoendelea kama Marekani, Ufaransa, Ujeruman, Uingereza utoaji wa ruzuku kwa wakulima wao ni kitu cha kawaida ndio maana wanashindana vizuri lakini sisi tumekuwa hatupati hii ruzuku na ndio maana tumekuwa na matatizo. Hili tunalipongeza na wakulima katika Mikoa hii wanatoa pongeza kwa Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinachotegemea hali ya hewa siku zote sio kilimo cha kuaminika. Hivyo sasa tunapozungumzia jinsi ya kuwasaidia wakulima wapate zana bora, mbege bora kuna umuhimu wa kuanza kufikiria ni jinsi gani ya kuwapatia wakulima hawa uwezo wa kutumia umwagiliaji maji katika mashamba ili waweze kupata mazao mwaka mzima, hili litasaidia kuondokana na njaa katika nchi hii. Hebu tujifunze kwa Afrika Kusini na Zimbabwe huko nyuma ambapo ukiruka kwa ndege katika nchi ya Afrika Kusini ukiangalia chini utaona maeneo kuna mabwawa yameziba Mito kwa ajili ya umwagiliaji maji na nchi hii haina matatizo ya chakula hata siku moja lakini sisi nadhani ndio tunazinduka katika usingizi huu.

Nadhani sasa Serikali inalionna hili na ifanye kazi kubwa ili ihakikishe kwamba kilimo kinaendelezwa kwa msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wakulima wadogo kupatiwa mikopo ya kununua zana bora, mbege na madawa, suala hili la kuanzisha Benki, nina hakika kuanzisha Benki ni pesa nyingi sana. Hatuna sababu ya kuanzisha Benki tunajua Benki ya toka mwanzo walisema ni Benki ya makabwela Benki hii sasa ipewe uwezo kiwepo tu Kitengo ambacho kitashughulikia moja kwa moja mikopo ya wakulima, mikopo ya wavuvi, mikopo ya wafugaji lakini kufikiria kuanzisha Benki nyingine ni kuiongezea Serikali mzigo na pesa hizo badala ya kwenda kwa wakulima zitakuwa zinakwenda kuanzisha Benki. Suala hili nadhani limeeleweka ni ushauri tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa miundo mbinu. Suala hili la miundo mbinu ni kitu cha msingi sana katika maendeleo ya nchi hii. Barabara zimetiliwa mkazo na tunatenga pesa za kutosha lakini siku zote huwa najiuliza hivi hii miundo mbinu ya reli *TRC* pamoja na *TAZARA* ni mali ya nani na tunaposema tubinafsishreli tunasema hapana hatubinafsishi tunakodisha miundo mbinu lakini miundo mbinu hii ambayo haipati msaada, haipati fedha kutoka Serikalini ili iweze kuendelezwa iwe ya kisasa hata wakodishaji wanapiga chenga. Halafu mbaya *TAZARA* tulipata kwa mkopo kutoka nchi ya Uchina lakini inasemekana hatujalipa hata senti tano ya mkopo. Serikali inasema nini kuhusu muundo mbinu huu na unasaadia sana katika uchumi wa nchi hii? Ipo haja ya Serikali kuangalia jinsi ya kuweza kuhimiza fedha zitengwe ziende kujenga reli kisasa na kupeleka zana ambazo zitaboresha *TRC* na *TAZARA* ili ziweze kuihudumia nchi hii. Tuna mizigo mingi kutoka *DRC* haichukuliwi kwa sababu tuna reli mbovu ambayo haiwezi kubeba mizigo hiyo. Tunaomba sana kuhusu suala hili Serikali sasa ianze kuangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ikiwa ni pamoja na *Fuel Levy*. Suala la *Fuel Levy* kweli tumejitahidi sana kwenye suala la barabara sasa barabara zinajengwa hatuna ugomvi lakini na hawa *TRC* ambao ni *competitors* katika suala la uchukuzi wapewe kiasi fulani ili kuendeleza miundo mbinu ile, reli ziendelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mazingira. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia mambo mengi sana kupunguza kodi na kupunguza kero za wananchi. Lakini suala la umeme ni tatizo. Umeme kuwa ghali wananchi wengi wanakimbia kuutumia hasa kama nishati ya kupikia na kwa sababu hiyo miti inaendelea kuteketea kwa sababu ya matumizi ya mkaa na kuni. Tukipunguza bei ya umeme nina uhakika kabisa tutanusuru misitu yetu. Tuhakikishe kwamba tunapozungumzia bei ya umeme tunataka tunusuru misitu ili mazingira yetu yasiweze kuharibiwa zaidi lakini tunapokaa kimya kuhusu suala hili la bei ya umeme kwa kweli hatutendi haki kwa mazingira yetu mazingira yetu yataendelea kuharibiwa, tutafute njia ya kuweza kupunguza bei ya umeme, mafuta ya taa na gesi. Hii ndio itakayotusaidia kulinda mazingira yetu na tutayanusuru mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pensheni kwa kweli naipongeza Serikali jinsi ilivyoangalia suala hili na huu usiwe mwanzo na mwisho tuendelee kuboresha kwa sababu na sisi Wabunge wengine tuliomo humu ni wastaaifu watarajiwa ambao tutaendelea kutumia huduma hii. Sasa tusijizibie riziki kwa sababu na sisi tukija kustaaifu watu watakaokuwepo madarakani wakati huo wakasema aah wacha wakati wao umepita nadhani na sisi tutaendelea kupata maumivu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie jinsi ya kuwalipa hawa wastaaifu katika muda wake na kwa sababu wengine wamestaifu wakiwa na umri mdogo bado wana majukumu ya kusomesha watoto wao na hata wajukuu fedha zinazotolewa wakati mwingine zinatolewa wakati ambapo watoto wao

wanakuwa wameshafukuzwa shule na nini. Mpangilio uwe mzuri ili waweze kulipa hasa mfano mwezi wa Januari ambapo tunapeleka watoto wetu mashulenii fedha hizi ziwe zimepatikana ili ziweze kuwasaidia kulipia karo za watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, kazi iliyofanywa na Serikali kwa kipindi hiki cha miaka miwili, mpango wa MEM na mipango mingine kwa kweli tunaipongeza sana Serikali. Lakini nina ushauri mmoja. Ukijaribu kufanya utafiti kuhusu suala hili la watoto kuanza na umri wa miaka saba na kumaliza akiwa na umri wa miaka 13 na 14 wanakuwa bado ni wadogo sana. Naomba Serikali ianzé kufikiria jinsi ya kuweza kuongeza Elimu ya Msingi ianzé darasa la kwanza hadi darasa la kumi halafu darasa la kumi na moja mpaka *form six* iwe ni Sekondari.

Hii itawaongeza muda watu kukaa shulenii na kuweza kuijandaa kwa ajili ya kujitegemea kuliko ilivyo hivi sasa mtu anatoka darasa la saba kwa kweli ni mtu ambaye hawezu kujitegemea kabisa kwa sababu umri bado ni mdogo na uwezo wa kuweza kufikiria na kufanya mambo yake binafsi bado atakuwa tegemezi kwa wazazi wake kwa miaka mingine mitatu au minne tunakuwa hatujawasaidia wangebaki shulenii wangeweza kufanya mambo mengine mazuri ili waweze kuijandaa kuwa watu wazima hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya watoto yatima na watoto wa wazazi maskini ambao hawawezi kuwapeleka watoto wao shule. Hili ni jambo la msingi ambalo Watanzania wote tunafurahia na tunaipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Watendaji Vijijini kupata mishahara yao ni jambo ambalo limekuwa kero kwa muda mrefu na Wabunge tumekuwa tukilisema hili. Tunaishukuru Serikali kwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuiunga mkono hoja hii na nina hakika hata Waheshimiwa Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani wameliona wazi wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango kuhusu mipango iliyopangwa kwa Mikoa hii minne Rukwa, Singida, Kigoma na Shinyanga mipango yake iko namna gani kwa sababu mwaka jana nilizungumzia suala la kupanga mipango ya kimakengeza kutojali Mikoa hii suala hili limerudia. Sasa sijui ananipa maelezo yapi kwa shilingi milioni 318 kwa Mkoo wa Rukwa, milioni 337 kwa Mkoo wa Singida, milioni 372 kwa Mkoo wa Kigoma na milioni 527 kwa Mkoo wa Shinyanga hivi ndivyo umeweza kujitahidi kubadilisha hali katika Mikoa hii kama ulivyozungumza mwaka jana? Naomba unipe maelezo utakapokuwa una-*wind up* katika suala hili otherwise naiunga mkono hoja hii, naitakia Serikali mafanikio. (*Makofi*)

MHE. ISAAC M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge walioingia katika Bunge hili kutokana na chaguzi ndogo ndogo. Mambo ya kusema hasa nani, hilo ni tatizo lingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bajeti hapa labda nianzie alipoishia Mwananzila kwamba mwaka jana nilisema Mkoo wa Shinyanga umepewa milioni 300 constantly kwa miaka mitatu, Rukwa, Kigoma na Tabora. Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la mwaka jana alisema mwaka huu haitatokea hiyo atafanya mabadiliko aweze kuongeza kidogo ile bajeti. Kwa sababu suala la msingi lilikuwa ni kwamba Mikoa mingine yote ile ambayo inaonekana inapewa pesa nyingi ni kwa sababu kuna wafadhili na sisi tukasema kama ni suala la wafadhili tu na sisi tuonyesheni hilo duka la kununua wafadhili na sisi tununue tuwapeleke Shinyanga, Kigoma na Rukwa ili walingane katika bajeti na hiyo Mikoa mingine. Lakini mwaka huu tumebak pale pale Shinyanga tumepokea sijui milioni 300, Rukwa na wenywewe wako hapo hapo. Singida na wenywewe hapo hapo na Kigoma pale pale. Sijui kama ndio mgawanyo wa pato la Taifa unakwenda hivyo basi natumaini sisi watu wa Shinyanga, Tabora, Kigoma na Rukwa labda tukae chini tuulizane jamani kuna nini kule kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii, nashukuru Mheshimiwa Waziri ametenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya njaa. Nchi haiwezi kutawalika kama kuna njaa. Mwaka huu Mikoa mingi hali ya hewa haikuwa nzuri. Watu wanahangaika nimesoma kwenye magazeti Ndugu zangu Wazaramo

wanakula mizizi na kule Shinyanga *we are not safe* tuna hali ya njaa. Mheshimiwa Waziri tukishapitisha bajeti yako Ijumaa hebu toa hiyo pesa iende kununua chakula wananchi wapelekewe kule wale kwanza ndio tuenze kuzungumza mambo ya bajeti na kuwekana sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana na mwaka huu Mheshimiwa Waziri amesema bajeti haikufikiwa, mwaka juzi Mheshimiwa Yona ukurasa wa 13 amesema haikufikiwa na sababu zilizotolewa za kutofikiwa bajeti zimeelezwa kwamba kuna wakwepaji wa kodi. Mimi najiuliza kama unajua maeneo yote ya ukwepaji wa kodi *definitely* unawafahamu na wale waliokwepa hiyo kodi kwa nini tusitafute njia ya *ku-arrest* hiyo *situation?* Tuwataje hapa fulani amekwepa kodi kiasi fulani na fulani amekwepa kodi kiasi fulani *then* hatua zilizochukuliwa ni hizi hapa lakini kila mwaka Serikali inasema kuna mianya ya ukwepaji kodi katika mafuta, sukari, *jute bags* na vitu vingine lakini haijasema ni nani kakwepa na ni kiasi gani ndio maana tukapoteza ile pesa ambayo *may be* ingeweza kutufikisha pale ambapo tulikuwa tumepanga tufkie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa minne iliyotajwa kwamba watasaidiwa pembejeo Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa nasema hongera kwa kuwapa huo msaada wa pembejeo. Lakini kilimo hiki cha kutegemea kudra ya Mwenyezi Mungu ashushe mvua hata ukiwapa pembejeo zote wanazohitaji haitasaidia lazima kuwe na mabadiliko katika sekta ya kilimo ni namna gani tutokane na hili la kutegemea Mwenyezi Mungu ashushe mvua. Tuweke mkakati kabisa kwamba sasa kule tutatengeneza *big dams* na *scheme* nzima ya kumwagilia mashamba ili tuweze kuondokana na tatizo hili lakini hii ya kuwapelekea mbolea sijui na kitu gani lakini bado tunanyoosha mikono kwa Mwenyezi Mungu ashushe mvua akikataa matokeo yake ndio hayo ambayo tumeyapata mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hapa la uftaji wa kodi, tunaweza kupongezana sana kwa kufuta kodi, mimi nataka wote tupongezana, sisi tulitoa hoja mapema kabisa, tukasema kuna kodi ya kipuuzi ni Kodi ya Kichwa mkaja juu mkaguna kama mlivyoguna jana. Lakini tunachosema ni hivi, sisi tulitoa wazo tunawapeni hongera sana kwa kufuta kodi hiyo na tunataka sasa ufute kodi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi nyingi za kipuuzi mpende msipende na tutaendelea kuwaambia wananchi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndio inahusika na hayo moja ni Kodi ya Ng'ombe. Ng'ombe wanatozwa kodi ya Sh.400 na Halmashauri zote lakini ukiangalia ile Sh.400 anayetozwa ng'ombe huyu mtu unayemtoza hana uwezo wa aina yoyote hiyo ndiyo benki yake, hiyo ndiyo raslimali yake, Serikali kwa njia yoyote ile haimhudumii yule ng'ombe. Ninachosema ni kwamba ng'ombe asitozwe kodi na sababu yenye kwa ukiangalia katika Halmashauri zote Kodi ya Maendeleo uliyoifuta wala haikuwa inawasaidia sana kwa sababu Halmashauri zote ukisoma tangu Halmashauri ya Nkasi anayesema uza na kuchuna ngozi za watu, bado pato lao ni dogo sana kama ukilitoa halitakuwa na athari yejote katika maendeleo yao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zote za Wilaya uwezo wao wa kutojitegemea ni kati 95% na 87% hata bila kodi. Kwa hiyo, uwezo wao wa kujitegemea kwa sasa ni kati ya asilimia tano na asilimia kumi na tatu kuanzia Halmashauri ya Bagamoyo, Halmashauri yangu bado uwezo wetu wa kujitegemea ni 13%. Kwa hiyo, kama ni 13% tu ya uwezo wa kujitegemea kwa nini uwe na hizi kodi zote ambazo zina usumbuwa wa kuzikusanya kwa watu kwa nini zisifutwe. Naomba Kodi hii ya Ng'ombe ingeondoka kabisa katika Halmashauri na after all umewapunguzia *payroll expense* yao, kwa sababu *VEO* na *WE0* watalipwa na Serikali Kuu *then* watabakiwa na hela za kufanya nini sasa? Hii Kodi ya Ng'ombe ingeondoka ili tuweze kuwarahisishia watu wetu kule kijijini maisha ambayo wanaweza kuishi na ng'ombe wao kama raslimali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine ambalo limezungumzwa hapa la kufuta usafirishaji wa *Tanzanite* bila kukatwa. *Tanzanate* ni sehemu ndogo sana ya pato inayoingiza katika nchi. Nafikiria kwamba sasa hivi ndio wakati ambao ungetufaa zaidi kupiga marufuku usafirishaji nje wa madini yoyote yale katika hali ghafi hata dhahabu. Badala ya kwenda kuichemsha Japan kule yanapelekwa makontena ya dhahabu kwenda kusafishwa tujenge kiwanda cha aina hiyo hiyo hapa hapa. Lakini sio hilo tu dhahabu isafishwe hapa na tu-*improve* viwanda vyta Masonara ili waweze kutengeneza kitu ambacho sio ghafi tena na kukiuzi katika bei ambayo ni kubwa zaidi kuliko hali iliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo nilikuwa nayo kwa leo, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. FATMA S. ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika muda huu. Kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Wabunge wapya wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Sumri, Mheshimiwa Karamagi, Mheshimiwa Ndeka na Mheshimiwa Kiwanga. Lakini pia napenda kuwapongeza Wabunge wapya wa *CUF* kwa sababu kule Mlandege ndio kwenye Makao Makuu yao na pale Mtendeni tutaonana kwa hiyo nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mramba, Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Kigoda, Waziri wa Mipango kwa hotuba zao nzuri ambazo nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wanaosimama hapa wanaunga mkono hoja hii. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa sababu kubwa kwamba wametuambia uchumi umeongezeka kutoka asilimia 4 mpaka asilimia 5.6.

Haya ni mafanikio makubwa katika nchi hii ya Tanzania kwa sababu miaka yote tunaambiya Tanzania maskini imeshika mkia. Sasa tunaposikia uchumi umepanda angalau kidogo na sis i tunafurahi kuwa kama nchi za zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Mlandege napenda na mimi kusema kwamba tunaipongeza Serikali kwa hoja zote hizi na pia tumaiunga mkono Serikali kwa kuweza kuunda Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano. (*Makofî*)

Sisi Wazanzibar katika hotuba yote na mazuri yote lakini hilo ndio namba moja na limetugusa sana kwa sababu ukiangalia karibu miaka arobaini ya Muungano huu na hii ilikuwemo kwenye Katiba kwamba lazima iwepo Tume ya Pamoja na katika kipindi chote hiki tulikuwa hatuioni. Kwa hiyo, sisi Wazanzibar tumeifurahia sana hii Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano. Tunashukuru sana na napenda nimpongeze Mheshimiwa Shellukindo kwa kuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Muungano zipo nyingi, za kisiasa tumezungumza hapa na mwisho wake tumepata muafaka sote kule Zanzibar baina ya *CUF* na CCM. Kwa hiyo, kwenye siasa hatua imepigwa na sasa hivi watu waliokuwa hawaendi mazikoni, wanakwenda, madukani wanakwenda na tunashirikiana kwa mambo mengi kwa kweli. Mimi katika Jimbo langu ndiyo naiona hii kwa sababu ndiyo tupo Makao Makuu yao Wapinzani na Wilaya yao ya Mjini ipo kwangu. Kwa hiyo, naelewa nini mahusiano baina ya *CUF* na CCM. Kwa sababu hata jamaa zangu amba walikuwa *CUF* walikuwa hata kwangu hawaji. Lakini sasa nawashukuru sana wote tunashirikiana na tunatembeleana. (*Makofî*)

Lakini sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Tume ya Pamoja isaidie kusukuma uchumi na kuondoa kero za Muungano za uchumi katika mambo ya fedha na misaada inayokuja nchini. Kamati itafanya kazi yake lakini angalau wajue tutawauliza Zanzibar tunapata asilimia ngapi. Misaada hii, Zanzibar tunapata ngapi, miradi iliypopo sasa hivi Tanzania, ipi ya Muungano. Sasa tunataka kwenda katika mambo ya kiuchumi ambayo yatasaidia nchi zetu zote mbili, ule udugu wetu maana sasa ni miaka arobaini kama ni watu wangkuwa na wajukuu, lakini ule udugu ambaa umekwishafanywa na wazee wetu marehemu Mwalimu Nyerere na marehemu Karume. Tunaomba Kamati ya Tume itakapokaa itasaidia kutatua matatizo yetu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni Muungano wa Forodha (*Customs Union*). Mimi napongeza sana kwa Afrika Mashariki mwezi Novemba, wataweka Mkataba na tutakuwa na Muungano wa Forodha. Mimi hapa namshukuru Rais kwa kuwateua hawa watu wa *TRA* Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga ambaa watasaidia kusimamia Muungano huu wa Forodha ambaa utaandaliwa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Ndugu Lauwo na wenzake kwa kuweza kusaidia katika kukusanya mapato Zanzibar isipokuwa mimi nina tatizo moja. Maandalizi yetu yakoje? Kama tunaingia huu Umoja wa Afrika Mashariki ambaa Novemba tunasaini? Maana wenzetu wameshajiandaa, kila siku nauliza swalii hili, wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar mpaka leo wanapofika bandarini Dar es Salaam bado wanapata matatizo kwa nini na sheria zote zipo? Wakibeba mizigo yao wanalipa

Zanzibar *TRA*, halafu inabidi walipe tena *TRA Dar es Salaam*, hili suala tungelipenda ndugu zangu wa *TRA* mlitazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wafanyabiashara wadogo wanavunjika moyo na hasa kama nilivyosema Mlandege ndiyo wengi. wanatoka hapo. Kwa hiyo, hili litazamwe ili tuweze kuingia katika huu Muungano wa Forodha kwa sababu inaonekana bado hizi nchi mbili hazijakaa sawa, je, tukiungana nchi tatu itakuwaje? Mimi nilikuwa napenda katika hili Mheshimiwa Waziri Mramba tuandae mikakati ili sisi tusinung'unike kule Zanzibar kwa sababu kila siku tunalamikia tu bandari ya Dar es Salaam inavyonyanya wa fanyabiashara wadogo wadogo. Wale wanaokwepa kodi, wakubwa siyo ninaowasemea, wale wanajulikana na *TRA* kwa majina na kampuni zao. Mimi nasema hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wanaotokea Mlandege, wakapanda boti zao, lakini wakifika bandarini wanapata matatizo. Naomba hili litatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka kuchangia ni kuhusu bajeti na wanawake. Nimeweka hivyo bajeti ya wanawake kwa sababu imesema katika hivi vitabu vya hotuba zote mbili kwamba tupo wengi idadi ni asilimia 17.7 katika nchi hii na wanaume asilimia 16.9. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukubali sasa wanawake tupo wengi na tunashukuru Serikali safari hii imetujali maana yake imeonyesha wazi kabisa katika vifungu vyake mbalimbali, ukisoma utakuta kwa mfano ukurasa wa 41 wa hotuba imesema kabisa: "Serikali inatambua matatizo yanayowapata wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wanawake katika kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao za kibiashara". Maana yake tumetajwa, tunaposema wananchi na wanawake wamo ahaa, tunajijua lakini unapotutaja na sisi tunapata nguvu za kutetea haki zetu. Kwa hiyo, tunakushukuru Waziri Mramba kwa kutufikiria na kutupatia huu mkopo ambaa utawasaidia akina mama kwa biashara zao ndogo ndogo. Sote tunaelewa Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yetu akina mama wanasuka, wanafuma vikapu, wanasuka mikeka na kupika vyakula mbalimbali kama mandazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba na akina mama wenye wakilizite kwa makini kwamba kuna mfuko utakaowasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, wao wawe makini, Waziri anayehusika akituelezea taratibu zake tuwe tayari kwenda kukopa. Kwa hiyo nashukuru sana. Napongeza Serikali kwa kuondosha hizi kero za kodi ndogo ndogo, hizi pia zinawagusa wanawake wengi kwa sababu wao ndiyo mara nyangi wanadhalilika na hizi kodi ndogo ndogo kwa mfano, kodi za baiskeli. Vijijini baiskeli ndiyo magari yao, kwa hiyo mara nyangi mtu anachukua mtoto wake anampeleka labda hospitali anakamatwa, anaambiwa lipa shilingi mia sita au mia saba. Kwa hiyo, anayeumia sana ni mama kule nyumbani maana ndiye anayesubiri na hamwoni baba wala mtoto, kumbe wamekamatwa na anadhalilika. Kwa hiyo naishukuru Serikali kwa kutuondolea hizi kodi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali kwa kupunguza kodi ya gesi. Sasa hii pia ni nzuri sana hasa kwa wanaokaa Mijini itasaidia maana mkaa ni ghali isitoshe tunaambiwa tusikate miti lakini hapa itasaidia kama nishati mbadala. Kwa hiyo, tunashukuru sana na akina mama naomba tutumie sana hiyo gesi kwa sababu hakuna moshi, afya yako inakuwa nzuri na haya macho hayawi mekundu kama wanavyotumia kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunashukuru kwamba itawekwa benki ambayo itasaidia mikopo kwenye mifugo. Kubwa kabisa hii bajeti na wanawake tunashukuru kujengwa ukumbi mpya wa Bunge kwa sababu sisi tuna asilimia thelathini na hatujatimiza. Sasa ukija ukumbi mpya tutaingia sote maana leo tunaambiwa ukumbi umejaa. Sasa ukumbi huo mpya asilimia thelathini yetu tutaingia. Tunaishukuru Serikali kwa kuliona hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda nimpongeze Waziri wa Utalii kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na *TTB* na *TANAPA* kwa kutangaza vivutio ndani na nje ya nchi na ndiyo maana biashara ya utalii imekua. Siyo kubwa sana kwa sababu matatizo chungu nzima yametokea hapa nchini lakini angalau kutoka asilimia 6.7 mpaka saba. Hivyo tunashukuru biashara ya utalii imechangia uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, pamoja na jitihada zote za Serikali tumeambiwa humu kwamba bado viwanda vina matatizo hasa umeme na maji. Umeme ni ghali. Kamati yetu ya Biashara na

Uwekezaji tumekwenda Kiwanda cha Urafiki tumekuta hilo tatizo ni kubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri Mramba hebu wasikilize. Marehemu Mwalimu Nyerere alisaidia kiwanda kile kukifanyia kazi kimefufuka, sisi wanawake tunafurahia vitenge na khanga. Ubia wanasema bado Wizara ya Fedha hamjatoa asilimia yetu yao wao ipo tayari wameshaweka fedha zao. Hebu wasikilize kwa sababu kile kiwanda kina historia na wamelalamika sana na hao wenzetu wa China wametusaidia sana mpaka leo. Kwa hiyo, naomba tuwasikilize kama kweli kuna hiyo pesa kidogo Serikali yetu ya Tanzania itoe, wametuambia sisi kwamba Serikali yao tayari basi naomba tuwasaidie ili na sisi katika nchi yetu hizi khanga na vitenge tuweze kusafirisha nchi za nje ili viongeze uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine vile vile napenda nizungumzie mpango wa elimu wa sekondari. Naishukuru sana Serikali imeonyesha kwamba safari hii wasichana wameongezeka kutoka asilimia thelathini na nane mpaka arobaini na mbili na hayo ni mafanikio makubwa maana sekondari tulikuwa tunashuka na sasa tunapanda. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwamba ada pia wasichana wamesaidiwa kama asilimia arobaini na mbili. Lakini kama walivyosema wenzangu elimu ya sekondari ni muhimu katika kuandaa wataalam katika mambo mbalimbali. Sasa kule kwetu Zanzibar tuna shule yetu ya Lumumba. Hapa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mungai alikuja akaiona. Hii shule ya Sekondari ya Lumumba wanapasi mia kwa mia. Mheshimiwa Mungai ameziona takwimu na shule ile ni kama hapa tunavyosema *Tabora school*. Viongozi wengi wa Zanzibar wamesomea hapo, tulikuwa na shule mbili tu kabla ya uhuru. Lumumba ya wanaume na sisi yetu ikiitwa Saida Maatuka ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ile ndiyo nzuri na ningeomba sana msaada, ingawa si ya Muungano kama tunaandaa watu wetu kwa nini haiwekewi motisha, haina uzio, punda wanapita, ng'ombe wanapita, shule ambayo ni best katika Zanzibar. Halafu vile vile badala ya kutumia bansel banners wanatumia vibatori. Mtihani utakuwa mmoja wa Tanzania Bara na Zanzibar lakini maandalizi ya Bara yameshawekwa na mipango yake Zanzibar bado na tunaingia Chuo Kikuu pamoja. Jamani naomba kama tunazungumzia kweli ile ya Muungano na kupata wataalam tuendeleze ili nchi yetu basi tuitazame hii shule. Hii ni shule mojawapo ambayo ni nzuri na ina mafanikio. Naomba itazamwe kwa jicho la huruma na Mheshimiwa Mungai atakapokuja ataelezea kwa sababu alikuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa na mimi napenda niseme. Haya yote tunasubiri mipango ya utekelezaji ili tuweze kufanikisha yale malengo yetu tunayotaka ili kukuza uchumi wetu. Kwa hiyo, mimi nashauri elimu kwa umma ni lazima. Mheshimiwa Mramba haya yote tunayozungumza kama hamjatuelimisha wananchi yatakuwemo humu humu Bungeni wajanja watatumia nafasi hizo na wengine bado tutakuwa tunasikitika na halafu nchi pia haiendelei. Hiyo mimi naomba elimu kwa umma iweze kuwekwa katika ngazi zote kuanzia sisi Wabunge twende Mikoani, Wilayani na vile vile Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nilikuwa nimekata tamaa hapa nilifikiri kwamba sitapata nafasi lakini nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kuwapongeza Wabunge wenzetu ambao wamejiunga na sisi nawapongeza sana na naahidi kwamba tutashirikiana nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunazungumzia Wizara ya Fedha natambua kwamba Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga wamepewa nafasi mpya na kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha nichukue nafasi hii kuwapongeza sana. Matumaini yangu ni kwamba watafanya kazi nzuri na tutafikia malengo ambayo tumejiwekea. (*Makofi*)

Mimi naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba kwa kazi nzuri waliyofanya. Mimi nataka niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha *and it is my sincere judgement* kwamba kazi iliyofanyika katika kipindi hiki cha bajeti kwa hotuba zote mbili ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya nani alisema nini, nani alishauri nini *is not an issue. Issue* ni nani aliyefanya kitendo hicho, Chama cha Mapinduzi kupitia Serikali yake *full stop*. (*Makofi*)

Wewe umesema, umefanya nini *fine good talk* sisi tunachoju ipo Serikali *responsible* imejibu, inasema sisi tunafikiri kodi hizi zinaleta kero kwa wananchi, *full stop*. Kama wewe uliwalii kusema huko *fine inaonyesha* kwamba Serikali hii inajali hata Wapinzani wakizungumza. Kwa hiyo, *what matters* hapa Serikali iliyoko madarakani imefanya maamuzi gani ya kisiasa, *impact* yake kwa wananchi ikoje. Hii ndiyo *issue* ya kuzungumza hapa. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba ni nzuri. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya mipango ni dhana ambayo inatokana na nchi zinazofuata mfumo wa kijamaa. *Is a socialist component.* Sisi sio wa kijamaa na ndiyo maana naungana na Profesa Mbilinyi alipomtaka Mheshimiwa Dr. Kigoda amweleze kwamba katika mazingira ya leo ile Tume ya Mipango ipo au haipo. Kwenye mfumo wa kibepari hawapangi, wanapanga katika *level* ya *enterprise*, hawapangi hivi, wanavyofanya kule Marekani ni *ku-coordinate* lakini hawapangi. Hii *component* inayozungumzwa hapa hii ni ya kijamaa, nchi hizi zenye *orientation* ya kijamaa kwa sababu njia kuu za uchumi zipo mikononi mwa umma kwa maana ya kule nyuma tulikotoka, basi kuna *Economic Commission* ambayo ipo pale. Sasa nilitaka nisaidie hapa.

Bajeti ni mpango wa Serikali unaonyesha namna Serikali itakavyopata fedha na namna itakavyotumia na haya yote yameelezwa vizuri hapa. Nataka kuweka *concept* hii vizuri kwa sababu mbele ye safari kule nitaingia *speed* na nini, kwa hiyo nataka nieleweke kwamba nasema nini. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kilichofanyika katika *micro level* hizi wanaziita *economic fundamentals* umeweka mazingira fulani, huna mtaji umetaka *ku-attract* mtaji unaweka *Bureau De Change*, unaondo urasimu, unaweka *Stock Exchange Market* na nini una *VAT* na ndiyo nilikuwa nazungumza na hii ni vizuri tukaelewana humu ndani kwa sababu mimi kila wakati nimesema ningetaka nione bajeti hii na mipango yetu inakuwa na *one to one function* kati ya kukua kwa uchumi na maendeleo ya wananchi, nataka nione hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa kila wakati tunaizingumza wapi inajitokeza kwa sababu mimi natoka katika Jimbo la Siha, nikitoka tu kichwa kichwa hapa nikaenda kule, nikawaambia wananchi, mnajua bajeti hii inaonyesha uchumi wetu umekuwa, hali yetu ni nzuri, wataniambia mwisho wako wa kukuchagua ni leo, hatukuchagui tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima iwe na maelezo yake, kuna hiki kitu alifanya Bill Clinton pamoja na matatizo yote aliyoukuwa nayo, Wamarekani wale walifika mahali wakaingia kizunguzungu kwa suala la *Trickling Down Policies*, toza kodi, Serikali itoze kodi lakini kodi ile mafanikio na manufaa yake yaende chini kwa mwananchi mmoja mmoja. (*Makofi*)

Hii huwezi kuisema tu hapa ukaishia hapo bila kuwa na mkakati, lazima useme hayo matrillioni yatafikafikaje kule kwa wananchi mmoja mmoja. Ni maoni yangu ukiondoa kodi kama ziliwa sitini zikabaki nane *it is my judgement* kwamba upo kwenye mstari huo wa kuhakikisha kwamba unamfikia mwananchi mmoja mmoja. Maana unamwondolea gharama ambazo ni *unnecessary* hazina maana na sisi tumeziona hapa umeondoa kodi ya maendeleo, umesema hii naiondoa naiona kwamba ni kero.

Mimi naona kwamba unamsaidia kwa sababu sasa atapeleka katika maeneo mengine. Kwa hiyo, hili ndilo tunalolitafuta hapa, unafika mahali kunakuwa na unafuu wa kodi maana yake ni kwamba na bidhaa zetu uzalishaji wake gharama zake zitakuwa ndogo. Kwa hiyo, *impact* utaiona. Hiyo *number one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hakuna Serikali ya nchi yoyote duniani ambayo itaondo umaskini kwa maana ya kutoa pesa ili umpe mtu mmoja mmoja. Unachofanya wewe ni *ku-create an enabling environment* kwa maana ya kwamba huduma muhimu, hospitali, elimu, barabara, umeme, maji vipatikane kwa bei nafuu kwa mkulima mmoja mmoja. Hayo ni maoni yangu na hii naisema kabisa kwa *courage* kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, *I see seriousness in this* na mimi nataka niseme kwamba napenda kupongeza Serikali kwamba *ime-address* jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huishii hapo, lazima utuonyeshe *conduit* itakayopeleka kule chini utapitia wapi, Halmashauri, Vyama vya Ushirika, utawapa kwa mkono au utafanyafanyaje? Lazima

utuambie. Chama cha Siasa na Serikali iliyopo madarakani lazima ijenge kada ambayo itapeleka mafanikio haya kule. Soma taarifa ya *LAAC*, soma taarifa za *PAC* si nzuri sana. Huna kada, huna *system* ambayo itapeleka haya maendeleo kule kwa wananchi. Kwa hiyo, ni lazima u-create hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Abraham Lincoln, mimi sasa nataka nitumie hawa maana yake ukitumia akina Marx utapata mgogoro. Abraham Lincoln alisema ningepewa kazi ya kukata mti kwa saa nane ningetumia saa sita kunoa shoka. Narudia ningepewa saa nane kukata mti ningetumia saa sita kunoa shoka. Ungepewa miaka ishirini na tano kuondoa umaskini ungehakikisha kwamba unatumia robo tatu ya muda huo kupanga kada maalum ya watumishi watakaofikisha maendeleo kwa wananchi wale amba ni wa kawaida. (*Makofi*)

Unae Mkuu wa Idara, unae Mkurugenzi, unazo Wizara, unao watu wapo katika *focal point* kiasi gani wapo *committed dedicated* kuhakikisha kwamba *24 hours* hizi hotuba mbili ni kauli ya siku na ni masharti ya siku na ni sheria ya siku. Huwezi tu hivi hivi ukasema mimi nitapeleka hapa, tutafika mahali tutasema tumeleta bajeti nzuri hapa Mheshimiwa Mramba tatarudi hapa watam-pin down pale kwa sababu hatukuweka kada ya kufikisha maendeleo haya, matarajio haya na matazamio haya kwa wananchi. Wanamwuuliza afanyeje sasa?

Asifukuze watu asiseme kwamba mimi nitawafukuza kwa kuwa hawatakwenda, mtu akichukua milioni thelathini au arobaini za Serikali anakuwa *dear* kwa vyombo, atafunga, atafanya nini, yeye amsukume amwambie kaa hapa pemberi wewe utakuwa unashimamia sera na nini, amwondoe kwenye mambo ya sekta.

Asimweke humo, akimfukuza atakwenda na watu watamtetea na nini atarudi tu huyu, amweke pemberi aweke watu overhaul system, watu makini ambaa hawajali hata akivaa viraka yeye yupo tayari, lakini yeye kichwani mwake ana mtu anaitwa Mtanzania anampigania. Hiyo ndiyo kazi tunayotakiwa kufanya hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mengine nisiyaseme kwa sababu humu tuna *potential* kubwa sana. Mimi nataka nieleze yale ambayo nafikiri yapo, ipo *political will* ya kuhakikisha kwamba kweli bajeti hii itatekelezwa, ipo *political will* ya kuonyesha kwamba mipango tuliyojijiwekea itaendeshwa. Mwaka jana tulipokutana hapa tuliambiwa kilimo kitapewa sehemu kubwa sana.

MBUNGE FULANI: Sekta kiongozi.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Ikaithwa sekta kiongozi. Sasa sisi tunatoka Wilayani. Mimi natoka Jimbo la Siha, maji yako wapi? Tulisema moja ya eneo ambalo tunataka tuliangalie ni mifereji ya kumwagilia kama mkakati wa kilimo. Ina-address humu lakini ipo wapi? Ukija hapa na mpango unafanya una-revisit, unafanya nini, tathmini ya mambo ambayo tulizungumza kipindi kilichopita. Tunataka tuione hapa kilimo hiki cha ku mwagilia kimepewa *prominence* gani? Tumezungumzia habari ya Mikoa, mimi watu wa Rukwa sina ugomvi na ninyi mimi nasema ni sawa kabisa, ile walijopewa ni sawasawa kabisa.

Lakini *the basic contradiction* katika nchi yetu ilikuwa ni nini? Tanzania ni nchi ambayo inafika mahali haiwezi kujilisha hasa ukiwa katika vipindi hivi vya ukame. Una-resolve vihi hiyo *contradiction* kwa ku-serve Mikoa minne na ile mingine umeacha pale.

Mimi nilifikiri kwamba kulisha Tanzania ni kumwezesha mkulima mwananchi mmoja mmoja kujilisha. Kwa hiyo huwezi ukasema utaishia Rukwa tu. Huwezi kuishia hapo actually kama hakuna chakula, kukibeba chakula pale kwake Profesa Mwandoza kukipeleka *Siha is very expensive*. Kuliko kutoa pale Kenya. Unasema nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba moja ya *potential areas* ambazo nimezi-*identify* na nitazipa mbolea, sawa. *What about the rest, what about the rest address the fundamental contradictions.* (*Makofi*)

Wakulima wa Tanzania sasa hivi wanachohitaji ni kupata mbolea kwa ajili ya mazao yao, Tanzania nzima wanashindwa kulima kwa sababu sasa hivi mfuko mmoja wa *Urea* ni shilingi 18,000/=.

WABUNGE FULANI: Shilingi 25,000/=.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Ishirini na tano, wananiambia mimi nasema kule Siha, unajua mimi kila siku Siha shilingi 18,000/=, sasa 25,000/= aondoe hiyo Mheshimiwa Waziri. Walikutana wenzetu hapa akina Shirak na akina George Bush wakaenda hapo Geneva wakawaambia wakulima ondoeni ruzuku, pale wakasema kata kata haiwezekani.

Haya ni Mataifa nakubwa yanakataa yanasema *subsidy* lazima ibakie pale pale, Marekani, Ufaransa katakuwa haka Katanzania, Kamalawi au Kazambia. Tunapata matatizo gani wewe mwenyewe kwenye hotuba unatuambia kwamba hakuna shinikizo lolote la *World Bank* wala kitu chochote. Tufanye hii basi na tufike mahali tuthubutu tuseme hivi sisi tunasaidia Mheshimiwa Mramba tuweke ruzuku kwenye kilimo chetu, kwisha hapo tutakuwa *tume-resolve the contradiction*. Hawa utawapa *prominence* yao, utasimamia na vitu vingine vya namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tulikuwa tunawaambia wananchi tuachane na utaratibu wa kutegemea zao moja au mawili. Leo tunaambiwa humu kwenye hotuba tukachague mazao mawili *it is going to be counter productive*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza utawachanganyachanganya hawataelewa kwamba huyu anazungumza nini. Wewe ulikuwa unasema, kule kwangu mimi kahawa imeanguka, nakwenda kule kuwaambia tuchukue zao gani sasa?

Nitakwenda kuwaambia nini si nitawachanganya! Ninachotaka kusema hapa ni kwamba mazao yote yanayolimwa katika eneo ni muhimu kwa Wilaya husika. Usichague, wewe sema ninyi mna kahawa pale, ninyi mna mvua za vuli, ninyi mna mvua za masika, mna *volcanic soil*, endeleeni kwa mazao yote magimbi na maboga na kila kitu kinacholimwa waendelee kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi nyuma, tukienda kuwaelekeza unampa maelekezo *Regional Commissioner, District Commissioner, Mkurugenzi, Mtendaji* wa Kata na Kijiji unamwelekeza mwelekezaje au unamwambia ambiaje? Unamwambia kutoka sasa kasimame kwenye kahawa, migomba, mahindi, mihogo na hivi vingine, utawachanganya changanya hawa jamaa, watashindwa kukuelewa. Mimi naomba tupate maelekezo hapa, tuelenze vizuri tunachozungumza hapa ni nini, tulitoka huko huko.

Kuangushwa kwa Kwame Nkrumah ni kwa sababu alikwenda akang'ang'ania *cocoa*, wakamwambia sasa sisi tumeshajaza bwana, hatuhitaji *cocoa* nyingine kwisha, akaondoka. Sasa hapa kwetu sisemi tutafanya hivyo, hapa kwetu sisi tupo imara, lakin mazao yetu sisi tunasema ni yapi? Mazao yote yapewe umuhimu unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kiangazi kama huu tulikuwa tunasemaje? Tulikuwa tunasema hivi, mazao yale ambayo hayahitaji mvua nyingi ambayo yanastahimili ukame ndiyo yalimwe. Leo tunakuja hapa tunamwa mbia kwamba asilime. Sasa mimi naomba *clarification*. *I know hawa ni watu makini, wana mawazo mazuri, they may be having a point on this but this is my immediate reaction as a representative* wa wananchi wa Jimbo la Siha.

Tusaidiane, sisi tunalima mahindi, tunalima ngano, tunalisha Dar es Salaam, Tanga na Arusha na Mikoa mingine. Nikawaambie waache ngano leo, mahindi au migomba, tunasema nini pale? Kinachotaka kuelezwu hapa ni nini, mboga, viazi, viazi vikuu au njegere? Mimi pale kwangu *West Kilimanjaro* ndipo kwenyewe kwenye ardhi, mimi nashindwa kusema nipeni ujumbe niwapelekee wananchi wangu nikawaambie nini? Nikawaambie kwamba *drop* haya mengine chukua kahawa, ngano, migomba au nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapakuwa na ugomvi, nilitaka tu kuunga hoja mkono na nashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Waheshimiwa Wabunge nimepata vijibarua vingi sana kila mmoja anataka kuchangia. Tunazo siku za kutosha na kama alivyosema Mheshimiwa Spika, tunajaribu kuangalia maeneo mengi. Kwanza tunaangalia masuala ya maeneo au Mkoa, tunaangalia jinsia, tunaangalia pande zote za Muungano, tunaangalia Vyama na tunaangalia maombi maalum. Kwa hiyo, yapo mambo mengi ambayo tunayatazama tunapokuwa tunaita wachangiaji. Sasa orodha yetu itaendelea jioni na kwa sababu nitakuwepo hapa hapa tutaendelea kuitana. Atakayeanza leo jioni ni Mheshimiwa William Shellukindo halafu atafuatiwa na Mheshimiwa John Singo na wengine baadaye tutakuwa tunaitana. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 Jioni)
(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ili nitoe maoni yangu kidogo kuhusu hoja za Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Awali ya yote napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja zote hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Mawaziri hawa kwa kuweka wazi na kwa kina masuala ya hali ya uchumi wa Taifa letu, juhudzi zilizofanyika katika kurekebisha na kutatua matatizo ya kukua kwa uchumi na katika kutoa huduma kwa wananchi. Vilevile nawapongeza kwa kuweka malengo ambayo yanaweza kutekelezeka. Aidha napenda kuwashukuru kwa kuweka mikakati vizuri ya ukusanyaji mapato na kufuta vyanzo vya kodi ambavyo ni kero kwa wananchi. Nawapongeza sana kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mchango wangu kwenye masuala yafuatayo. Kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuitambua Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano katika vifungu viwili vya Hotuba yake, Kifungu cha 5 katika Utangulizi na Kifungu cha 43(k). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameniomba nizungumzie kidogo kuhusu Tume hii. Sasa kwa kuwa imetajwa katika Hotuba ya Bajeti na vile vile inaombewa fedha katika Bajeti, nadhani hapa ndipo mahali pake kusema maneno machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la haja ya kuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano kama ilivyotamkwa kwenye Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (pamoja na marekebisho yake) na kutungiwa Sheria Namba 14 ya mwaka 1996, ni kwamba Dola yoyote ile Huru au mamlaka yoyote ile Huru (*Sovereign State*) inapaswa kuwa na mambo yafuatayo:-

Kwanza, lazima iwe na Benki Kuu Moja, (*One Central Bank*), lazima iwe na Sarafu Moja, (*One Currency*), lazima iwe na Mamlaka Moja ya Masuala ya Fedha (*One Monetary Authority*), lazima iwe na Sera moja ya masuala ya Fedha (*One Monetary Policy*) na iwe na Udhibiti na Usimamizi wa Mabenki Mmoja (*Single Authority for Control and Supervision of Banks and Financial Institutions*). Sasa haya ndiyo ambayo kama tunavyoju sisi Tanzania tumeungana Nchi mbili, Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Zanzibar. Kwa hiyo, katika hali hiyo tuna Nchi Moja, lakini tuna Serikali mbili. Kwa hiyo madhumuni ya Tume hii ni kuangalia namna ya Mambo ya Fedha yatakavyoshughulikiwa kwa maana ya michango kwenye Masuala yale ya Shughuli za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Tume zimeelezwa vizuri sana katika Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa hiyo ninawashauri Waheshimiwa Wabunge wayapitimayo ili waweze kutusaidia katika kutekeleza shughuli hizi. Kwa sababu jukumu hili ni la Kikatiba, na kama kuna tatizo basi tatizo hilo liweze kuangaliwa. Na pengine kuna Watu wengine walikuwa wanaona kwamba pengine hakuna haja ya kuwa na Tume; iko haja kabisa kwa sababu huu ni Muungano na kuna masuala ya Muungano ambayo yanatakiwa yashughulikiwe na kuchangiwa na Serikali zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa kitu ambacho ningependa kusema hapa ni kwamba hii Tume ya Fedha ya Pamoja inashughulikia suala moja tu la Fedha. Sasa kuna masuala mengine katika Muafaka wa Muungano wa mwaka 1994 ambao ulilenga katika kuondoa kero za Muungano ambao umejadiliwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi na kupatiwa Muafaka.

Kwa hiyo, mimi ningeishauri sana Serikali kwamba ingetazama vilevile yale masuala mengine ya Muafaka na kujihakikishia kwamba yametekelawa kwa kiasi gani. Kwa sababu ukitazama haya ya fedha tu kuna mengine ambayo yanahusika, na nashukuru kwamba Watu ambao walihusika katika kuchambua masuala haya, wamo ndani humu, nakumbuka *Attorney General*, Mheshimiwa Andrew Chenge, alikuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati ambayo ilichambua suala hili. Na nitashauri kwamba ni vizuri ule Muafaka ukapatikana kwa wajumbe wa Kamati ya Mazingira na Maliasili ambayo ndiyo yenyeh portfolio ya mambo ya Muungano ili wasaidie kufuatilia utekelezaji wake. Sisi tunashughulikia Mamb o ya fedha lakini kuna mengine ambayo yanazunguka sehemu hiyo ya fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu suala la Umiliki wa Ardhi. Hili liko katika kifungu cha 34(k) cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hili suala nimejaribu kutazama katika taarifa ya Gavana wa Benki Kuu, ya miaka iliyopita mpaka mwaka wa Fedha uliopita wa 2002/2003alikuwa anazungumzia hili suala la kuipa thamani ardhi, kwamba ni mojawapo ya tatizo katika suala la kujua thamani ya mali kwa maana ya Ardhi. Ardhi yetu hatujaipa thamani isipokuwa vile vitu vilivymo kwenye ardhi. Sasa katika utandawazi ni vizuri suala hili likawa wazi ili Mtanzania ambaye ana ardhi basi yeye ana mali. Kwa hiyo, kama anaingia ubia na Mtu nwingine basi ile thamani ya ardhi yake inaweza kuwa ni mchango wake kwenye ubia huo kuliko ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa napendekeza kwamba ule Muswada wa Ardhi uliotajwa katika Kifungu 34 (vi) Mheshimiwa Waziri angeuombea kibali usomwe kwa mara ya kwanza, (*First Reading*) halafu twende nao ili tuwasiliane na wadau ili tuwe na mchango zaidi. Kwa sababu suala hili kwa kweli linatakiwa kuangaliwa kwa kina sana, na tuweke sheria ambayo inazuia kuhodhi ardhi au kununua ardhi ambayo inategemewa na Watu wengi zaidi hasa watu wa Vijiini ambao wako asilimia 80. Kama hatukufanya hivyo kuna hatari kwamba ukishafanya *business* ya kuuza ni uuzaji halali huwezi kuupinga kama uuzaji wa hali nyingine ulivyo. Lakini kama kuna Sheria ambayo inaweka udhibiti hasa katika maeneo ya Vijiini basi tuna uhakika kwamba Watu wa Vijiini watanufaika na mali hiyo waliyonayo ambayo sasa haina thamani kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kunukuu kidogo Gazeti la *News Week* la tarehe 6 Juni, 2003, wananchi wa nchi ya Hungary walikuwa wanazungumzia matatizo ambayo watayapata wakiingia kwenye Umoja wa Jumuiya ya Ulaya (*Eropean Union*). hawa wanajihesabu kwamba ni watu wadogo na kuna Watu wakubwa ambao kama wataingia pamoja basi watakuwa na uwezo wa kununua ardhi yao.

Kwa hiyo, Watu wa huko, *Eastern Europe* wana wasiwasi. Je, sisi Watanzania tusiwe na wasiwasi? Na kama utaniruhusu Mheshimiwa Mwenyekiti nisome kitu ambacho wameandika wanasesma hivi: “*Foreign capital is welcomed when it means new jobs and factories are not welcomed when it means ceding control of the soil*”. Mwandishi anaendelea “*Without the Land there cannot be a Hungarian Nation, Land can't be multiplied like TV sets once it sets. Once it get into foreigner's hands you want get it back*”. Hao wako huko Ulaya na ndiyo wanaozungumza haya. Nadhani sisi tuijandae tuweke kinga, kinga ambayo inasaidia wanyonge hawa wasijie wakanunuliwa. Hawa Wahangari walikuwa na wasiwasi na Watu wenye uwezo wa kutoka Ujerumani, Uhlanzi na Australia kwamsba kama wataingia kwenye Umoja wa Ulaya basi watanunua basi ardhi kwa bei ndogo tu na baadaye ndiyo watakuwa na nguvu ya kumiliki uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji hasa Kifungu cha 70 kuhusu Mashirika yaliyobinafsishwa. Nashukuru na naipongeza Serikali kwamba inaweka utaratibu wa kufuatilia

Mikataba iliyoingiwa. Lakini mimi nitapenda kusisitiza ombi la Kamati za Bunge au ushauri kwamba Mikataba ile ipewe Kamati ili Kamati zijue wamesaini nini na kusaidia kuifuatilia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hili kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wakulima wa Chai, *Usambara Tea Growers Association (UTEGA)* katika Jimbo la Bumbuli, tukishirikiana na mwenzangu wa Jimbo la Korogwe Magharibi. Tumeunda Umoja na tumeuziwa Kiwanda cha Chai cha Mponde na tumesaini Mkataba,. Mkataba ni huu hapa “*very simple*” wala siyo siri.

Lakini kuna Kifungu cha 5 ambacho kina sharti *or condition* tuliyopewa ya kuwa na *Investment Plan and Future Expansion Programme*. Tulipewa masharti kwamba tuweke *investment* ambayo itakuwa zaidi ya shilingi bilioni 1.55 na maeneo ya kuwekeza tukatajiwa, mfano bustani za miche ya chai, kukarabati kiwanda na kadhalika. Mpaka sasa sisi tumekwishawekeza kufikia shilingi bilioni 1.58. Hatujasaini *Sale Agreement*. Walikuja kukagua wenzetu wa *PSRC* na kwa bahati nzuri na Kamati yangu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashasra ilikwenda Lushoto, lakini walishindwa kufika kwenye Kiwanda cha Mpande cha Chai kwa sababu mvua ilinyesha sana na wengine hawaajaona ile milima ya kule Usambara. Lakini sisi wenyewe ilikuwa ni kazi ndogo kwanza gari likiteleza ndiyo unapunguza kutumia mafuta linakwenda lenyewe kwa hiyo hatuna wasiwasi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ndiyo nasisitiza kwamba hii Mikataba, mimi huu nitawapa wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara wautazame. Hii ndiyo Mikataba ambayo watu wamesaini. Zile Hesabu za Fedha sisi hatuna kazi nazo. Hii *investment por-folio* ndiyo tukazanie na *expansion programme* kwa sababu ndiyo madhumuni ya kuuziwa Kiwanda.

Sasa kama Mtu ameuziwa Kiwanda amekifunga, kwa kweli sijui tutamwita jina gani! Kiwanda ambacho kilitakiwa kifanye kazi na Mkataba upo. Watu wanasema ukimtazama nyani unaweza usimwue na huku kala mahindi yako, sasa wakati mwingine inafaa hujifunga kitambaa ili usiwone nyani ndiyo unaweza kumwua nyani. Na mimi nimefanya hivyo kwa sababu mimi ni Mbunge humu ndani, kama tunasema Watu wengine hawatekelezi Mikataba, kama kuna Mbunge humu ndani ameingia Mikataba na *PSRC* na hakutekeleza hana nguvu ya kuweza kuishauri Serikali kwamba hapa kuna dosari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niishie hapo na napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Napenda kusema tena kwamba naunga mkono hoja hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu jioni hii. La pili, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya kwa kuchaguliwa na kuingia katika Bunge letu hili, tunawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kabla sijaanza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, nichukue nafasi hii kumpungeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Manaibu wao kwa kazi nzuri waliyofanya na kutulete Bajeti nzuri pamoja na mpango mzuri wa uchumi na maendeleo ya nchi yetu, nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi zingine kwa Serikali yetu kwa ujumla Baraza la Mawaziri, pamoja na Mheshimiwa Rais wetu William Mkapa pamoja na kwa Chama cha Mapinduzi, kwa sera zake nzuri ambazo zimetuletea mafanikio ya maendeleo makubwa karibu yapatayo sita (6). La kwanza ni lile ambalo ni la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, ambapo tumefuta karo za shule za Msingi, naipongeza sana Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mpango wa Maendeleo wa barabara katika maeneo ya nchi yetu ya Tanzania, Kusini mwa Tanzania, Magharibi na katikati mwa Tanzania, barabara ambazo zitawenza kuondoa na kuibua uchumi ambao uko katika maeneo hayo. La tatu, nipende vilevile kuipongeza Serikali kwa kuweza kufaulu kufanya makusanyo makubwa ya kodi kufikia bilioni 100 kwa mwezi. Nina imani katika kipindi hiki tumeweza vilevile kufaulu kupita kiwango hicho ambacho tumekuwa tukikusanya

kwa mwezi mmoja. La nne, niipongeze Serikali kwa kuwa na bajeti ambayo imeweka fungu la kujenga uwanja wa kisasa wa michezo.

Michezo ni burudani kubwa na uwekezaji mkubwa katika maendeleo ya watu, na kuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu kwa kufikia lengo hilo. Lengo ambalo huko nyuma lilikuwa halitegemewi. La tano, niipongeze Serikali kwa kuweza kutawala mfumko wa bei katika miaka 10 ya utawala wa awamu ya tatu. Bei zimekuwa hazipandi sana kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali. La sita, niipongeze Serikali kwa juhudzi zote ambazo imeweza kuwaondolea wananchi kero ya kodi ya maendeleo na kuwapa wananchi nafasi ya kuweza kushiriki katika njia zingine za kufanya maendeleo yao vijijini katika kata na katika Wilaya, naipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizo, sasa niombe kwanza kutoa mchango wangu katika kilimo. Napenda pia niipongeze Serikali kwa kuanza kuipa Sekta ya Kilimo nafasi ya kwanza katika maendeleo ya nchi yetu.

Watanzania wetu wengi asilimia 80 wanaishi vijijini na wengi wao ni maskini, na wengi wao kazi yao kubwa ni kilimo, na kilimo chao kinategemea jembe la mkono, na kilimo cha jembe la mkono hakimfanikishi wala kumpatia tija mwananchi wetu. Lakini Serikali sasa imechukua hatua za makusudi za kuwekeza katika kilimo na kuboresha kilimo kuanzia mwaka wa fedha uliopita na mwaka huu na nina imani mwaka huu tutaweza kufanya makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningiomba na kuishauri Serikali ichukue hatua zifuatazo katika kilimo. La kwanza kumsaidia mkulima mdogo haachane na jembe la mkono. Jembe la mkono limepitwa na wakati, *human power*. Tusaidie wakulima wetu waende katika kilimo cha kutumia *animal power*. Jembe la kukokotwa na ng'ombe na *mechanical power*, ili kuweza kumjenga mkulima kuweza kuongeza pato lake. Naambiwa kuna matrekta yapatao 9,000 katika nchi yetu ambayo mengi ya hayo yamekuwa, labda Serikali ingeanza katika kuyafufua hayo na kuweza kujenga vituo ambavyo watu wanaweza kukodisha matrekta hayo kwa ajili ya kilimo ili wananchi wetu wasitegemee kilimo cha jembe la mkono angalau katika kulima ardhi. Kwa sababu kilimo kikubwa cha Tanzania kinatumia jembe la mkono, kulima, kupalilia, kupanda, kunyonyuzia dawa mpaka kuvuna ni mikono. Sasa kwa hatua ya kwanza tungesema tuachane na kilimo cha kutayarisha mashamba kwa kutumia mikono tutegemee wanyama kazi au tutegemee kilimo cha trekta.

La pili, katika kilimo ambalo ningiomba Serikali katika kipindi kijacho ikaliangalie sana ni kuwatambua wataalam wetu wa kilimo na kuwawezesha katika kufanya tafiti mbalimbali za kilimo. Sisi katika nchi yetu sehemu za tafiti hatujazipatia kipaumbele. Mahali ambapo tafiti zimefanyika basi fedha ambayo imekuwa ikitumika ni ile ambayo inaombwa kwa wafadhili kupitia Vyuo Vikuu mbalimbali.

Lakini sasa kuna kila sababu ya Serikali kutambua eneo hilo, tuna matatizo ya kushuka kwa bei ya kahawa, korosho na mazao mengine. Lakini nchi nyingine ambazo zimefanya tafiti za mazao yao zimeweza kuwekeza vizuri na kuwa na mazao ambayo yanakubalika na yana *quality* ambayo na bei yake iko kubwa. Kwa hiyo, tukiingiza utafiti katika kilimo na tukakipatia kipaumbele nina imani kabisa tutaweza kufaulu katika malengo yetu ya kufanikisha kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko katika *tropic* sehemu ya juu kali, joto kali na hivyo tukitegemea kwamba wananchi wetu uwezo wao wa kulima kwa kutumia jembe la mkono utakuwa mkubwa tutakuwa tunajidanganya. Wale ambao tuko katika mazingira ya kuishi na wanavijiji uwezo wao wa kulima mtu mmoja ni karibu nusu hekta, wakiwa watu 4 katika kaya basi watakuwa wanaweza kulima hekta 2, kwa sababu ya mazingira yetu ya hali ya hewa. Kwa hiyo tungefanya makusudi kabisa tukijua kwamba wananchi wetu hayo hawayawesi ili waweze kufaulu katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika kilimo ni kuipongeza Serikali kwa kuondoa msururu wa kodi ambazo zilikuwa zinawasumbua wakulima. Lakini nafikiri bado haijatosha. Kwa sababu wananchi wamefikia hatua ya kuachana na mazao yale ya biashara kama kahawa, baada ya kuona bei ya kahawa imeshuka sana hata zaidi ya gharama za kuzalishia zao lile. Tungeomba Serikali iendelee kuangalia ni kodi zipi zinaweza kuondolewa na vilevile uwezekano wa kuwapatia wakulima ruzuku ili mazao hayo

wakati wa bei ya soko la dunia imeshuka yasiweze kuachwa kulimwa katika nchi yetu. Lingine ambalo ningependa kuipongeza Serikali katika kilimo ni mpango ambao Serikali imeonyesha nia ya kutoa mikopo kwa walikuma wadogo hili ni jambo nzuri sana na tunaipongeza Serikali. Lakini wakulima wetu wadogo hawana dhamana na hawana uwezo, Serikali iangalie kwa njia ya pekee sana ni vipi watawasaidia wakulima hawa ambao hawana uwezo wa kupata mikopo hii wawekewe masharti nafuu.

Nimesikia kwamba Serikali ina mpango wa kuanzisha Benki Maalum kwa ajili hiyo naipongeza Serikali vilevile. Lakini nafikiri Serikali inaleta hoja hii wakati ambapo tuna *National Micro-Finance Bank*, sasa inanikumbusha mfano wa baba mmoja kule kwetu Kilimanjaro ana beberu wake anataka kumchinja kwa ajili ya kisusio, lakini akakosa kisu, sasa yule beberu pale alipofungwa, alikuwa anafukua pale chini kwa miguu yake, kishapona kuchinjwa lakini kwa bahati mbaya akafukua kisu, sasa na kule kupona kukapotea. Sasa Mheshimiwa Waziri, kisu kimefukuliwa sijui huyo beberu attachinjwa ama ataendelea kubaki. Kwa hiyo, mimi naomba niipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kuwawekea wananchi wetu maeneo ya kuwekeza katika kilimo kwa kupata mikopo. (*Makofi*)

Sasa nichangie kwenye madini. Sheria zetu za madini ni za mwaka 1997, 1998. Mimi nafikiri wakati ule tulikuwa hatujawa na wawekezaji wengi walikuwepo akina Williamson peke yao. Sasa hivi wako wengi wanapenda kuwekeza katika madini. Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuona kwamba tuliweka sheria kwa mazingira ya wakati ule, sasa sheria hizi ziangaliwe upya ili Taifa letu liweze kupata faida kubwa kutokana na madini hayo. Kwa sababu madini hayo mahali yanapovunwa ndipo wananchi walipo. Sasa wananchi wanaposikia kwamba nchi yao bado ni maskini basi wanakata tamaa.

Sehemu nyingine ambayo ningependa kuchangia ni katika mkakati wa kupunguza umaskini. Wananchi waelimishwe mpango mzima wa kumtaka kila mtu mwenye uwezo afanye kazi.

Hili ni moja ambalo linatufanya tushindwe kujenga uchumi wetu. Wananchi waelimishwe kwamba wanatakiwa wafanye kazi, kila mtu mwenye uwezo afanye kazi. Ikiwezekana Serikali imwekee mazingira muafaka, *enabling environment* ya kufanya kazi, tumeondoa kodi ya maendeleo, tumeondoa karo za shule za msingi, sasa hakuna sababu kwa nini wananchi wenyе uwezo wasifanye kazi, tukawaelimishe, viongozi wote, Waheshimiwa Wabunge, ma-DC, waweze kuwaelimisha wananchi wafanye kazi ya kuzalisha.

Lakini njiombe Serikali vilev ile kuangalia kuwfakishia wananchi huduma vijijini, huduma muhimu za umeme na simu. Hivi ni vitu muhimu katika maendeleo ya uchumi wa sasa. Wananchi hawa wanaweza kuingia katika uzalishaji, lakini huduma hizi kama hazipo uzalishaji wao utakuwa bure. Tunaomba umeme upelekwe vijijini.

Hiyo ni sehemu moja ya kuweza kufanikisha mkakati wa kuondokana na umaskini. Simu kule katika Jimbo langu kuna karibu tarafa tatu, hazina huduma ya simu na ni tarafa za mlimani, usafiri ni shida, tarafa ya Mambamuta, ya kule Ngonja na Mwembembaga hakuna simu, mwananchi inabidi asafiri kilomita nyingi tu eti kwa ajili ya kupata huduma ya simu katika karne hii baada ya kujitawala miaka zaidi ya 40. Tunahitaji hili katika mpango huu ambao sasa tunapeleka huduma hizi vijijini zifkishwe. Vile vile umeme ufikishwe huko vijijini. Tarafa hizo nilizozitaja hazina umeme na kama zina umeme ni sehemu chache tu, tunaomba nao wafikiriwe kupelekewa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije lingine la utendaji Serikalini. Kila mwaka tunaletewa bajeti nzuri hapa, ina mipango mizuri sana. Lakini kwa sasa tunahitaji Wahasibu kama tulivyoweza kuboresha upande wa TRA wakalipwa vizuri, wakafanya kazi vizuri na Wahasibu wetu Serikalini nao wapewe hiyo nafasi, wao ndiyo wanaotunza hesabu zetu zote za fedha zinazopitishwa na Bunge.

Lakini kwa sababu ya kuwa na mazingira mabaya ya ajira hatuna Wahasibu wa kutotosha, na ndiyo maana kila mwaka tukiletewa ripoti za fedha ni mbovu. Wanakimbia wanakwenda sehemu ambako ajira ni nzuri. Tunaiomba Serikali kwa makusudi sasa iwaangalie Wahasibu katika nchi hii kama vile ambavyo iliangalia TRA. Ili yale tunayoyapanga yaye na wataalam ambao wanaweza kuyaangalia kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mishahara ya watumishi. Serikali ilifanya *retrenchment* ya wafanyakazi kwa kuahidi kwamba itakuwa imeweka misingi mizuri ya ajira. Sasa nafikiri hiyo ahadi ya Serikali isisahafulike kabisa, kwamba idadi ya wafanyakazi imepungua sasa kuna kila sababu ya mishahara yao ikawa minono ili wafanyakazi waondokana na kero mbalimbali za kuwafanya wasifanye kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Mashirika ya NSSF na PPF zile fedha zinazokusanywa tunaomba kuwepo na msingi angalau wa wafanyakazi wanaohusika kupata mikopo ya kujenga nyumba. Ulaya watu hawajengi nyumba zao kwa fedha zao hawana uwezo. Sasa hapa wafanyakazi wetu wanapata fedha wapi za kujengea nyumba. Tunaomba wapewe msaada huo ili waweze kuondokana na kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mafao ya wale wanaoacha kazi. Sheria inawataka wafikie umri wa kustaafu ndiyo wapewe mafao yao. Siku hizi kwa sababu ya maradhi mengi pamoja na gongwa la UKIMWI wengi hawafiki umri wa miaka 60 na hata takwimu zinaonyesha kwamba umri umeshuka mpaka miaka 46. Sasa ile sheria kwa sababu ya maradhi imepitwa na wakati. Mtu anapoondoka kazini na hategemei kurudi tena kazini apewe mafao yake akayatumie, vinginevyo akija kufikis ha miaka 60 atakuwa amekufa na atakuwa hajafaidi mafao yake. (*Makofi*)

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu marekebisho ya kodi ya dawa ya mbu. Tunaomba ishushwe, halafu na vyandarua tunaomba kodi ishushwe. *Petroleum Jelly* tunaomba ishushwe hiyo inatumika kwa watoto sana. Watoto wadogo lazima watumie *petroleum Jelly* ishushwe. Kodi ya VAT kwa magari, tunaomba na Waheshimiwa Wabunge waondolewe hiyo kodi kwa sababu yale magari hayana tofauti na ya Serikali tunayatumia kwa huduma za watu huko katika majimbo yetu. Mashirika ya Dini yameondolewa hiyo VAT, kwa nini sisi tukailipe. Tunaomba Serikali ifikirie kuondoa VAT kwa ajili ya magari ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa kutuletea hotuba nzuri, na mimi naunga hoja mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Kwanza, nianze kwa kuzipongeza hotuba zote mbili zilizowasilishwa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Serikali kwa ujumla na Baraza lote la Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi pia zimwendee Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mama Nyoni ambaye ni mwanamke aliyewenza kuhimili Wizara hii na kubuni ubunifu huo aliouonyesha hivi sasa. Huyo mama ni mwenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi wa TRA walioteuliwa jana na Mheshimiwa Rais, kwa kweli imedhihirisha wazi kwamba hotuba hii hata Rais anaiunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni wa CCM, Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed, Mbunge wa Mpanda Magharibi, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mbunge wa Kasulu Kusini na Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero pamoja na Wabunge wenzetu wengine walioingia kwa tiketi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza hotuba hii kwa suala zima la kodi ya maendeleo ambayo ilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi. Wabunge wenzangu waliotangulia

wameongea sana. Kwa hiyo, sisi pia kama wanawake ni lazima tulichangie ili ionekane kwamba Serikali imetutendea haki katika jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala la kodi lilikuwa limetenganisha hata nyumba za watu hasa akinamama wengi walikuwa wanaishi bila waume kwa sababu ya kodi. Baba anakimbia anamwacha mama na watoto kwa kuogopa kodi. Pia niwapongeze kwa kuondoa kodi za biashara ndogo ndogo. Asilimia 85 ya wafanyabiashara ndogo ni wanawake. Niliona sina sababu ya kutokuongea au kuchangia suala la kodi ya maendeleo na kodi nyingine ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Serikali kwa uchungu mkubwa kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Sheria na Katiba, kama sheria itaruhusu au haitaruhusu kufuatana na mapendekezo ya Waziri wa Fedha aliyopendekeza Kifungu namba 50 ukurasa wa 52 amezungumzia marekebisho ya sheria mbalimbali. Kifungu hiki nilikuwa naomba pia kitumike kwa vijana na wanaume waliokuwa wamefungwa katika kipindi hiki cha ukusanyaji kodi cha kutokuwa na uwezo wa kulipa kama wako Magerezani wangepewa msamaha pia wakawa nje ili washirikiane na familia zao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi hapa tutakaa kupiga makofi lakini familia zingine ndani yake wako vijana wao ambao ni nguvu kazi wamo ndani kwa kutokulipa kodi, wapo wanaume ambao wameacha familia zao na watoto wako ndani, wamehukumiwa kufungwa, kama wapo nilikuwa naomba na kuishauri Serikali iwaachie huru hawa watu ili tushirikiane nao katika kusherehekea hili suala la kodi ya maendeleo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuchangia suala zima la Bajeti yenewe. Kuna Sekta ya Ubinafsishaji wa Viwanda au Uwekezaji ndani ya Viwanda. Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, amezungumzia suala zima la kufufuliwa kwa baadhi ya viwanda. Kila ninaposimama mimi katika njadala wa Bajeti ni lazima niongelee Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kwa kweli mpaka sasa tangu mwaka 2001 najaribu kuchangia ili angalau niipe Serikali msukumo wa kufikiria kwamba nayo hii ni moja ya kero ya wakazi wa Tabora. Kwa sababu kiwanda hiki Serikali ulipokileta ilijua kwamba asilimia kubwa ya umaskini wa wakazi wa Tabora utakuwa umepungua, usiondoke wote lakini utakuwa umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa cha kushangaza katika hotuba zote nimejaribu kusoma, kupekuwa, kuangalia mpaka macho yanaingia giza siaona kama kuna mahali kimezungumziwa Kiwanda cha Tabora Serikali ilishaweka fedha nyingi kwenye Kiwanda kile. Kuna majengo mazuri, kuna mitambo mizuri sasa hebu Serikali itueleze kuna matatizo gani au kuna mkosi gani uliotokea kwa yule aliyekuja wa kwanza, ama wa pili au wa tatu, kuna nini kilichosababisha kiwanda hiki kwa kweli kisifanye kazi mpaka sasa?

Hili ni tatizo. Tunasherehekea mambo mengine lakini kama kweli Serikali ingekwenda kule kwa makini ingeelewa kwamba ninachozungumza ni nini kwenye kiwanda kile, wangekuwa na uchungu na fedha za Serikali zilizokuwa zimetumika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia nizungumzie hili suala la barabara. Suala la barabara ni kero katika kufufua uchumi. Sisi tumepakana na Kigoma, Mbeya, Dodoma, Rukwa na Mwanza. Lakini hizi barabara za kufungua njia kuu za uchumi mpaka sasa hakuna matarajio yoyote. Nimejaribu kusoma kwenye kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2003/04 wamezungumzia kuna Kampuni binafsi ya ujenzi ya PRODECO ambayo Serikali bado inawasiliana nao hivi mjenzi ni huyo peke yake. Mjenzi wa hizi barabara ni yeze peke yake maana yake imesema bado inaendelea na mazungumzo na huyo mfanyabiashara mjenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kampuni kama hakuna zingine hebu watoe kwa wananchi. Hapo nilikuwa naomba Waziri hebu huu mkataba ambao uko hapa hapa sio mkataba mazungumzo yaliyopo baina ya PRODECO na Serikali kikwazo chake ni nini, kiwe wazi inawezekana baadhi ya Wabunge wakaweza kusaidia kama walivyoweza kupokea na kuyafanyia kazi kwenye Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee kuhusu suala zima la SIDO. Serikali kama ingekuwa imeliangalia suala hili la SIDO kulikuwa hakuna haja ya kuhangaika tena kusema tuzipeleke wapi fedha za

kuwakopesha wanawake. *SIDO* ina mtandao mkubwa, ina uzoefu. Juzi tu kulikuwa na mashindano ya Maonyesho ya Kanda ya Wafanyabiashara ndogo ndogo yalifana sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa mgeni rasmi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, alikuwepo, aliona jinsi akinamama walivyojituma, aliona jinsi gani walemavu walivyoweza kufanya vitu vya ajabu, Naibu Waziri aliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walemavu walitengeneza kwa kubuni baiskeli zao wenye, ni nzuri ambazo huwezi kupata muda tena wa kuagiza nje kama wangeweza kupata ushirikiano mzuri na Serikali. Baiskeli hizo kama ningekuwa na uwezo nilikuwa nataka nimletee Waziri wa Fedha azione ili ajue kwa nini nataka kusema *SIDO* iwe ndiyo kiungo kikuu cha ukopeshaji wa fedha kwa wanawake na vijana hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka suala la mawasiliano. Kwa kweli mawasiliano Mkoa wa Tabora hivi sasa ninavyotamba kuzungumza humu ndani wao hawasikii, wala hawana habari labda wasoma kwenye magazeti, kwa sababu hakuna redio inayosikika. Kama itasikika ni saa 6.00 au 7.00 usiku kuna kipindi cha saa 6.00 usiku? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kiko kimoja tu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala la redio kwa Tanzania sisi tuko nyuma, tuko mwisho.

Redio anazosema mtangazaji wa redio yule mchekeshaji anasema zinaishia Manzese, basi ni bora ziishie Manzese lakini sisi hata Manzese hazifiki wala Kariakoo hazifiki.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iliangularie hili suala la redio kutuwekea angalau kituo kidogo tuweze kusikiliza na kufaidika na redio zetu. Kituo kidogo tu ambacho kingeweza kikarusha matangazo.

Pia nimwombe Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, atuangarie, tunasikiliza matangazo kwenda Mbeya, Ruvuma, Mtwara anaturuka hata sisi jirani zake. Naomba jamani atufikirie *Radio Free Africa* tuisikilize hata Tabora. Nayo pia hatusikilizi pamoja nayo inatoka Mwanza.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hayo yangu machache kwa msisitizo, nilikuwa naomba *SIDO* ipewe mikopo, pia Kiwanda cha Nyazi kiangaliwe upya, tatu tuna mapungufu ya Redio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie chandarua haraka haraka. Mimi sasa hivi nina uchungu nacho pamoja na dawa ya mbu. Mheshimiwa Waziri, tunakusifu sana kwa busara zako, lakini tunaomba kwa chandarua na dawa ya mbu hebu liangularie tena upya suala hili. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Jang'ombe, kwanza sina budi kuwashukuru Mawaziri wote waliowasilisha mawazo yao mbele yetu na kwa bahati nzuri wengi tumeyaafiki na tumeyakubali, lakini tunaamini kwamba walitengeneza ni binadamu lazima kasoro ziwepo na hii ndiyo kazi tunayoifanya sasa kuboresha zile kasoro ndogo ndogo ambazo kila mtu kwa mawazo yake ameziona kwamba ni kasoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Manaibu Waziri wote, pamoja na Wakurugenzi, Makatibu Wakuu, Wataalam na Watendaji wote walioweza kushirikiana pamoja kwa kuweza kuandaa hotuba nzuri kama hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii japo pongezi zimekuwa nyingi kwa wenzetu ambaa wamepata ridhaa ya wananchi wao kuwachagua kuingia ndani ya Bunge hili nawapongeza sana wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote mengi yamezungumzwa na kila mtu alitoa mawazo yake kwa upande wake lakini na mimi nitaongeza kidogo yale ambayo yamebakia bakia kwa upande wangu ili kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza na suala la pensheni. Ukweli Serikali imeona kero ya wastaafu na imeona iko haja ya kuwasaidia wastaafu, lakini wastaafu wako wengi ambao wapo nyuma kwa miaka mingi na wengine wako wanaendelea, la kushangaza zaidi kwamba mtu anafanya kazi karibu miaka kati ya 25 au 30 siku anayosema anastaafu basi hakuna takwimu wala taarifa zozote za kumpatia mafao yake kilichopo ni nenda rudi.

Kwa kweli inashangaza sana kwamba hawa watu walikuwa watendaji wazuri, walikuwemo katika Wizara kwa muda mrefu tu lakini ile siku inapofika maana yake imekuwa kama ganda la ndizi, ukisha kula unalitupa kwa sababu huna haja nalo tena. Sasa hili lazima liangaliwe na tuweze kuwasaidia kwa sababu halina mmoja kustaafu sawa sawa na kifo, kila mfanyakazi litampata tu hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ninalotaka kulichangia ni suala la *TRA*. Kwa kweli *TRA* wanafanya kazi nzuri sana, lazima tuwape haki yao kama ni watendaji wazuri. Lakini kuna kasoro ndogo ndogo nydingi tu. Kwa mfanano, mwaka 2000 kulikuwa na kero nydingi za *TRA* kati ya Zanzibar na Bara kwa wafanyabiashara wetu. Kwa kweli mzozo huu uliendelea kwa siku nydingi na finali yake tulijaribu kumwita Ndugu Sanare, ili awe kama msuluhishi wa tatizo hili.

Lakini jambo la kushangaza sana ambalo linaendelea hadi hii leo tafsiri ya Ndugu Sanare, imenishinda mpaka leo. Sijui kwamba imani yake ilikuwa ndogo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar ama alikuwa ana nia gani kwa sababu kama ni tatizo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kupeleka mizigo Bara ambako ndiko kwenye soko kubwa zaidi kuliko pengine pote kutoka Zanzibar, lakini hakuweza kujali suala hilo na alijibu kirahisi tu kama matatizo yote haya mnayapata kwa nini hamleti biashara zenu Bara moja kwa moja badala ya kuleta Zanzibar. Ukweli ndio maana nikasema tafsiri yake ilinishinda mpaka hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Rais, kumwondoa katika sehemu hii, nashukuru sana na amefanya jambo la maana sana kwa sababu mahali panapokuwa na udugu hasa huu udugu tulionao wa Kimuungano tukisema kwamba tuweke ushuru wa aina moja kati ya Zanzibar na Bara, maana yake ilikuwa kwamba....

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa Bunge si vizuri kumzungumzia mtu ambaye hawezি kujitetea na ambaye hayumo humu ndani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Ndugu Sanare, hayumo humu ndani hata kama ana mambo yake aliyatenda si vizuri kufanya hivyo.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Nafikiri Mheshimiwa Mbunge, anaelewa hilo. Kwa hiyo, changia tu hoja.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana narekebisha kauli yangu kulikuwa na mtu mmoja ambaye hakutaka kuelewa tatizo hilo. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Usiendelee kubishana na kitu, changia tu, tusirudishe hadithi. Karibu.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala bora niliache kwa sababu lina ukweli naona bora niliache. (*Makofi*)

Suala lingine ambalo nahisi lina matatizo yake nilikuwa nataka nielewe tu kwamba kwa mara ya kwanza, nimeanza kusikia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna asilimia 4.5 ambayo itawekwa na imeshawekwa kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kidogo uelewa wangu mdogo nilitaka nielimishwe Waziri wa Fedha, safari hii amefurahi kuamua kwamba aisaidie Bajeti ya Zanzibar ama ilikuwa ni haki? Maana yake inastahili kwamba wapate Zanzibar kitu hiki. Hili nilikuwa nataka nielimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote suala la kuondoa umaskini, suala la kuwasaidia wananchi kuwaondolea matatizo madogo madogo, naipongeza sana Serikali kwa kuondoa kodi ya maendeleo kwa wananchi ambao kwa kweli wapo watu wa aina nydingi. Kuna wengine wamejiua kwa sababu asubuhi wanagongewa milango wanadaiwa kodi, wengine wako jela na kadhalika. Kwa hiyo, nashukuru kwamba hili limeonekana japo limechelewa, lakini litaweza kuweka heshima yetu pamoja na kuwasaidia wengi wale ambao wana matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilileta maneno mengi kwamba ni sera ambayo wenzetu wameitoa, lakini mimi naamini mwenye dola ndiye mwenye uamuvi wa kufanya yale mazuri kwa wananchi. Sasa kama hivyo ndivyo, mimi nasema wenyewe dola walikuwa na haki ya kutoa mawazo haya na ni mawazo yao si ya kuchangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kuamua kwa makusudi safari hii kutenga shilingi bilioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa ambao kweli ndio tatizo letu kubwa na la miaka mingi. Kama sasa limefikia hatua ya kupata usuluhishi kama ni kianzio basi tunaanza vizuri. Kwa maana hiyo, nina imani kwamba tunapoendelea tutaweza kupata fedha zaidi ili kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumalizia suala la ubinafsishaji. Ukweli naamini kwamba sote humu ndani tunaukubali kwa moyo mmoja isipokuwa tatizo letu aina ya kubinafsisha hilo ndilo tatizo. Sasa na hili kama litapatiwa ufumbuzi nafikiri tutaweza kwenda vizuri katika hali ambayo itatuweka sote tuwe katika mwendo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofifi*)

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwanza kabisa nianze na kuwapongeza askari wa miamvuli Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi yake nzuri na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, vile vile kwa kazi nzuri, lakini nisimsahau *RPC* wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bwana Alfred Tibaigana, kwa kazi nzuri anayoifanya Dar es Salaam ya kudhibiti majambazi. Salaam hizi zimfikie *IGP*, aangalie faili lake ili aweze kuangalia namna ya kumsaidia zaidi. (*Makofifi*)

Pamoja na maelekezo mazuri ya Bajeti na uzuri wote wa Bajeti, lakini kuna mambo ambayo ningependa nizungumzie. Tuna matatizo katika utekelezaji na mengine hayako kwenye uwazi.

Moja la kwanza ni kwa nia safi kabisa nakuomba Waziri wa Fedha katika fedha shilingi 38.7 bilioni zilizokuja kutoka *European Union* za *STABEX* kwa ajili ya manufaa ya wakulima wa Kahawa ziwekwe wazi kwenye magazeti maana tunapata shida sana kuwaeleza wananchi kwamba kuna shilingi 38.7 bilioni kwa ajili ya kuboresha kahawa, lakini tunashindwa kuwaeleza vizuri zinafanya fanyaje. Nalo hilo nakuomba sana linatupa shida sana huko tuliko kwamba mlimto kwenye magazeti kwamba kuna shilingi 38.7 bilioni ni kodi kutoka kwa wenzetu wa *European Union* na zimeletwa kwa ajili ya kusaidia wakulima wa kahawa Tanzania sasa tunataka uwazi wake ili wasinisumbue huko ninakokwenda vijijini. Kila nikienda swali la kwanza naulizwa zile fedha za *STABEX* ziko wapi, nakosa jibu.

Mimi niko tayari kugharamia gazeti *page* moja ni shilingi 200,000 ili magazeti yote yaandike vizuri matumizi ya fedha hizi na mtiririko wake na ndio maana nimempongeza Waziri wa Fedha alikwenda mpaka *Paris Club* kwa ajili ya kuomba fedha hizi ili wale wenzetu watusaidie na fedha hizi tulisaidiwa zikaja shilingi 38.7 bilioni. Lazima kuweka bayana kwa sababu mara nyingine tunasikia kwamba zinataka kutengeneza barabara sasa tunataka tujue zinafanya nini. Ni kweli zinakwenda kwenye kuboresha kahawa kama tulivyoahidiwa au zinakwenda kwenye kutengeneza barabara? Hilo naliomba sana na ndio msisitizo wangu wa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba Bajeti hii ni nzuri kinadharia. Ni nzuri kinadharia kwa sababu gani? Kwanza kabisa, mwaka 2001 tuliambiwa hapa kwamba sekta ya kilimo imepata *allocation* ya shilingi 95 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama Waziri wa Kilimo na Chakula, anaweza akasimama hapa akatuambia kweli kama alipokea shilingi bilioni 95 kama zilivyosomwa kwenye Bajeti ya mwaka 2002/2003, wala nusu yake au robo yake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyosema nadharia, sina maana kwamba ninajiropokea tu, ninakwenda *through history*. Nina wasiwaso kwamba huenda na hii ikawa ni nadharia, lakini tukipata maelezo haya kuwa ni kweli zile shilingi bilioni 95 tulizoambwa zinaenda kwenye kilimo katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 kwamba zimeweza kupatikana na Waziri wa Kilimo na Chakula, akatueleza ningeshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shilingi bilioni 38.7 zimekuja na zimefikia *treasurer*, ndiyo maana ninataka Waziri anisaidie hilo. Vile vile, ningeshukuru sana kuweza kusaidiwa kutolewa wasiwaso huo na ukishanitoka nina hakika kabisa mwaka 2005 nitarudi hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusositiza ni kwa nini nasema hivyo. Tunaambiwa utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2002 ni 52% tu, 48% haikutekelezwa! Tulivyododosu tumeambiwa matatizo mawili.

Tatizo la kwanza ni utata kwenye *Procurement Act* ya mwaka 2001, kwamba imeleta utata kiasi imesababisha mpangilio wa Serikali ambao labda ungeweza kufikia kiwango walichokuwa wamepanga kuwa ni tatizo. Sasa kama ni tatizo, hiyo Sheria tumetunga sisi na kama kuna shida kwenye hiyo Sheria basi iletensi hapa Bungeni tubadilishe tuweke utaratibu mwingine ambao hautakwamisha maendeleo. Tunataka Sheria ambazo zinapeleka maendeleo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili, tumeambiwa kwamba hawa wenzetu amba ni wafadhili kwanza ninawapongeza, lakini tunaambiwa kwamba wakati Serikali inawaambia walete hizo fedha ambazo wametukubalia, kwamba sasa tuko tayari kutumia, wakiweka *query* tu, ili uweze kujibowi tena hilo ulizo ni miezi sita mingine. Suala hilo inabidi nimwombe Waziri wa Fedha, kwa sababu yeze ni mzoefu kule *Paris Club*, wanamfahamu ni wa siku nyingi, aende kule awaambie mchezo huu siyo mzuri tunakwamisha maendeleo, kama umekubali kitu fanya, kama huwezi, sema siwezi kuliko usumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bei ya umeme. Bei hiyo ni tatizo Tanzania. Sikubali na siafiki kabisa kwamba eti kwa sababu Dola ilikuwa shilingi 7/= au shilingi 6/= mwaka 1975 leo imepanda sasa na sisi wananchi tulipie hiyo, haiwezekani! Hatukubali kwa sababu lile deni siyo la *TANESCO*, lile deni ni la Serikali, linaingia kwenye kapu moja la Serikali. Kwa hiyo, kama madeni ya Serikali yanalipwa usi-indicate kwenye *TANESCO* peke yake. *TANESCO* ni kama Mashirika mengine tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafadhili amba walitaka kuwekeza katika nchi yetu wamekimbilia Msumbiji, wengine wako Kenya wamesema hatuwezi kuwekeza Tanzania ambako umeme ni ghali namna hiyo, hailipi! Hayo ni matatizo makubwa ya nchi. Kwa hiyo, ningeomba tuliangalie suala hilo ambalo linadumaza uchumi wetu. Kwa kuongeza bei ya umeme tunakosa mengine makubwa kabisa ambayo labda yangefanikisha tukapata maendeleo katika nchi yetu na kuinua uchumi.

Binafsi nimetembea katika mashamba ya wakulima na wametoa rai hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hilo kwa mapana kuhusu umeme Tanzania. Umeme wa viwandani, wanakimbilia wanasema haukidhi, ni ghali mno. Tunanunua bidhaa Kenya kwa sababu ni bei rahisi na kwa sababu umeme wake ni rahisi. Kwa nini jambo hilo Tanzania linatushinda? Tushushe hiyo bei ya umeme ili tuweze kufanana na wenzetu kwa kujenga haya maendeleo ambayo tunasema.

Napenda kuongelea zaidi kuhusu kilimo. Tunasema kilimo ni uti wa mgongo. Katika Bunge hili kila jina la heshima tumekipa kilimo. Kilimo ndiyo kinatunza 80% ya Watanzania na ndiyo kinacholeta zaidi ya 50% ya Pato la Taifa, lakini bado hatujakipa kipaumbele kabisa. Leo tunasema eti tumeongeza fedha za kilimo shilingi bilioni 6, *what is* bilioni 6 wakati unamlipa *IPTL* fedha ya ndani shilingi bilioni 42

kwa mwaka? Kwa upuuzi tu, hizi ni pesa za upuuzi tu, shilingi bilioni 42 kwa mwaka! Shilingi bilioni 3.5 mara 12 ni shilingi bilioni 42. Ni kwa nini tusiwekeze kwenye kilimo tukapima mashamba makubwa na kuwekeza humo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, katika shilingi bilioni 129 ambazo zinakusanya kama kodi kwa mwezi, wanipe shilingi bilioni 29 wabaki na shilingi bilioni 100, nipewe Mkoa wa Morogoro kwa miaka mitatu nizalisha chakula cha kutosha Tanzania nzima. (*Kicheko*)

Nimetembelea Morogoro ina Mito karibu 280 na yote ina maji, na unawenza kufanya *irrigation* na kuzalisha nchi ikapata neema. Ninasema hayo kwa sababu naona uchungu sana, sisi tunapiga danadana, lakini tunatakiwa tupate maendeleo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda, niende kwenye ubinafsishaji. Nimempongeza Waziri kuhusu ubinafsishaji, lakini nataka anieleze ni kwa nini *Kibo Breweries* imebinafsishwa na sasa ni zaidi ya mwaka wamefunga, wameweka kufuli. Katika uchunguzi wangu ni kwamba wanataka kufanya *monopoly*, kama wanavyotaka kufanya *monopoly NMB* yaani hawa Makaburu wanataka wanunue vitu wafanye *monopoly!* Hawataki ushindani, sasa hivi *control* ya fedha ya Tanzania huwezi *ku-draw* katika *National Bank* bila kule *South Africa* kubonyeza kompyuta iseme sawa mpe huyu pesa! Wakichukua na hii *NMB* itakuwa hivyo hivyo!

Mengi ninayo ila sitakuwa na nafasi ya kuzungumzia yote, lakini ningeomba wenzangu wayasikie haya na wayatilie maanani, kwamba ubinafsishaji mwingine, mikataba ije hapa Bungeni tuiangalie. Matatizo mengi yanatokea huko nje ndiyo tunakuja kutupiwa sisi! Tatizo la *IPTL* tutalimaliza vipi? Tutawasaidiaje wazawa wawe na mashamba makubwa? Kwa mfano shamba la Kilombero ni zuri kabisa na ni katika shamba lenye mfano mzuri sana na naomba Serikali iende pale ikajifunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule bwana amewekeza pale na analalamika kwamba kuna sukari ya magendo inaingizwa ndani ya nchi! Naomba hiyo nayo izuiwe, ni mambo ya fedha hayo! Inafanya biashara yake isiende vizuri. Yule Mzungu amewekeza mashamba Amerika anasema Tanzania pekee ndiyo haitoi ruzuku kwa wakulima. Hivi tatizo ni nini? Hii ruzuku ambayo tumesema ni ya Mikoa ya Kusini, kwa nini Serikali hajasema ni shilingi ngapi zinakwenda huko? Si zaidi ya shilingi milioni 500, wakati Chama kimoja tu cha Siasa hapa kinapata shilingi milioni 630 kwa mwezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaambia wananchi maneno mazuri, lakini siyo kwenye utekelezaji, *not real*. Ndiyo maana nikasema kwamba, haya mambo mengine ni ya kinadharia na siyo yanayotakiwa. Tuingie kwenye umwagiliaji, tuzalishe na tufanye kweli kilimo na tukifanye kilimo kama inavyopasa, matatizo ya tegemezi tutaachana nayo. Hii tegemezi hatutaweza kukwepana nayo kama hatutasaidia kilimo. Madini yanayochimbwa ardhini yatakawisha, vitu vingi vitakwisha, lakini kilimo kitabakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kitaendelea kutunza Watanzania, kama hatuwekezi humo kwa namna ya pekee, hatutaweza kutoka katika tatizo hili ambalo tunalo sasa hivi kila siku Bajeti tegemezi. Sawa ni tegemezi, la kini mnafanyaje na hizo pesa? Ni kweli zinakwenda kwenye miradi ambayo inatakiwa? Ni kweli zinafanya ile kazi kwa wakati? Kwa sababu ukiwa na cha kwako unakifanyia jinsi unavyoona ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Pamba Kusini zilimwe. Hilo ni onbi kubwa sana, mwaka 2002 nilisema na mwaka 2001 nilisema. Tutapata uchumi mzuri bila kuogopa huyo mdudu, maana Msumbiji wanalima Pamba hiyo hiyo ambayo tunaikataa tunasema ina mdudu na Msumbiji wanapata fedha nydingi sana za Taifa kutokana na Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba *NMB* iwe ni Benki ya Kilimo. Mheshimiwa Waziri alituambia hapa kwamba tunatafuta Benki ya Kilimo, *why?* Kuna *NMB* iko hapa, ni kwa nini isibadilishwe ikawa ndiyo ya kilimo na ikawekewa utaratibu kama benki nyingine zilivyo duniani? Duniani kuna Benki za Wakulima ambazo zina Wataalam wa Kilimo ndani ya hiyo benki, kama unataka kulima shamba kuna mtaalam wa kilimo hapo benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hoja hii ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze Wabunge wote wapya ambao wameingia Bungeni kuititia uchaguzi mdogo wa mwezi Mei, 2003. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri sana ambayo wamewasilisha kwenye Bunge kwa mwaka 2003/2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda niwapongeze sana, kwanza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Wataalam wa Serikali walioshiriki katika kutengeneza Bajeti hii, kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii imesikiliza sana kilio cha wanyonge kwa kufuta kodi ya maendeleo, kufuta kodi ambazo ni kero kwa Wananchi kama ushuru wa mchicha sokoni, ushuru wa ndizi, ushuru wa ng'ombe, kondoo, mbuzi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii imesifiwa sana kwenye Jimbo langu la Uchaguzi na kwa niaba ya Wanamwanga wote, ninapenda niishukuru sana Serikali kwa katuondolea adha hii ambayo ilikuwa inatusibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuweka viwango vya kodi ya VAT, kwamba viwango hivi viendane na ukubwa wa biashara. Cha kuangalia hapa ni kwamba, wafanyakazi wa *TRA* na wafanyakazi wa *Idara za Biashara* katika *Halmashauri* sasa wasiwapanie kodi kubwa wale wafanyakazi wa *TRA* na wafanyakazi wa *Idara za Biashara* zile. Ninapenda nisilitize kabisa kwamba kwa kufanya hivyo watapanua sana wigo wa kodi na wafanyakazi wa *TRA* na wafanyakazi wa *Idara za Biashara* wengi sana wenye kwenye watakwenda kulipa kodi na Serikali itakusanya kodi nyingi zaidi kwa sababu imewe kwenye viwango hivi ambavyo ni *very realistic*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kodi moja ambayo imesahauliwa. Katika Bajeti hii tumesitisiza sana suala la kilimo cha umwagiliaji, lakini katika umwagiliaji kuna kodi ambayo mabonde haya yaliyopewa mamlaka ya kuangalia mito hii yanawa-*charge* wakulima wanaomwagilia. Katika vijiji vyangu vya Kileo, Kivulini, Kiria na vijiji vingine humu Tanzania, Wananchi wana matatizo ya kumwagilia kwa sababu inabidi lazima walipe kodi hii ya umwagiliaji kwenye mamlaka hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri wa Fedha, kuititia kwako, leo ajaribu kuifuta kodi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii unaweza kuiacha kwa mashamba makubwa kama *TPC, Kilombero Sugar and so forth*, lakini kwa Wanavijiji ningeshauri kodi hii iondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nichangie katika maeneo ambayo nadhani yataleta ufanisi katika Bajeti hii na zile zinazokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tulipata sifa huko nyuma kuwa Taifa ambalo limepiga hatua sana katika elimu ya ngumbaru, ile elimu ya watu wazima. Katika siku za hivi karibuni tumepata maendeleo makubwa katika kuandikisha watoto wa Shule za Msingi na tunaweza kujivuna kwamba kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuandikisha watoto wote wa darasa la kwanza tangu mwaka 2002. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiwango chetu cha kuandikisha watoto katika Shule za Sekondari ni cha chini kupita nchi zote duniani na Bajeti hii haiangalii suala hili! Tanzania imekuwa kama Kisiba hapa katikati, wenzetu wa Kenya wameandikisha watoto katika Shule zao za Sekondari 1,300,000 na sisi tumeandikisha 294,000.

Napenda niseme hapa kwamba, tumeandikisha watoto wote katika Shule za Msingi kwa sababu tuliondoa mchango wa shilingi 2,700/=. Katika Shule za Sekondari za Serikali huwezi kwenda *Form One* kama huna shilingi 105,000/= mpaka shilingi 140,000/=. Sasa, mtu anayeshindwa kulipa shilingi 2,700/= vipi unamtegemea alipe shilingi 100,000/= ili apeleke mtoto Sekondari! Atapata wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nchi yetu itaendelea kuwa Kisiwa hapa katikati. Tuna maadui watatu na ujinga ni mmojawapo, itakuwa Kisiwa cha ujinga! Wahenga walisema: "Kama unadhanani kwamba elimu ni ghali basi jaribu ujinga" na sisi tumechagua kwenda huko! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hizi ni kweli kabisa kwamba fedha ni kidogo, lakini lazima kuwe na uwiano wa kukuza sekta zote. Hatuwezi kuacha nchi ikawa Kisiwa cha ujinga, kwa sababu tunasema tutaweka fedha zote Polisi na kadhalika, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi watoto waliokuwa wanastahili kwenda kidato cha tano katika nchi hii ni 16,000 walikuwa wamefaulu, wana sifa. Watoto 6,000 wamekaa nyumbani kwa sababu hatuna walimu, hivi hatuna walimu kweli! Leo kwenye magazeti tunaelezwa kuwa watoto 6,000 amba wana sifa za kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wengi wao hawataingia, wameingia 2,500! Safari hii hata watoto waliopata *first class* kwenye mtihani wa *A level* wamekaa nyumbani hawawezi kwenda *University* kwa sababu Serikali haina uwezo! Hivi ni kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupiga mbwembwe hapa inatubidi tuangalie kabisa hivi huko tunakokwenda sawa sawa? Nina uhakika kabisa hatuendi sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba twende upya, *lets recast the whole thing*, tuangalie ni jinsi gani hata hao watoto 6,000 wanaweza kwenda *University*. Wenzetu wa Kenya wana watoto 30,000 katika *University*, sisi tuna watoto chini ya 10,000, lakini watoto 4,500 wanakaa nyumbani tunapiga makofi, haiwezekani!

Kwa hiyo, ni lazima tutafute njia hapa, haiwezekani kwenda hivi hivi tu! Ni lazima tutafute njia ya kuhakikisha watoto wetu wanakwenda na ni lazima tuongeze idadi ya watoto wanaoingia Shule za Sekondari. Maendeleo hayawezi kuja kwa watu amba hawakusoma na Shule ya Sekondari ndiyo msingi mzito wa maendeleo. Wenzetu wa *South East Asia* amba wameondoka kwenye umaskini, hawa *tigers* katika watu wao 100, watu 10 wamepata Elimu ya Sekondari, huko kwenye mtaa ndiyo wakapata maendeleo. Sisi hatujafika hata 0.01%! Hebu niambieni, tunasema mwaka 2025 tunatoka kwenye umaskini, tutatoka namna gani? Hilo moja.

Suala la pili linahusu madini. Mapato ya madini yanayotoka Tanzania ni makubwa sana, lakini tunachopata sisi kama Watanzania ni *token*, kidogo sana! Hivi wenzetu wanafanyaje? Huko nyuma tulikokuwa tunabembeleza wawekezaji, kulikuwa na sababu ya kukubali kulaliwa, lakini leo tunakubali kulaliwa kwa sababu gani? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutengeneza *ounce* moja ya dhahabu hapa Tanzania inachukua Dola 156. *South Africa* kutengeneza *ounce* hiyo ni Dola 230, lakini wao wanapewa mrahaba wa 6%, sisi tunapewa 3%, hivi ni maneno haya! Ni lazima kuna sababu kabisa hii mikataba tuirudishe, tuangalie upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, wenzetu katika madini yao wanapata karibu 30% na zaidi. Kwa sababu kwa kuwa na ile mali wanakuwa na hisa 25% ya madini yale, inakuwa ndiyo mchango wao katika kuendeleza yale madini. Kwa hiyo, pamoja na hisa wanakuwa na mrahaba. Sisi tunakuwa na mrahaba 3% halafu hatuna hisa, *we own nothing!* Inakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kabisa kwamba Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Bunge hili ichukue mikataba yote hii iangalie upya kama hakuna sababu ya kuibadilisha. Kama haiwezekani kubadilisha, hakuna ndoa isiyokuwa na uwezekano wa talaka! *There is always a possibility for divorce.* (*Kicheko/Makofi*)

Binafsi nimetembea nchi nydingi, kule kwenye nchi zilizoendelea wenyewe Kampuni zao zinazochimba hapa madini, wanayauliza makampunu haya: "Hivi kwa nini mnachukua madini ya watu maskini kwa bei ndogo kiasi hicho?" Majibu yao wanasema: "Wenye wamekubali."

MBUNGE FULANI: Ayaa, yayaaa, wajinga!

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Eeh, wenyewe wamekubali! Jamani suala hili ni lazima tuliangalie upya. Hata kama ni sawa, basi wote turidhike kwamba ni sawa. Liletwe hapa wote turidhike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nina neno kidogo kuhusu kilimo. Kwenye Bajeti hii katika kuboresha kilimo tumeambiwa kumetengwa maeneo ya kilimo cha biashara. Kwa kweli katika enzi hii ya sayansi, teknolojia na utaalam huwezi kutenga maeneo ya kilimo cha biashara. Ni lazima upeleke sayansi, utaalam na teknolojia kwa wakulima wako wadogo, uongeze uzalishaji na ndiyo nguvu iende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Asia ya Kusini, Wahindi, watu wa Malaysia, watu wa Thailand, watu wa Taiwan, China na Japan, wameleta maendeleo na kuweza kulisha watu wengi sana kwa kupeleka sayansi, teknolojia na utaalam kwa wakulima wao. Huwezi kuleta wakulima wa Rhodesia hapa ukasema utaleta maendeleo ya kilimo. Utasahau kwamba Wananchi wako 85% wanategemea kilimo kwa ajili ya maisha yao na Serikali inategemea kilimo kwa 65% ya *gross domestic product* yako. Kwa hiyo, lazima tulenge katika kuboresha kilimo cha wakulima wetu wadogo wadogo, tupeleke sayansi na teknolojia kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazalisha mahindi kwa kiwango cha 12% kwa maana pale tungezalisha tani 10 tunazalisha chini ya tani 1. Tunazalisha kilo 170 za kahawa wakati wenzetu Kenya wanazalis ha kilo 500, Uganda 600 na Vietnam 1,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofifi*)

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba hizi mbili, hotuba ya Mipango na Ubinafsishaji na hotuba ya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri wote wawili kwa kuanda taarifa zote mbili ambazo sasa zimetupatia hoja hii ambayo tunaijadili. Shukrani hizo pia ziende kwa Manaibu wao, Makatibu Wakuu wao na Watendaji wote katika Wizara kwa kuwa makini kwa kufanya kazi ambayo sasa tunaijaribu kuihakiki

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hizi nitakwenda nazo pamoja, lakini kwanza nitakuwa na maneno ya jumla. Napenda kutoa maoni yangu kuhusiana na suala zima la ukuaji wa uchumi. Lengo la Waziri ni kwamba, mwaka ujao tuweze kuwa na 6.6% kutoka kwenye 6.2%. Pia, katika kulinganisha na kuangalia hali halisi ya ukuaji wa uchumi ni kwamba nchi zilizoendelea zinakua kwa 4.6% hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii najaribu kuangalia tutakwendaje hapa? Tukijipima na nchi zilizoendelea na sisi tulivyo tunakuta kwamba tuna *gap* kubwa kati yetu na wao.

Kwa hiyo, inatubidi katika mawazo yetu tuweke mipango ambayo inatutia tamaa kubwa, kwa maana twende haraka au kama ni kukimbia tukimbie, kwa sababu tofauti inakuwa ni kubwa mno. Ni vizuri kama tunaweza tukapiga mawazo na kuangalia tutumie vivutio gani katika uchumi au tutumie mbinu gani katika uchumi kama ni sheria ili tuweze kwenda haraka kidogo. 6.6% bado ni ndogo, tujitahidi ili twende mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nikiangalia suala zima ambalo liko katika Bajeti hii hasa kuhusiana na shuehuli za kilimo kumbukumbu hivo imenitia mawazo na kusema angalau tunajaribu

kutafsiri kwa vitendo maoni yetu kuwa kilimo ni uti wa mgongo. Tuangalie jambo hilo kwa sababu utaratibu na hali halisi tunaifahamu kuwa 80% ya Wananchi wa Tanzania wako Vijijini.

Tunapopanga na kuweza kuwawekea utaratibu mzima wa kuinua kilimo na kuzungumzia masuala ya mazao ya biashara na chakula angalau basi tujaribu kuangalia tunaendaje na hali halisi ya uchumi ili wananchi vijijini waweze kuwezesha kifedha na wakipata fedha baada ya kuuza mazao yao watakuwa na uwezo mzuri wa kuweza kushiriki kiuchumi na kuchangia katika Pato la Taifa, jambo ambalo nikiliangalia, linanipa picha kwamba kama tukilitekeleza tunaweza kuanza kujikwamua kwenye matatizo mengine ambayo tunayo yanayotusumbua sasa hivi.

Kwa hiyo, suala zima nikiingalia Bajeti inataka hasa twende na wakati, twende na taratibu, tujaribu kufanya mambo haya tuweze kuwa na utekelezaji, tufanye kwa vitendo kwa mfano kama mwaka jana picha tunaifahamu na mwaka kesho ndiyo matarajio haya basi tuanze mipango ya utaratibu wa kuhakiki utekelezaji wa shughuli zetu tuweze kupima kwamba tumetenga fedha kiasi hiki, je hizo fedha zimefanya nini katika uchumi wetu? Pia tuweze kufahamu ili tuweze wote kuridhishana na kuona hali inakwenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi katika hayo mimi ningeomba labda kwanza nijaribu kusisitiza tu na kutaka kupata majibu kwenye masuala matatu yafuatayo:-

La kwanza nasisitizia hili kwa upande wa mafanikio ya Bajeti tunayoimaliza kuhusiana na shughuli za mipango ambako asilimia 52, imetekelezwa, ningefurahi na kujua ni maeneo yapi yametekelezwa vizuri na ni miradi ipi imetekelezwa vizuri. Hii inajazia sehemu ambako wenzangu wameuliza kutaka kujua kwamba kule ambako hawakutekeleza miradi ile na sehemu zipi na ni miradi ipi ya kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ukiangalia ukurasa wa 55 wa Hotuba ya Waziri wa Fedha, kuna hii hoja ya kutaka kufuta leseni au *fees* ya asilimia tano ambayo ilikuwa inatozwa kwa vifaa vya kuwindia wanyama.

Mimi sikujua sababu iliyotolewa pale ni kujaribu kulinda mazao ya ndani au vipi. Sasa kwenye hili jambo mimi sjajielewa ningependa kupata zile sababu hasa kwa nini hii leseni au *fees* inaondolewa? Kwa sababu ilikuwa ikilipwa kwa fedha za kigeni na inalipwa na watu ambao wanajiweza. Tatizo hili ni nini hasa? Hawa watu wanajiweza wana uwezo wa kulipa hizi fedha? Sasa tunajiondoa kwa nini ? Sasa hiyo sababu sjajipenda ningependa itolewe maelezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la kodi ambazo zimetolewa kwamba ni kero. Lakini ukiziangalia zinazigusa Halmashauri na ndiko yalikuwa maeneo yao makubwa ya kupata mapato ya kuweza kuijiendesa Halmashauri. Sasa ni nini Serikali inasema kuwa mbadala, hizi Halmashauri itazisaidia namna gani ili ziweze kuendesa shughuli zake? Nikiangalia kwa mfano kwa Halmashauri ya Mwanza soko la Kilumba lilikuwa ni moja ya maeneo mazuri ya chanzo cha kupata pesa na mapato makubwa.

Sasa kwa utaratibu huu hali imebadilika labda watakusanya robo ya kile walichokuwa wakikusanya kule nyuma. Sasa kwa hali hiyo ni vizuri tungepewa utaratibu mzima hasa kwamba baada ya hapo Serikali itasaidiaje Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kujua katika suala zima la huduma za afya, naona sasa msisitizo mkubwa umekuwa bima ya afya na tarehe 12 Juni, 2003 palikuwa na swali hapa Bungeni liliulizwa na Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lilikuwa swali namba 24 akitaka kujua matatizo ya huduma za afya. Lakini kuna moja ambalo tumekaa tukilizungumzia imekuwa ahadi yetu kwa wananchi kuhusiana na namna gani tuwahudumie akinamama wanaokwenda kujifungua hospitalini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo naliangalia kwenye Bajeti silioni, pia na wazee wenyе umri mkubwa nimejaribu kuzungumzia leo asubuhi. Sasa hapa tunasema nini kwa sababu huko nyuma tumeshaelezwa hili, tumewaeleza wananchi na tumekwishaweka msimamo kuhusu taratibu na hasa ukweli wa kuwahudumia hawa wapate huduma bure je, Waziri anasemaje kwenye hili?

Baada ya kusema hayo, sasa ningependa nizungumze ya jumla ambayo nataka nichangie na kutoa maoni kwenye suala zima la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja au Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusiana na jambo zima la ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya shughuli zetu za mwaka ujao, ambako amelenga kukusanya asilimia 13.3 ya Pato la Taifa, ili kwamba tuweze kuendesha shughuli zetu. Pamoja na michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwenye Bunge lako tukufu, suala la ukusanyaji kodi bado halijakaa vizuri kwa wananchi wengi, hasa uelewa wao. Matatizo mengine yamekwisha ainishwa lakini kuna mengine ambayo yanapaswa tuzidi kuyafanua ili wanaohusika na kukusanya hizi kodi waweze kufanyakazi kwa ufasha zaidi.

Kwa mfano, mfano uliotolewa ukiangalia *page 58* ya hotuba ya Bajeti kuna *table ikionyesha utaratibu wa namna gani nini kikusanywe kiwe kodi ambacho kinapaswa kikusanywe kwa mwananchi*. Kwa mfano, imesemwa wazi kwamba kiwango kadhaa kwa mfano shilingi milioni tatu inakuwa na kiwango cha kodi cha shilingi 50,000/=. Haya ni mawazo ambayo yametoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kueleza hapa ni kwamba ili kuweza kuweka urahisi na usahihi wa mambo yote kwa wananchi kwa uwazi kwa nini hizi kodi zisiwekwe wazi viwango vikatangazwa vikawekwa wazi kwenye mbao za matangazo, mtu anaweza akasoma ili aweze naye kujiteea mahali ambapo anaona kwamba amebanwa kwa sababu kuna maeneo mengi ambako wananchi wanaonewa. Kuviveka wazi viwango kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 58 itasaidia sana wananchi waweze kufanya vizuri na wasionewe na mtu yeyote na wajue viwango vyao ni nini kinatakiwa kutozwa kama kodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mwisho ambalo naliona hapa nilielezwa na walipa kodi na hili nililipata Dar es Salaam kwamba kuna mtu alikwenda kwenye ofisi ya Kodi linapaswa kulipa kodi, lakini alipofika pale akaambiwa kwamba yeche angeweza kusaidiwa na kodi yake ikafanywa vizuri, lakini akaambiwa aziache fedha pale aje arudi atakuta mambo yote yamewekwa sawa sawa.

Aliacha kiasi kama cha shilingi 250,000/=. Lakini aliporudi akakuta risiti za Serikali ni shilingi 75,000/= tu zimetolewa. Sasa hali ya namna hii inaanisha kwamba haya tunayolenga yanaweza kuwa yamefikiwa lakini Serikali ingeweza kupata zaidi kama fedha zote zingeingia katika Mfuko wa Serikali. Sasa haya yote nayasema makusudi ili tujaribu kuona utaratibu bora wa kuisaidia mamlaka ya mapato iweze kufanya kazi yake kwa ufasha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naona niseme wazi hapa ni kwamba katika hotuba zote mbili, nashukuru Mawaziri wamejaribu kusema wazi kwamba Serikali inapata mapato mengi sana hasa kwa fedha za kigeni kuititia mazao ya samaki, kuititia dhahabu, almasi, madini. Lakini tukiangalia hali halisi ni kwamba hayo yanayozungumziwa kutoka Shinyanga, Mwanza, Mara, Kagera na maeneo ya karibu ya pale, nikiangalia uwazi unakuja kwamba hali halisi ni kwamba mji wa hawa watu mkubwa ni Mwanza. (*Makofî*)

Sasa nikiangalia naona kwamba ng'ombe wa maziwa wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yuko maeneo ya Mwanza na anapomkamua ningeshauri kwamba aweze kumpatia malisho mazuri, tusimwache hivi hivi, ili kuweze kukamuliwa tena akatakopokuja kukamua. Lakini akimwacha juani itakuwa balaa anaweza hata kupatwa na kizunguzungu na kuanguka. (*Makofî*)

Sasa suala hili najaribu kulisema wazi ili lieleweke kwamba Bajeti nzima kwa kweli imeuacha Mji wa Mwanza mtupu na tukiangalia ni kwamba sasa unaelekea ndiyo kituo cha msingi kwa maendeleo mengi yetu sisi wenye na ya kitaifa kwa ujumla, tukiangalia pia na kuna Bonde la *Lake Victoria* liko eneo la Mwanza. Pia nchi jirani kama vile Congo, Rwanda, Burundi zinaelekea Mwanza. Sasa hali halisi ya Mwanza kwa kweli inahitaji kupewa msaada wa kuweza kwenda vizuri na iweze kuwa na mandhari ambayo inatakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nalisema kwa dhati kabisa kujaribu kumwomba Waziri ajaribu kuona atausaidiaje Mji wa Mwanza na Bajeti yake kama anaweza kuiweka sawa basi aweze kusaidia Mwanza tuweze kwenda sawa na tuweze kuendelea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusiana na madini. Kwa kweli suala la madini katika Bajeti hii, usipolisemea utakuwa umeacha mambo yale ya msingi na ya maana. Lakini ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji katika ukurasa wa 25 na 26 anajaribu kueleza kwamba hii migodi inasaidia wananchi katika shughuli zao za kijamii na maendeleo. Lakini haelezi ni vipi? Kwa sababu mpaka tumekaa tukipiga piga hodi na kuombaomba pale kwa ugomvi kwa nini? Hii ni biashara inapaswa biashara iende na sheria. Ipangwe vizuri hakuna haja ya kumpigia piga hodi mtu alete tu basi na ile ipelekwe tuache uombaomba endelevu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi jambo hili ningependa ili wananchi wawewe kuja wanachofanya. (*Makofî*)

Waziri atueleze hasa ni nini

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nilitaka kusema kwamba na hisa za migodi ziuzwe katika *stock exchange* ya Dar es Salaam. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi na mimi kuunga mkono hotuba za Mawaziri hawa wa wili ambao ni Mawaziri muhimu kwa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia safi kabisa nataka niwapongeze Mawaziri hawa wawili. Nataka niwapongeze Wabunge wote ambao wamechangia hotuba hii muhimu kwa Taifa letu kwa nia safi kabisa. Mawaziri hawa wawili wana mzigo mkubwa sana kwa Taifa letu hili na wala siyo jambo la kufanya masihara. Juzi tu nilikuwa namtania Mheshimiwa Said Nkumba, mbele ya Waziri wa Utawala Bora, nikasema bwana ukiangalia usiangalie upande mmoja ukasema labda kuna Mawaziri wana miili mikubwa, lakini mwangalie Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pengine amekuwa na mwili kama wa Mheshimiwa Said Nkumba, kutokana na mzigo mzito wa Taifa ambao tumemkabidhi nao. Kwa hiyo, hakuna jambo zito kama kutekeleza dhamana ya watu. (*Makofî/Kicheko*)

Kwa hiyo, nataka nimpongeze Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Serikali kwa ujumla na hakuna sababu ya kujengeana majungu wala kufanyiana wivu, ni kumuunga mkono mwenzetu kwa sababu anafanya kazi kwa niaba ya nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu hali ya uchumi wa Taifa. Mimi nataka nimpongeze sana Waziri. Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu imetoka mbali sana naomba tukumbuke, uchumi umeanza kukua miaka ya 2000. Nchi yetu mara baada ya kupata uhuru tulikuwa na kazi kubwa ya kukomboa Bara la Afrika tuisisahau haya.

Vile vile tukaingia kwenye vita vyta Uganda na Kenya, hatujakaa vizuri tumeingia kwenye migogoro ya kisiasa na mionganoni mwetu Watanzania tukazuia misaada wenywewe. Ndani ya miaka ya 2000/2003 ndio viongozi wetu wamesimamisha uchumi na kufikia asilimia 6.2, wamefanya kazi kubwa kwa kweli. Tuwape ushirikiano kwa nguvu zetu zote watutekelezee kazi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namnukuu Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kwamba kwa upande wa vigezo na viashirio vyta msingi vyta uchumi jumla, *Macro Economic Fundamentals*, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.2 mwaka 2002. Hivi jamani kuna kazi ndogo ilifanyika hapo? Tuifikirie hii hali wala hakuna pa kutafuta sera na kadhalika. Sisi tuangalie kazi kubwa iliyofanya na wenzetu kwa faida ya Taifa hili na pili lazima tuwaunge wananchi wetu mkono. Kwa kweli walituunga mkono muda wote na kwa kupunguziwa hii kodi ni halali, tusiwaogopeshe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa asilimia zote. Amezungumza kwamba ukuaji huo wa uchumi zaidi ya lengo lililowekwa la asilimia 5.9 kwa mwaka 2002 zaidi. Hivi kuna hofu gani? Sisi ni Wabunge tuna jukumu kubwa kwa taifa hili si kulaumiana ni kuelekezana. Tufanye kazi kwa faida ya wananchi wetu wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 34 nataka nieleze kwamba kuna suala la ukodishaji wa hii kampuni ya DAWASA kwa kampuni ya *Dar es Salaam City Water Service* kwa kipindi cha miaka 10. Hili nilitaka pia Serikali iliangularie sana ukodishaji usije ukaathiri wananchi kwa sababu

lazima kunawezekana kukatokea mambo atakayemiliki kampuni akaja akapata shida. Ukodishaji huu usije ukawaathiri wananchi kwa sababu kunawezekana kutokea mambo kwa atakayemiliki kampuni akaja sahihi. Hapo nataka tuwe waangalifu tutakapokodisha hii kampuni ili isije kuja kugombanisha wananchi hasa Mji wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukienda ukurasa wa 38 Mheshimiwa Waziri amesema napenda kusisitiza ya kwamba hakuna Mtanzania atakayenyang'anywa ardhi ili apewe mgeni, bali Mtanzania husika ndiye atakayetumia ardhi hiyo kumwezesha kuwekeza. Mheshimiwa Waziri, Serikali hongera sana. Suala la ardhi lazima limilikiwe na Watanzania wenyewe. (*Makofit*)

Hivi karibuni nilipokuwa nachangia nilizungumza hili kwamba hivi watu wetu watakuwaje maskini wakati mgodi umewekezwa katika eneo lao? Yule anayewekeza kwa nini hatumpi majukumu baadhi akatia saini mkataba na hawa wananchi wenyе hilo eneo kama ni wanakijiji au Wilaya fulani? Ili fedha hiyo watakayopata waweze kuendeleza maeneo kwa ajili ya kuwajengea mazingira mazuri wananchi wetu kuleta mabadiliko katika karne ya 21. Kwa hiyo, kwa hili ningeliomba Serikali iwe makini ili tusigombane. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 47 Mheshimiwa Waziri, amesema pia matokeo yameonyesha kuwa ukosefu wa ajira umeathiri zaidi vijana wenyе umri kati ya miaka 10 na miaka 34, kijinsia vijana wa kike ndiyo wanaoathirika zaidi kuliko wanaume. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa imenipa nguvu ya kuzungumza kwa uwazi kabisa. Sasa hivi kwa kweli hali ya vijana wetu imekuwa ni ya udhalilishaji mkubwa sana katika Taifa letu. Lazima tuwe wakweli. Vijana wadogo sasa hivi wanaingizwa katika biashara mbaya sana ya ngono. Tunaposoma magazeti yanatumumiza. Kama Serikali kwa maeneo tuliyopo lazima tufanye kazi. Tuna majukumu kwa Mungu, tuna majukumu kwa Taifa, tuna majukumu kwa wazazi wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi wa magazeti matatu, naomba nikuonyeshe na inasikitisha. Kuna gazeti moja hili linasema: "Nini Mombasa, nini Dar es Salaam, nini Zanzibar linasema mambo yote Tanga, anasema yote haya ni mashoga" kwenye Gazeti la Kiu. Tena linasema Tanga ambako Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ametoka huko, wasaidie sheria vijana wetu waweze kwa kweli ni udhalilishaji mkubwa katika magazeti kama haya. Tunazungumza kwa uwazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vijana wetu wako katika *age* hizo hizo katika maeneo hayo tunao watoto *serious* kabisa wala tusifanye ubishi. Kuna gazeti lingine la Jumatatu limeandika Danguro la Watoto hili hapa, lina vitoto vyenye umri chini ya miaka 15 na mmoja anaonyeshwa kwamba anatangaza biashara hiyo. Hivi hapa magazeti yanafanya halali juu ya watoto hawa?

Kuna gazeti lingine la Jumatatu linasema: "Hiki sasa kiama" kuna watoto hapa sijui wanakula kitu gani. Linasema: "Nani kawafundisha watoto hawa wa Magomeni mchezo huu wa hatari, soma ukurasa wa nne." Hivi magazeti kama haya yanasaidua jamii? Sisi tulifiki labda watakuwa wameona haya masuala watawasiliana na vyombo vyetu vya usalama kuweza kufuatilia tukaweza kusaidia jamii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limetisha zaidi suala la mashoga hivi karibuni tuliambiwa kuna mashoga 100 watatoka Marekani watakuja Tanzania kama Watalii. Tunampongeza sana Waziri kuzuia suala hili, lingeleta mgogoro mkubwa sana hapa Bungeni. Imetutisha. (*Makofit*)

Kwa hiyo, mimi nalizungumza hili kwamba vijana wetu sasa tuhakikishe tumewapatia elimu ya kutosha, tusiwe wabishi tuna dhamana kubwa ya kuwapa elimu. Leo ni watoto wadogo wanafanya vitendo hivi vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda asubuhi mazoezini leo nimefuatana na mtoto mdogo tu kama saa 12.00 asubuhi hivi au saa 11.30 alfajiri, nikamwuliza unakwenda shule, akanambia naenda kazini, nikamwuliza kazi gani? Kasema nabeba toroli hapo, nikasimama mimi nilikuwa nakimbia kutoka gesti mpaka uwanjani. Nikamuuliza umemaliza mwaka gani shule? Akasema 2001 darasa la saba, ni mdogo sana. Kama mimi mtoto wangu, ningeliona lazima Serikali iliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 52 na 53 maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa Bajeti ya 2000 Mheshimiwa Waziri amesema ni pamoja na kuboresha huduma za kijamii na kuimarisha miundombinu. Ametaja sekta zilizopewa kipaumbele ni elimu, afya, maji, barabara, madaraja vijijini na huduma za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wanasema kwamba msingi wa uchumi wa nchi yoyote duniani ni elimu, sayansi na teknolojia ndiyo msingi mkuu wa uchumi yoyote duniani. Kama watoto wote waliomaliza darasa la saba tumepewa takwimu ya watu ambao wamekosa nafasi ya kuingia elimu ya sekondari kutoka laki tano kwenda laki mbili, je tutafikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa nataka kuzungumza kwamba Pemb a tunachohitaji ni maendeleo, suala la elimu tunaomba liboreshwe sana. Katika Bajeti hii kwa masuala ya barabara nataka njue ni barabara ngapi Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatusaidia ndani ya Pemba? Tumechoka na fitina. Kwa hiyo, Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, hongera sana kwa dhati kabisa na Mungu atakusaidia na naomba viongozi wa Serikalini msibishane na watu bwana, chapeni kazi kwa dhati, hamna haja ya kubishanabishana na watu huko mitaani. Tekelezeni tu Ilani na Katiba ya nchi. Kwa hiyo, nakupongeza sana.

Lakini nataka nimnukuu Waziri wa Fedha amesema: "Uchumi tulivu umeiweka nchi yetu katika matumaini ya kufikia malengo ya dira ya mwaka 2025." Mimi kama kuna mtu anasema hatutafika hapa siamini naifahamu sana Tanzania, mwaka 1979 mimi nilikuwa Dar es Salaam, nilikuwa na miaka 19, nilikuwa Ilala nacheza mechili za daraja la Ilala, hebu fikiria wewe mtoto umetoka Pemba unacheza mechili za ligi la daraja la pili pale.

Nilikuwa nachezea timu ya *Super Star* daraja la pili, Ilala mwaka 1979. Wakati huo kama kwenda mazoezini nikipenda kuja karibu na kituo cha Polisi Msimbazi kulikuwa na ngoma, nikimwona bwana mkubwa na mkia wake anazuia watu na ngoma sasa haithubutu kuchezwa ile ngoma siaiona, anazuia pale magari watu wanapita na ngoma yao.

Lakini kutokana na hali ya usafiri wa Dar es Salaam sasa hivi hali ya watu walivyokuwa wengi si rahisi. Kwa hiyo, naifahamu Dar es Salaam. Kwa hiyo, hii dira tunaweza kufikia tusibishane, tuelekezane, tuwape nguvu wenzetu wawewe kuendeleza Taifa hili. (*Makofî*)

Nawapongeza watendaji ambao wameonekana kwamba ni kiungo muhimu baina ya Serikali kuu na wananchi. Lakini kubwa namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 44 amesema: "Bajeti hii pia imetenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada, (*Program Assistance*) ya nje kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Mapinduzi," hongera sana Mheshimiwa Waziri, nilikuuliza Bajeti ya mwaka 2002/2003 tunafaidika nini sisi Zanzibar, sasa tumepewa asilimia 4.5. Leo umenijibu nakupongeza sana na nakuunga mkono sana. (*Makofî*)

Vile vile tunapongeza sana Mheshimiwa Rais, Amani Abeid Karume, kwa kwenda na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kusema mtu Zanzibar sikubali hata siku moja, tumeshatoa Makamu wa Rais mara mbili, tumeshatoa Rais wa Jamhuri ya Muungano, mara mbili, tumeshatoa Mawaziri wengi kutoka Zanzibar wapo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini haya mengine yafanikiwe leo hii. Tuepusheni na migogoro kama kuna haki yetu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tusaidie kwa nguvu zote mtupatие. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 44 Mheshimiwa Waziri amesema: "Ni matumaini ya Serikali kwamba Tume ya pamoja ya Fedha ya Muungano ambayo imeshaundwa itazishauri Serikali zetu kuhusu utaratibu wa kudumu wa kugawana mapato. Nawatakia mafanikio mema. Mheshimiwa William Shellukindo, nakutegemea utufanyie hiyo haki yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho nataka nimalizie nchi yetu ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hili halina ubishi kabisa. Tunalaumiana kwamba uchumi tegemezi. Sasa hivi bila kusaidiwa na *World Bank, IMF* na mashirika mengine ya Kimataifa huwezi kuwa na uchumi, tunalaumu mataifa haya jamani wakitukataa tutakwenda wapi?

Mimi nawashangaa! Tunalaumu mrahaba, si tulikuwa na huo tunashindana na Kenya kwa muda mrefu wenzetu hawana migogoro ya kisasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nalizungumza kwa uwazi hili. Nataka ninukuu maneno ya Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere, kuna msemo unasema kwamba inasemekana kuwa njia bora ya kumuenzi Mwalimu Nyerere ni kutekeleza ushauri wake, je, tunayafanya hayo? Vile vile nataka ninukuu katika hotuba ya Baba wa Taifa, unasema tunalo Taifa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hizi. Ahsante sana (*Makofi*)

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hizi zote mbili ambazo ni hotuba ya Waziri wa Fedha na ile ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Awali ya yote ningependa kuunga mkono hotuba zote mbili ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na ile ya Waziri Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Pia napenda kuwapongeza watalaam waliohusika na maandalizi ya hotuba hizo zote mbili. Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Wabunge walioshinda uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni hususan wa Chama Tawala CCM na mimi naungana na walionitangulia kuchangia kwa kuipongeza Serikali kuondoa kodi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kodi hii ilikuwa inanyanyasa wananchi na mara nyingi ilikuwa Halmashauri zetu katika msukosuko mkubwa sana wa wananchi na mwisho hatma yao wanasiasa, ilikuwa inalegalega kutokana na ukusanyaji wa kodi ya aina hiyo. Lakini pamoja na hayo naomba Serikali ifanye jitihada zake zote kwa makini iweze kufidia pengo hilo haraka iwezekanavyo kusudi mipango ya maendeleo katika Wilaya zetu iweze kuendelea kama ilivyokuwa hapo awali au iwe na kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumwomba Waziri wa Fedha, ajaribu kudhibiti kodi nyingine ambayo inaitwa kodi ya majengo.

tumechukua *THB* na tunaishi humo, tulianza kulipa shilingi 15,000 kuna majumba sasa hivi yamefikia shilingi 50,000, kuna majumba yamefikia zaidi ya shilingi 100,000 naona hapana uhalali hasa zile nyumba ambazo wenye we tunaishi. Kama ikibidi basi tulipe angalau iwe shilingi 20,000 au shilingi 15,000, kama ilivyokuwa pale awali. Kwa mfano, Dar es Salaam nyumba ziko nyingi tu wakikusanya shilingi 10,000 kwa mwezi zitakuwa fedha nyingi tu. (*Makofi*)

Vile vile naipongeza hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kuwalipa mishahara Watendaji wa Vijiji. Lakini huo ni mwanzo mzuri, napendekeza pia Waziri uone uwezekano wa kuanza kuwalipa pia Madiwani wetu katika Halmashauri. (*Makofi*)

Pia napongeza hatua ya Serikali ya kuona baada ya kuathirika kwa hali ya hewa katika nchi yetu na kuwa na upungufu wa chakula kutenga fedha kiasi kikubwa kwa ajili ya kununulia chakula. Lakini la muhimu katika suala hili ni kwamba hicho kipatikane mapema iwezekanavyo ili kiweze kuwafikia walengwa haraka kabla ya maandalizi ya msimu ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha kilimo tunashukuru hatua zote zilizochukuliwa. Lakini nataka kumtahadharisha Waziri, kwamba kuboresha kilimo kijumla kusema kweli haitatusaidia kila Wilaya. Kwa mfano, Wilaya ya Liwale ina eneo la *square km* 39,000. Asilimia 53 ya eneo hili imezungukwa na mbuga za wanyama. Unapozungumzia kilimo katika Wilaya ya Liwale lazima uzungumzie pia ma-game

scout katika Wilaya ya Liwale. Vinginevyo inavyojitokeza na hali ilivyo kwa Liwale ni ngumu sana. Hata kidogo kile kilichokuwa kimepatikana wakati ule mvua ilipokuwa haitoshi kimeliwa na wanyama pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wamezagaa Wilaya nzima, Vijiji 42. Hata mkituletea Maafisa wataalam wa kilimo 2,000, kama hili baa la wanyamapori halitaweza kuzingatiwa kikamilifu na Serikali na ikibidi iweke mkakati wa kuweka kabisa pesa za kuweza kuajiri *Game Scouts* wapatao 42 ili kila Kijiji waweze kuwa na *Game Scout*. Hivyo ndivyo ilivyo kuwa wakati wa ukoloni na wakati wa Awamu ya Kwanza. Sisi tulikuwa hatuna Askari Polisi, askari wetu walikuwa ni *Game Scouts* na hili wakoloni waliliona kwamba eneo letu lina wanyamapori ambao wanahitaji kudhibitiwa ili wananchi waweze kuishi kwa usalama. (*Makofi*)

Ningeweza tu kunukuu takwimu ambazo tukiacha mashamba yote kwamba sasa hivi yameliwa na tembo, lakini pia wananchi kadhaa wamepoteza maisha yao. Kuanzia mwaka 1996 mpaka 1999 wananchi waliouawa na wanyama wakali au wanyama wa porini wanapata 43 na wale wanaojeruhiwa wanapata 40. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba la msingi kama mnataka kilimo kifanikiwe kila Wilaya, basi tutafute mazingira ya kila Wilaya ilivyo halafu tuweze kuweka mikakati ya pamoja kwa kumshirikisha Waziri wa Utalii au Waziri wa Maliasili pamoja na Waziri wa Kilimo na Chakula, ili tuweze kulima vizuri katika maeneo yetu hasa ya Liwale na tuweze kuvuna vizuri. Tembo sasa hivi wanakula hata korosho, kwa hiyo, hata yale mazao tunayodhania kwamba tungeweza kunufaika nayo kwa kuuza, pia hayo yanaathirika vibaya sana na wanyama hao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri uitazame Liwale kama hivyo ilivyo kwa kuangalia kwamba kama tunahitaji kuboresha kilimo, basi tuboreshe usalama wa wananchi wanaolima, usalama wa mazao yanayolimwa na pia kudhibiti wanyama. Kilicho jitokeza ni kwamba, kuna mradi wa wanyama wa *Selous*, lakini hakuna mradi wa kuwatunza wananchi wasiathirike na wale wanyama. Sasa nilidhania ni wakati muafaka wa kuliangalia hili kwa ngazi ya juu tukaweza kupata *solution* ambayo itawafanya wana Liwale waweze kujumuika na wenzao kwingine kote kwa kuleta maendeleo kwa Tanzania na pia kwa Wilaya yao.

Pia kuhusu ushuru wa dawa ya mbu pamoja na chandarua, kusema kweli mimi ni mionganoni mwa watu tunaopata shida sana na matatizo ya Malaria katika Wilaya yangu. Huo ndio ugonjwa pekee ambao unasumbua sana wananchi kiasi kwamba wengine wanashindwa kufanya shughuli zao za kawaida za kuwaletea maendeleo. Kwa hiyo, ningeshauri pawe na punguzo la kodi katika chandarua pamoja na dawa ya mbu kwa manufaa ya wananchi wa Liwale pamoja na Tanzania nzima kwa ujumla. (*Makofi*)

Ningependa pia kuchangia upande wa ubinafsishaji. Kwa mazingira ya Tanzania ubinafsishaji ni kunyume cha kutaifisha. Wakati wa Awamu ya Kwanza tulikuwa na zoezi la kutaifisha Makampuni, majumba na kadhalika. Zoezi hili lilikuwa limefanyika vizuri sana kwa maana kwamba lilikuwa la uwazi kabisa na kile kilichokuwa kinataifishwa kilikuwa kinaleweka kinakuwa ni mali ya umma, *full stop* na si vinginevyo. Palikuwa na miiko mizuri tu ya kufanya kwamba hakiwezi kutaifishwa kitu kile kwa manufaa ya watu wachache wa aina fulani. Kwa bahati mbaya kabisa wakati tunahitaji kubinafsisha, miiko ya aina hiyo ama haipo au hatujui. Sasa matokeo yake ni kwamba inapotokea migogoro katika kubinafsisha hapo ndipo wananchi wanakuwa na wasiwasi na zoezi zima. Wanakuwa na hofu na mawazo potofu. Sasa hili suala sio zuri. Mimi nadhani katika suala la kubinafsisha, hata kama tumefikia hatua karibu ya mwisho, lakini ingekuwa vizuri mikataba yote ikapitia Bungeni na tukashirikishwa kwa uwazi zaidi ili kuondoa wasiwasi huu ambao wengine wanakuwa nao. (*Makofi*)

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika zoezi hilo la kubinafsisha, lakini mimi nadhani kigezo cha kufanikiwa kisiwe peke yake. Ongezeko la kodi kama vile tunavyopata *TBL* na sehemu nyingine, mimi nadhania tuendelee mpaka huko ndani kujuu nini kinachofanyika kwa kuwa kuna mashirika kadhaa ambayo yamebinafsishwa, mimi nadhani kama yana matatizo au yameanza kwa matatizo kwa mfano *ATC*.

Mimi nimesafiri na *ATC* mara nne. *ATC* ya zamani ilikuwa sina sababu ya kubeba kipepeo kujipepea kwa muda wa dakika tano kabla ndege haijaruka. Lakini sasa hivi huo ndio mtindo. Ukiingia ndani ya ndege ya *ATC* ya sasa hivi ambayo tayari tumeshafanya ubinafsishaji unakwenda na kipepeo, dakika tano za mwanzo lazima ujipepee. Mpaka ikipaa juu ndipo inapokwuwa *full enough* kiasi cha kwamba

huhitaji tena kujipepea na dakika tano za kushuka pia hali inakuwa hivyo. Sasa *that is punishment*. Kwa hiyo, vitu kama hivyo vingetakiwa kurekeblishwa au vifuatiliwe kikamilifu.

Takwimu zinazungumzia kwamba viwanda vilivyobinafsishwa 51% ingekuwa vizuri takwimu zikaelezea zaidi ni viwanda vipi. Inawezekana viwanda hivi ambavyo viko mikononi mwa wananchi au Watanzania ni viwanda uchwara. Ni vipi hivyo? (*Makofi*)

Kabla *TTCL* kubinafsishwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, aliniahidi kwamba katika Wilaya yangu tutapata simu kabla ya mwaka 2003. Baada ya kubinafsisha, kusema kweli mimi na wananchi wangu wa Liwale tumefikia hatua ya kukata tamaa. Pamoja na Uprofesa wake Mheshimiwa Mwandosya, nikimwuliza hana jibu kamili kuhusu suala hili. Sasa hapo ndio inatupa wasiwasi sisi wengine. Kulikoni katika kubinafsisha? Tunategemea kupata matunda, matunda yake ni yapi? (*Kicheko/Makofi*)

Tatizo lingine la kubinafsisha ni kwamba hata kwenye *NMB*, *NMB* zipo mpaka Vijijini, tuseme mpaka Wilayani. Wasiwasi tulionao ni kwamba endapo ikibinafsishwa kitakachotokea ni kwamba zile zilizoko Wilayani zitafungwa. Sasa zikishafungwa zilizoko Wilayani ni kusema wananchi sasa Wilayani watapata shida sana na wao wanacheza mchezo katikati ya sherehe kwamba *80 percent* ya *business* iko katika Miji Mikuu pamoja na Mikoani. Lakini sisi kisiasa *80 percent* ya uhai wa Chama upo kwenye Vijiji pamoja na Wilaya.

Sasa lazima pawe na mikakati ya kuwawezesha hawa kama tutabinafsisha Benki kama hii lazima hizi Benki ziwepo huko Vijijini kwa manufaa ya wananchi. Kama Wilayani, basi zisitoke Wilayani. Vinginevyo hata bei, nani atakwenda kuchukua pesa Makao Makuu ya Mkoa kupeleka Vijijini kwenda kununua mazao, kama pesa au mishahara inayokwenda Polisi inaibiwa? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa hali kama hii ndiyo tunayoogopa. Sio kwamba mtu hataki, hapana. Mimi niko radhi lakini pawepo na utaratibu wa kuweza kuwafunga hawa kwa manufaa ya wananchi, vinginevyo tutacheza huu mchezo wa kubinafsisha kama ni viwanda vilivyoko huko Wilayani, vitafungwa, vitabakia vya Mijini mpaka Mikoani kiasi cha kwamba kule Vijijini ndio wasahau kabisa na wale wananchi ambao wametuchagua kule na kura zote ambazo tunazipata kwa wingi zinatoka kule Wilayani ambako tukibinafsisha baadhi ya Makampuni yaliyoko Wilayani yanafungwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa hilo. (*Makofi*)

Kuhusu mazao, kusema tuchague zao moja moja la biashara na la chakula, kusema kweli kwa eneo kama Liwale kama nilivyosema eneo letu ni kubwa sana. Kuna maeneo ukipanda korosho zinastawi na ndipo unapoweza kupata zao la biashara na kuna maeneo unaweza kupanda ufuta. Kwa hiyo, nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba mimi nitakwenda kuwashimiza wananchi wangu kupanda mazao yote ambayo yanakubalika na yatapatikana kila mahali. Wazo la kusema liwe moja, kusema kweli sitakwenda nalo kwa kuwa nitakosa kura zangu. (*Kicheko/Makofi*)

Baada ya kusema hayo, naomb a tena kuunga mkono hotuba zote mbili, kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. JUMANNE H. NGULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi mbili zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia, naomba basi na mimi njumuike na wenzangu katika kuwapongeza na kuwakaribisha Wabunge wapya ambao wameingia baada ya kushinda chaguzi ndogo ambazo zimefanyika. Nawatakia kila la kheri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwapongeza hao, naomba pia nimpongeze ndugu yangu pale, jina bado sijalipata vizuri ambaye amechaguliwa kuwa Kamishna wa *TRA*.

MBUNGE FULANI: Kitilya.

MHE. JUMANNE H. NGULI: Kitilya ehee! Naomba nimpongeze kwa kuchaguliwa kuwa Kamishna wa Mamlaka yetu ya Mapato kwa sababu kwa kweli ndiyo ambayo sasa hivi inatufikisha katika hali hii ya maendeleo yetu katika Tanzania. Nampa hongera sana na afanye kazi ya ziada kushinda hii ambayo imetufikisha hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba basi na mimi niweze kuishukuru Serikali katika kufanya maamuzi muhimu ambayo kwa kweli ni ya kihistoria katika nchi yetu.

Mwaka 2002 Serikali ilifanya maamuzi ya kusamehe ada ya Shule ya Msingi, ni maamuzi mazito na ni muhimu kwa sababu tunajua kwamba kuna shule nyingi na kwa kweli fedha iliyokuwa inatolewa kama ada ilikuwa nyingi. Mwaka 2003 pia Serikali imekuja na maamuzi muhimu tena ya kusamehe kodi ya maendeleo. Nasema kwa kweli inastahili kupata sifa na hongera sana kwa maamuzi ya namna hiyo. (*Makofi*)

Ndugu zangu, kodi tangu siku nyingi au tangu nyakati zile za Manabii kama akina Yesu kule nyuma, haikuwa ni kitu ambacho kilikuwa kinapendwa. Kwa hiyo, ni kila wakati kodi inachukiwa. Watu walimwuliza Yesu wakati ule wakamwambia hivi, unatuambia kwamba tutoe zaka, tutoe sadaka, lakini pia na Kaizari anatutaka tutoe kodi. Ni lipi sasa ambalo tulifanye ambalo ni halali? Aliweza kuwajibu akionyesha kwamba yote yalikuwa ni halali kwamba ya Kaizari mpe Kaizari na ya Mungu mpe Mungu. (*Makofi*)

Lakini hii imeonyesha nini ndugu zangu? Imeonyesha kwamba kodi haikuwa ikipendwa wakati wote. Maana watu walikuwa wanajaribu kukwepa kwa kila namna, kujaribu kutafuta ni namna gani waepukane na kodi. Lakini kwa sababu tunahitaji kuendeleza nchi yetu, wakati wote kodi nayo imekuja ni halali kwa ajili ya maendeleo ya nchi zetu.

Kwa hiyo, naomba katika kuijewa katika hali hii ya kufuta kodi, iwe ndio changamoto ya kutufanya tufanye kazi. Katika Vijiji vyangu vya Singida Mjini, wananchi wake wengi ni wafanyabiashara ndogo ndogo. Wananchi hawa huamka asubuhi saa 12.00 wanakimbia wanakwenda Mjini, wanapelea chochote walichonacho. Wanapelea ndizi, nyanya, kuni, mkaa na kadhalika kwenda kufanya biashara na wanarudi jioni labda kwenye saa 1.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nafanya ziara hapa juzi juzi kwenye mwezi Mei, nilipambana na maswali magumu sana juu ya kodi. Watu hawapatikani ili waweze kulipa kodi, badala yake Afisa Mtendaji wa Kata aliamua kuanza kuwasaka watu kulipa kodi usiku kwenye saa 2.00, saa 3.00 usiku wakati watu wanajitayarisha sasa kulala, Afisa Mtendaji anafika. Masuala hayo niliyapata na kwa kweli yalikuwa ni magumu sana kuweza kuyajibu. Lakini wameshukuru sana. Mheshimiwa Waziri alipozungumza hili, simu nyingi sana nimezipata wakashukuru sana juu ya kusamehewa kwa kodi na hivyo kuachana na matatizo haya ya kusakana usiku ili waendelee na kuzalisha angalau kile kidogo kwenda kuuza sokoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kwamba ni lazima sasa Serikali iangalie hali ya ufanyaji kazi wa Watanzania wetu sisi, kwa sababu haya nasema ni maamuzi muhimu na magumu. Si maamuzi ya lelemama tena kukaa bila kufanya kazi. Niliangalia katika kitabu chetu cha hali ya uchumi wa Taifa 2000 ukurasa wa 97 inaonyesha jinsi pia uwekezaji au mgawanyo wa uwekezaji katika nchi yetu ulivyo. Sasa nikiangalia katika hali hiyo, mgawanyo huu kwanza ukiuangalia unakuta uko upande mmoja. Miradi ambayo imewekezwa kwa mfano katika Miji yetu au katika Mikoa yetu, Dar es Salaam unakuta kuna miradi 191, Arusha miradi 62, Mwanza 14, Tanga 10 na kuendelea.

Lakini unafika mpaka Singida unakuta kuna miradi miwili na sikumbuki ni miradi ya nini. Unakuta Mikoa mingine mradi mmoja na Mikoa mingine hakuna hata mmoja. Sasa hii inaashiria nini ndugu zangu? Inaashiria hali ya Mikoa mingine kwenda kasi na Mikoa mingine kuendelea kubaki hivyo hivyo. Lakini wote katika nchi hii tumesamehewa kodi, lakin Mikoa mingine sasa hivi inapata *push-up* nzuri ya maendeleo. (*Makofi*)

Sasa niiombe Serikali katika hili kwa sababu vinginevyo tutajikuta tunaachana kwa hatua kubwa sana ya maendeleo Mkoa hadi Mkoa. Niiombe Serikali basi katika Mikoa hii ambayo uwekezaji wake ni

mdogo, aidha, inawezekana wanachagua kwa sababu mbalimbali za kihistoria, za hali ya hewa na nini, lakini naomba Serikali yenye iangalie kwa sababu hii nchi yenye ndio yenyewe kuamua. Iangalie kupeleka au kuwezesha kuweka hali nzuri ya kuweza kufanya watu au wawekezaji wapende sehemu nyingine pia kuwekeza. Kama sio hivyo, iwawezeshe wananchi wa Mikoa hiyo kuwawekea hali nzuri ya kuweza kujipatia maendeleo wenyewe. (*Makofi*)

Nashukuru Serikali pia katika kuweka hali ya miundombinu kwamba barabara kuu sasa imeanza kujengwa. Uwanja wa ndege nimeangalia nimeona Serikali imeendelea kutenga fedha ili uwanja wa ndege wa Singida nao uendelee kukarabatiwa. Lakini nimeangalia katika utengenezaji wa reli yetu, sijaona. Labda Mheshimiwa Waziri baadaye anaweza kunielekeza, lakini reli hiyo kwa kweli bado sasa hivi tunakwenda kwa kudra ya Mwenyezi Mungu. Bado si nzuri. Bado mataruma mengine madogo, mataruma mengine makubwa na kila wakati tunapewa kichwa ambacho ni kidogo kinachowenza kuhimili au ambacho kinahimiliwa na yale mataruma. (*Makofi/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni kipana. (*Kicheko*)

Ninachowenza kusema ni kwamba kule bado reli sio imara na sisi ni moja ya miundombinu ambayo inatusaidia sana na inatusaidia katika kuwawezesha wananchi wetu hata kwa kile kidogo ambacho wanakizalisha na kingine ambacho wanapata kutoka Dar es Salaam kwa ajili ya biashara kiweze kutufikia kwa urahisi.

Nakumbuka wakati wa *El-Nino*, ilibakia ni reli peke yake iliyoweza kutuokoa. Sasa reli ambayo bado iko katika hali hiyo Mheshimiwa Waziri naomba na hiyo pia iweze kutengewa fedha ili iweze kuendelea kuimarishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia pia kwa upande wa umaskini aidha wa kipato, kwa chakula na fedha taslimu, mwaka 1991/1992, mpaka 2000/2001 kilipungua kwa kiasi cha kutoka asilimia 21.6 mpaka asilimia 18.7 kwa upande wa chakula na mahitaji muhimu kilipungua kwa asilimia 38.6 mpaka 35.7. Huu ni wastani wa asilimia kama 2.9 hivi kwa kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii ambayo ndio tumefuta kodi, tumefuta ada, tunataka nchi iendelee. Kwa ukuaji huu naona ni ukuaji kidogo ambaao haustahili kwa kweli kuendelea kuwa katika hali hii. Sasa naomba basi na ukuaji huu ukiuangalia upo zaidi au pungufu, upo zaidi Mijini. Asilimia kubwa ya jinsi umaskini unavyopungua ni Mijini na ndio maana inawafanya hata vijana kukimbilia Vijijini kuja Mjini. Ni kwa sababu wanaona hali ni nzuri. Lakini Mjini sasa tunakimbilia wakati hakuna kazi, hakuna shughuli ya kufanya, kwa hiyo tunaongeza idadi ya walaji, tunapunguza tena kasi ya kupunguza umasikini.

Sasa naiomba Serikali, pamoja na kuweka fedha kwa ajili ya kilimo, lakini ihakikishe mazingira mazuri yanawekwa Vijijini ili wananchi waache kukimbilia Mijini. Itawezesha kuongeza uzalishaji badala ya kuongeza ulaji wakati uzalishaji hamna. Kidogo kinachozalishwa tunachangia kwa wingi. Kila wakati tunatakiwa kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo naomba nichangie lingine la mwisho. Hili la mwisho si lingine, ni upotevu wa fedha za Serikali na matumizi mabaya ya fedha hizo za Serikali. Sasa hivi tunaisifu Bajeti nzuri namna hii. Pesa zinatengwa nzuri, zinakwenda katika miradi mbalimbali, lakini tunajikuta wapo nao ambaao sasa hivi wanafurahia pesa nyingi kwenda katika miradi hii. Wana mipango yao makusudi katika kuweka matumizi mabaya au katika kujilipa bila nyaraka zinazotakiwa.

Namshukuru Mhasibu wa Serikali, kwa juhudhi alizozichukua katika miaka miwili hii katika kuboresha hali ya uhasibu na katika kuboresha matumizi mabaya ya fedha za Serikali lakini hiyo bado. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mkemia.

MHE. JUMANNE H. NGULI: Mkemia. (*Makofi*)

Lakini hiyo bado. Ndugu zangu pesa zinazopotea kwa matumizi mabaya ni nyingi mnaji. Tunajiwekeea shilingi 10 lakini unakuta shilingi nne zinakwenda kwa matumizi mabaya. Hii miradi yetu kweli itafika?

Namwomba Waziri awe mkali zaidi, adhibiti zaidi ili fedha za Serikali tunazositenga, basi zifanye kazi inayodhamiriwa, ili tuweze kusonga mbele na tukiendelea kufanya lelemama namna hii wakati tumefuta kodi, tumefuta ada, tutakuja kujikuta katika hali mbaya zaidi, ya aibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo na baada ya kengele ya kwanza kulia, kuniambia kwamba muda umekwisha, naomba basi nishukuru kwa nafasi hii na ninaomba kuunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. OSCAR T. MLOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho jioni hii kuchangia hoja iliyoko mezani kwetu kuhusu Bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa na Mawaziri wawili wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Iakini pia nichukue nafasi hii nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wabunge wenzetu wapya ambao wamefika Bungeni humu kupitia chaguzi ndogo zilizofanyika mwezi Mei mwaka huu wa 2003.

Napenda niwapongeze sana na niwaarifu tu kwamba, wafahamu kwamba wana dhamana waliyopewa na wananchi kwenye Majimbo yao. Hivyo nawaomba wazingatia dhamana hiyo na ahadi kwamba watawatumikia kwa uadilifu mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili walitota hoja iliyo mbele yetu kwa hotuba nzuri ya Serikali iliyowasilishwa wiki iliyopita na ambayo tuko kwenvye mijadala nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba zote mbili za Fedha na Mipango na Ubinafishaji zimepewewa mwelekeo mzuri wa ukuaji wa uchumi wetu ambao sasa unasemekana kuwa kwenye asilimia 5.6 ukilinganishwa na ule wa nchi za Kiafrika ambazo ziko kwenye wastani wa asilimia 3.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika hii inatia moyo sana pamoja na kwamba mimi naiona ni yakinadharia kwa sababu labda pengine kwa kuwa mimi kitaaluma sio Mchumi, mimi ni Mhandisi, inanipa taabu kidogo kujua hili hasa kwa sababu Morogoro na Dodoma ni pua na mdomo.

Kwa hiyo, wakati Waziri anawasilisha hotuba hii, wapiga kura wangu wa Morogoro Mjini walikuwa hapa wakisikiliza wakanitwisha mzigo wa swalı kwamba hivi hii asilimia unayosema imeongezeka ya ukuaji wa uchumi ikoje? Inatusaidia nini sisi watu wa kawaida? Sikusita kumwambia kwamba hivi hukusikia kwamba tumeondolewa kodi kadha wa kadha ambazo zilikuwa ni mzigo na kero kwetu na kwenu ninyi wananchi? Akanielewa. Nilishukuru sana. (*Makofii*)

Akanibebesha swali lingine ambalo linaonyesha kwamba hakuridhika na jibu lile nilolomba kwamba ah, lakini Waziri pia amesema kwamba shilingi yetu imeporomoka vibaya sana toka shilingi 800/= kwa Dola sasa iko kwenye 1,040. Hivi hii maana yake nini? Ni kwamba haina uhusiano na ukuaji huu wa uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mbunge ni mwakilishi wa wananchi si vizuri ukatoa jibu la kubabaisha. Nikasema mimi kama mwakilishi natakiwa nipeleke Bungeni mambo ambayo nimetumwa na ninvi wananchi.

Hivyo hili ni moja kati ya masuala ambayo nitayapeleka nikamwulize Waziri, hivi huku kuperomoka kwa shilingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja na huu ukuaji wa uchumi wetu? Kwa hiyo, naleta mbele yako Mheshimiwa Waziri, ili badala ya kukuletea wewe kama swali Bungeni basi ukalifafanua hapa ili wote tuptate kulielewa kwa uzuri zaidi. (*Makofii*)

Lakini niseme lingine tu kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata uhuru mwaka 1961 tumekuta thamani ya shilingi yetu ilikuwa inafananishwa na dola ya Kimarekani kwa shilingi 7 na

imeng'ang'ania hapo si chini ya miaka 15 mpaka katikati ya miaka ya 1970 imeendelea kuwa shilingi 7. Nilikuwa najiuliza hivi kuna siri gani hapa ambayo ilitumiwa mpaka ikabaki hivyo. Lakini ilianza kuporomoka nadhani mwishoni mwa miaka ya 1970 hasa baada ya nchi yetu kupata mtafaruku wa kuingiliwa na Nduli Iddi Amin, ambaye alimega kipande cha ardhi yetu na tukaamua tujitoe mhanga tuweze kurudisha pale, ndipo ilipoanza kuporomoka mpaka ikafikia hapa tulipo.

Lakini asubuhi Mheshimiwa Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa John Mwakipesile, alisema amepata fununu kwamba Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuiacha shilingi ishindane na soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona hii kama ni sawasawa na kuchezea shilingi kwenye shimo la choo. Kwa sababu hata siku moja thamani hii ilikwisha kuwa imeenda huko ilikoenda, haitarudi nyuma. Maana yangu ni kwamba hatutarudi kwenye shilingi 7 ile ya mwaka 1961 tulipopata Uhuru. Sasa viptuanze kuichezea? Kama iko namna ya kuweza kuisimamisha walau basi ibaki hapo hapo ilipo isiendelee tena. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi, kama tukiiacha katika utaratibu huu itafikia wakati dola ya Kimarekani tutabidalisha kwa shilingi milioni moja. Hatuna kapu la kubebia shilingi hizo ili tukabdalishie Benki tupate dola ya Kimarekani kwa kiwango hicho. Naomba sana ikiwezekana kama kuna namna yoyote ya kuifanya hii shilingi isizidi kuporomoka basi tuishikilie hapo ilipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ile changamoto iliyotolewa kuwa kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi atimize wajibu wake kwa bidii zake zote na ufanisi mkubwa ikiwezekana uwe wa kuigwa.

Napenda kumpongeza Waziri mtoa hoja kwa kuweka upendeleo wa makusudi kabisa wa mgao wa fedha za Bajeti kwenye mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini walio nao wananchi wetu. Kwa hakika mkakati huu siyo wa kinadharia tena kama nilivyokuwa nazungumzia hapo awali kuhusiana na kukua kwa uchumi. Kwani tayari sasa matunda yameshaanza kuonekana katika nyanja mbalimbali. Nyanja kama Elimu ya Msingi, tunayaona. Sekta ya Afya, Maji, Barabara tunayaona yakiwa yanatekelezwa.

Kwa hiyo, kwa kweli hapa tumefika mahali ambapo tunapaswa tujivunie na kwa kweli hili ni jambo la kujivunia kubwa sana kwa Serikali yetu inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyanja ya Kilimo, nilipenda nipongeze sana busara za Serikali zilizotumiwa kuchanganua au kuchagua maeneo machache ambayo yatarewa au yamepewa kipaumbele katika Bajeti hii ili kupanua uchumi na kwa kweli niseme uamuzi huu ni uamuzi wa kisayansi kweli kweli. Kwa sababu hakuna mtu yeoyote ambaye atakataa kwenye usemi kwamba kilimo ni moja ya sekta muhimu sana inayobeba dhamana ya Watanzania walio wengi zaidi ya asilimia 80 na kama tutaitumia kikamilifu kama walivyosema Wajumbe wengine tukatumia ardhi tuliyonayo kwa umwagiliaji tusingoje kudra ya Mwenyezi Mungu kupata mvua. Nina hakika pia tunaweza tukasaidia Pato la Taifa kuchangia kwa asilimia isiyopungua 50 kwa fedha za kigeni.

Lakini niseme tu ni vyema na Waziri amelibaini hili kwamba tatizo letu kubwa hapa ni kujielekeza katika usindikaji wa mazao haya badala ya kuyapeleka na kuyauza yakiwa ghafi kwa sababu tunachokipata itakuwa ni kidogo sana kuliko tukiyasindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri kwamba tunayo ardhi kubwa ambayo hajatumika kikamilifu kwa kilimo lakini kwa maeneo ya mijini ambako mimi ni mmoja kati ya wale tunaoyawakilisha, tunayo nguvu kazi ya vijana kubwa sana. Lakini nguvu kazi hii haitumiki kikamilifu kwa sababu vijana wetu wanapenda biashara zaidi kuliko kilimo. Hivyo utakuta tunaipoteza bure hkini niseme kwamba hivi majuzi katika muda wa miezi mitatu, minne, iliyopita pale Mjini Morogoro na eneo la jirani la Wilaya mpya ya Mvomero, kumegunduliwa machimbo ya madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha ugunduzi huo pale mjini tumpemata amani kubwa sana na tulikuwa tunalala usingizi kwa sababu vijana wote ambao walikuwa ni kero pale mjini walihamia kwenye machimbo hayo, kila mtu kwa biashara ya aina yake. Wako wanaouza bia kule, wako mama ntilie

kule kwenye machimbo. Kwa kweli kulikuwa hakuna unyang'anyi au wizi hata ujambazi ulikuwa umefifia. Kwa sababu kumbe wamepata mahali ambapo wameweza kujipatia ajira ya namna yake.

Mimi niombe Wizara yenye dhamana ya madini. Kwanza, niwashukuru sana kwamba kuna wakati walitugawia vitabu vinavyoonyesha maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambayo yana madini mbalimbali. Lakini nina hakika kwa ugunduzi huu unaofanyika sasa na wananchi wa kawaida ni kwamba bado tunayo maeneo ambayo hayajagundulika. Sasa kwa Morogoro nilikuwa naomba nitoe ombi mahsuswi kwamba watuletee wataalam waliobobe ili waweze wakatubainishia kwenye maeneo haya ambayo yamegundulika na wananchi kwamba kuna dhahabu hii ipo kwa kiwango gani, kiasi gani kipo na imefuata mkondo gani kwa sababu maeneo haya mawili yaliyogundulika ya Mindu na Melela, yameachana kwa umbali kama wa kilomita zisizozidi 10. Nahisi kwamba pengine ni mkondo huo ni mkondo mmoja basi tuweze tukayatafuta upande ule ambao haukuingiliana.

Bahati mbaya sana machimbo ya Mindu walipoyagundua yameingiliana na miundombinu ya Serikali, kuna miundombinu ya Taifa, kama barabara ya *TANZAM* inapita pale, kuna gridi ya Taifa ya umeme inapita pale, bomba la mafuta la *TAZAMA* linapita pale. Mbaya zaidi kuna chanzo kikuu cha maji ya mji wa Morogoro ambacho kinalisha mji ule kwa asilimia 75. Si rahisi kuweza kuyapuza yote hayo na ndiyo maana Serikali ya Mkoa iliamua kusitisha uchimbaji ule ambao ulikuwa unafanyika. Lakini tunathamini ule mkondo umeelekea wapi ili hatimaye watu waweze kupewa *Prospecting Right* ya uchimbaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naona kengele imeshagonga, basi napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi ninaowawakilisha wa Jimbo langu la Morogoro Mjini, kwa utaratibu walioweka mezani katika kurekebisha vianzio mbalimbali vyta mapato katika Halmashauri zetu na kuondoa kabisa ile kodi ya maendeleo ambayo ilikuwa ni kero ukusanyaji wake na kwa kweli niseme kodi hii ya maendeleo pamoja na jina lake kuwa kubwa na zuri sana. Lakini haikuwa inatumika kuleta maendeleo ambayo yalikuwa yanakusudiwa.

Kodi nyingi utakuta zilikuwa zinatumiwa aidha, kulipa mishahara au posho ya wale wanaokusanya. Ni kiasi kidogo sana kama kitakuwa kinapatikana cha kuweza kusaidia maendeleo ambayo yamekusudiwa. Kwa hiyo, nina hakika hili litakuwa limetuondolea kero lakini litazidisha wigo wa maendeleo yetu kwa kuwaelekeza wananchi sasa wafanye kazi wasiogope kushikwa au kufukuzwa mabarabarani kudaiwa kodi hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo niseme kwamba naiunga mkono hoja hii mia kwa mia.
(*Makofit*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge, nataka tuijiweke sawa kwa jambo moja ambalo limetokea wakati Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, akichangia na baada ya Mheshimiwa Soud kumtaja na kumshambulia Ndugu Sanare, niliona wengi wanaanza kama kukunja nyuso na hatimaye Mheshimiwa Jackson Makwetta, akaomba kuhusu utaratibu.

Sasa taratibu zilizopo katika Kanuni zetu zinasema, Kanuni ya 55, fasili ya kwanza inasema: "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu, lakini Mbunge anapofanya hivyo itabidi ataje Kanuni ya Bunge inayokiukwa."

Naomba nisisitize kwamba kwa leo tuliona tulikuwa na mazoea haya. Ni vizuri tukasoma Kanuni Waheshimiwa Wabunge, ili unaposimama ukataja na Kanuni na huo ndio utaratibu.

La pili, ni Kanuni ya 50 fasili ya sita, inasema: "Isipokuwa tu kama kunatolewa hoja mahususi kuhusu jambo kama lilivyotajwa huko juu. Itakuwa ni marufuku kwa Mbunge ye yeyote katika mijadala wowote Bungeni kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Wabunge, Majaji, Mahakimu au watu wengine wanaoshughulikia na utoaji wa haki."

Waheshimiwa Wabunge, tunajua Ndugu Sanare, alikuwa ni Kamishna Mkuu. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo yalikuwa mezani pake akitoa haki na kwamba itakuwa ni kinyume cha utaratibu wa

Bunge kugusia mienendo ya watu hao waliotajwa wakati wa hoja yoyote au kupitisha hoja na hivi, kuuliza maswali au wakati wa kutoa maoni juu ya hoja inayohusu jambo lolote.

Kwa hiyo, kwa bahati nzuri hata Mheshimiwa Spika, alipokuwa akitoa adhabu kwa Wabunge wale wanne na tukatoa na adhabu ya kuandikiwa onyo kali kwa mtumishi wa Bunge. Lakini Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka Spika, alisema kwa sababu yeye hawezi kujitetea hapa, si vyema sisi Bunge tukatoa hukumu hiyo. Ni vizuri ipelekwe kwenye Tume inayohusika na kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, tumefanya naye mawasiliano tulikubaliana. Kwa hiyo, naona tulifikia mahali pazuri.

Waheshimiwa Wabunge naona shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zimeisha. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
Tarehe 18 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*